ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Tano – Tarehe 17 Disemba, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 32

Upotevu wa Upanga wa Dhahabu wa Polisi

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Hivi karibuni baadhi ya vyombo vya habari hususan magazeti viliripoti juu ya upotevu wa upanga wa dhahabu aliopewa *IGP* Said Mwema kwa niaba ya Jeshi la Polisi la Tanzania wenye thamani ya shilingi milioni mia sita (600,000,000/=). Kadhia hii iliyozagaa hapa nchini imetoa picha mbaya kwa Jeshi la Polisi na vyombo vyengine vya ulinzi na usalama.

(a) Je, serikali inaweza kutueleza ukweli wa kadhia hii.

(b) Kama upotevu huo upo. Je, ulipotea katika mazingira gani.

(c) Je, ni kweli ulipotea chini na ndani ya mikono ya Jeshi la Polisi Zanzibar kupitia Kamishna wake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 32 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ninakiri kutokea kwa kadhia ya upotevu wa Upanga wa Jumuiya ya Jeshi la Polisi la Nchi za Kusini mwa Afrika *SARPCCO* katika ardhi ya Tanzania. *(Makofi*)

(b) Bado uchunguzi unaendelea kubaini upotevu huo ulitokea wapi na wakati gani, ama wakati wa kuweka upanga huo kwenye *box* au wakati wa kuusafirisha kutoka hapa Zanzibar kwenda Dar-es-Salaam au baada ya kufika Dar-es-Salaam.

(c) Mpaka sasa hakuna ushahidi au uthibitisho wowote uliobaini kwamba upanga huo ulipotea ndani ya mikono ya Jeshi la Polisi Zanzibar. Hata hivyo, jitihada zinaendelea za kutafuta upanga huo na wahusika watapambana na mkono wa sheria na tayari upanga mwengine umeshatengenezwa baada ya ule uliopotea. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu ya Mhe. Waziri, naomba niulize swali la nyongeza lenye vifungu vya (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mhe. Waziri, amekiri kwamba upanga huo wa thamani umepotea katika hali ya kutatanisha. Vile vile, mpaka leo bado hatujajua nani aliyepoteza upanga huo na kwamba vyombo vya habari viliripoti kwamba upanga huo ulipotea katika mikono ya Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar.

a) Je, hatuoni kwamba kutangazwa kwa kadhia hii ndani ya mikono ya Jeshi la Polisi Zanzibar kupitia Kamishna wetu, si kutafuta mwanya wa kumnyang'anya madaraka na kuoneshwa kwamba Wazanzibari hawawezi kuwa viongozi wa Jeshi la Polisi.

b) Juzi Mhe. Rais, amefanya mabadiliko ya Jeshi la Polisi na Kamishna Mussa Ali, sasa amekuwa Kamishna wa Polisi Jamii Tanzania. Mhe. Mwenyekiti, hiyo nadhani ndio sababu tosha iliyomfanya ashushwe hadhi hiyo ya Kamishna Zanzibar. *(Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ninaomba lile swali la kwanza Mhe. Mjumbe alirudie, ili niweze kulifahamu vizuri, kwa sababu sikumsikia vizuri na pia azungumze karibu na *speaker*, kwa ajili ya kutusaidia kusikia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ielekee hiyo *speaker* ili Mhe. Waziri, aweze kukusikia vizuri.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ninaielekea *speaker* na ninakushukuru.

a) Kwanza ni kwamba vyombo vya habari viliripoti kwamba upanga huo ulipotea katika mikono ya Jeshi la Polisi kupitia Kamishna wetu Zanzibar. Hiyo, si sababu inayowafanya wazanzibari kuonekana kwamba hawawezi kuwa Viongozi wa Jeshi la Polisi na hiyo si njama iliyopangwa ya kuonesha kwamba Zanzibar hatuwezi kuwa viongozi wa Jeshi la Polisi.

b) Kama ulipotea katika mikono ya Kamishna Zanzibar nadhani ni sababu iliyomfanya Kamishna wetu sasa kunyang'anywa ukamishna na akawa Kamishna wa Polisi Jamii Tanzania.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, mabadiliko yaliyotokea katika Jeshi la Polisi hayakutokea kwa sababu ya kutokuwa na uwezo kwa Kamishna Mussa Ali wa kuongoza Jeshi la Polisi Zanzibar au njama zilizofanywa kwa makusudi kuibiwa kwa upanga huo ili ionekane kwamba wazanzibari hawana uwezo wa kuongoza jeshi hilo.

Kwa kweli mabadiliko yaliyotokea ni ya kawaida yanayofanyika wakati wowote pale Mhe. Rais, anapoona kuna haja ya kufanya hivyo. Kamishna Mussa Ali ameteuliwa sasa kuwa Kamishna wa Polisi Jamii Tanzania nzima. Kwa hivyo, ukiangalia kimamlaka atakuwa na eneo kubwa zaidi la kufanya kazi ukilinganisha na kuwa Kamishna wa Zanzibar peke yake. Kwa maana hiyo, bado amepewa heshima kubwa ya kuendelea katika kuongoza Jeshi letu la Polisi.

Aidha Kamishna aliyeletwa ni kijana mzanzibari shupavu ambaye anao uwezo mkubwa wa kuongoza Jeshi la Polisi Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, kilichotokea ni wizi wa kuiba upanga. Sasa kinachoendelea kufanywa ni uchunguzi kwa ajili ya kujulikana nani aliyeiba na kama nilivyosema katika swali la msingi umeibiwa wapi, kwamba wakati wa kuondoka au ulipofika Dar-es-Salaam, ama njiani. Kwa hiyo, uchunguzi huo unaendelea kufanywa.

Vile vile, kama nilivyosema katika swali la msingi ni kwamba tayari kwa kuwa kuna utaratibu wa kubadilishana kila baada ya kipindi kutoka nchi moja kwenda nchi nyengine na hivi sasa Botswana ndio anakuwa Mwenyekiti wa *SARPCCO*. Kwa msingi huo tayari Botswana wamejitolea kutoa upanga mwengine na shughuli zinaendelea kwa mujibu wa utaratibu tulioweka kwenye utaratibu wa *SARPCCO*. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza swali la nyongeza. Kwa kweli Mhe. Waziri, amekubali kwamba wizi umefanyika pia amekiri kwamba utaratibu upo na unaendelea.

Je, Mhe. Mwenyekiti, tuangalie tokea uibiwe mpaka leo hii ni siku ngapi. Vile vile, kutokukamilisha utaratibu haoni kama kuna sehemu fulani ya chombo hichi cha Jeshi la Polisi kudhalilishwa kutokana na kutokujua wajibu wao. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli ni muda tokea kuibiwa kwa upanga huu na kwa vyovyote vile sura kama hii huwa haioneshi kuwa sura njema kwa Jeshi la Polisi, kwa sababu wao ndio wangetumainiwa kuwa walinzi na wachunguzi wazuri pale wizi unapotokezea. Kwa hiyo, linapotokea jambo hili na ikashindwa kuthibitishwa mapema, basi kwa vyovyote vile haileti sura nzuri.*(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, naomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba Mhe. Mjumbe, pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi wote pamoja na wananchi kuwa wavute subira ili jambo hili liendelee kufanyiwa uchunguzi na baada ya hapo tulitake Jeshi la Polisi litoe taarifa vizuri zaidi kuhusu jambo hili, kwa ajili ya kuweza kuhakikisha kwamba mambo kama haya yasiweze kutokea katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Mhe. Mwenyekiti, wakati alipokuwa akijibu swali la msingi Mhe. Waziri, alisema kwamba upanga huo baada ya kupotea kuna gharama fulani zinahitajika zitolewe. Je, gharama hizo zitakuwa ni za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

b) Kwa muda mrefu tumekuwa tukishuhudia kwamba Jeshi la Polisi Zanzibar linashindwa kabisa kufanya uchunguzi juu ya matukio mengi ya kihalifu ikiwemo watu kumwagiwa tindi kali, mauaji pamoja na hata hilo la kupotea kwa upanga wa dhahabu. Mhe. Mwenyekiti, haoni kuwa Mhe. Waziri, kwamba kuna haja sasa ya kulibadilisha moja kwa moja Jeshi la Polisi katika mfumo wa uendeshaji wake Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, tatizo lile lile kwa mfano ukinitizama mimi huku sikusikii na ukisema na *speaker* nakusikia.Hivyo, lile la pili sijalisikia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, rejea swali lako.

a) Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi nilimuuliza kwamba, kwa muda mrefu sasa Jeshi la Polisi Zanzibar linashindwa kufanya uchunguzi juu ya matukio mengi ya kihalifu ikiwemo watu kumwagiwa tindi kali, mauaji ya kinyama pamoja na hata hilo la

kupotea kwa huo upanga wao wenyewe polisi. Mhe. Mwenyekiti, haoni kuwa Mhe. Waziri, kwamba kutokana na kushindwa kwao huku kuna haja sasa ya kulibadilisha moja kwa moja Jeshi la Polisi Zanzibar tukiacha kuwaondosha Makamishna tu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba tuwasikilize baina ya muulizaji swali na anayejibu swali ili waweze kufahamiana na tukiongea sana itakuwa watu hawafahamiani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu nani analipa gharama kama nilivyosema awali kwamba ndugu zetu wa Botswana wametengeneza upanga mwengine na bila ya kulipisha nchi yoyote mwanachama wa *SARPCCO*. Kwa hivyo, wamejitolea kufanya kazi hiyo na upanga umepatikana hivyo shughuli zinaendelea.

Vile vile, ni kweli kuna vitendo vingi vilivyofanyika vya uhalifu na mpaka leo bado uchunguzi haujathibitisha kuwapata watuhumiwa wa makosa hayo. Mhe. Mwenyekiti, kwa njia moja au nyengine utaona kwamba lipo tatizo. Kwa hivyo, nataka niupokee ushauri wa Mhe. Mjumbe, ili jambo hili lifanyiwe kazi, kwa sababu kwa vyovyote vile wahalifu wanatakiwa wapatikane na wafikishwe kwenye vyombo vya sheria ili wananchi wawe na imani na Jeshi lao la Polisi. *(Makofi)*

Kwa msingi huo tutafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba hatua zinachukuliwa, uchunguzi unafanyika na tujenge mazingira mazuri katika Jeshi la Polisi yatakayowezesha yanapotokea matatizo ya namna kama hii basi hatua zinachukuliwa kwa haraka na wahusika wanapatikana. *(Makofi)*

Nam. 17

Kuondosha Kero katika Utendaji wa Shirika la Bandari

Mhe. Rufai Said Rufai (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) – Aliuliza:-

Shirika la Bandari ndio nguzo ya uchumi wa Zanzibar.

(a) Kwa nini Septemba 10 usafirishaji wa magari ulikwama kutokana na ukosefu wa mashine ya kunyanyulia vitu vizito (*crane*) wakati magari yanaingiza kipato kikubwa kwa serikali na kusababisha msongamano mkubwa wa magari na Bandari yenyewe ni ndogo.

(b) Kwa kuwa shirika limeshindwa kutoa huduma kwa kiwango cha ubora, kwa nini lisibinafsishwe, ili wadau wa Bandari hiyo

waondokane na kero ya urasimu na huduma duni katika ushushaji wa mizigo na upekuzi.

(c) Ni lini shirika hilo litakuwa makini kufanya kazi kama nchi za jirani ikiwemo Mombasa, Dar-es-Salaam kufanya kazi masaa 24 ukizingatia kuna umuhimu mkubwa wa kufanya hivyo kutokana na ufinyu wa bandari yetu kuwa uchochoro mdogo wa kufanya kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 17 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba usafirishaji wa magari kwa siku ya tarehe 10 Septemba, 2013 haukufanyika. Hali hii ilisababishwa na shirika kutokupokea maombi ya kifaa cha kunyanyulia vitu vizito (*crane*) kutoka kwa wenye meli kwa ajili ya upakizi wa magari hayo. *(Makofi)*

(b) Tokea kuanzishwa kwa Shirika la Bandari halijawahi kushindwa kutoa huduma ya upakizi na uteremshaji wa mizigo bandarini na kwa sababu hiyo, wizara yangu bado haioni haja ya kubinafsishwa shirika hilo.

(c) Shirika la Bandari toke lilipoanzishwa linaendesha shuhguli zake kwa masaa 24 kwa mpangilio wa zamu (*shift*) 3 za kazi kwa kila siku.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri, swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa Bandari yetu ya Zanzibar haina nafasi ya kutosha ya kuekea mizigo na kwa kuwa wachukuzi wetu wanaumia sana kubeba mizigo kwa kichwa na huchukua muda mrefu sana.

Je, wizara haioni haja ya kumkubali mwekezaji alete *crane* yake binafsi kwa ajili ya kuihami hali iliopo bandarini na serikali inaendelea kupata mapato. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Bandari ya Malindi ina eneo finyu na kuna haja ya kuongeza vitendea kazi ikiwemo *crane*, ili kuweza kuimarisha utoaji wa huduma kwa wafanyabiashara na wananchi wengine wanaofuata huduma hii.

Mhe. Mwenyekiti, shirika na serikali hatuna kipingamizi na mwekezaji, isipokuwa msingi mkubwa ni kufuata taratibu husika katika upatikanaji wa kifaa hicho, kukidhi mahitaji na utaratibu uliokamilika. Kwa mfano kama vile ambavyo tumeweza kuwaruhusu wengine kutupa misaada, kushirikiana nao au kutusaidia na wala hatuna sababu ya kuwazuia wengine kutupa misaada wa kushirikina nao katika nia ya kutaka kutoa huduma bora kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nataka nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, kwa mara ya mwanzo leo kutaka ushauri na kupokea. Kwa hiyo, ninampongeza sana Mhe. Naibu Waziri, kwa sababu tokea kumfahamu kwangu. *(Makofi)*

a) Mhe. Mwenyekiti, huduma za upakizi na ushushaji mizigo ni jukumu la Shirika la Bandari, inakuwaje shirika likose kifaa cha kushushia mizigo mizito kwa muda wa saa 24. Je, hii ni hatua ya kwenda mbele au kurudi nyuma kimaendeleo.

b) Lini Shirika la Bandari litakuwa na vifaa vyake vya uhakika vya kushushia mizigo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bandari linatoa huduma na miundombinu yake iko ya aina mbili, ile ya kukaa na vifaa. Sasa tunapozungumzia suala la miundombinu ya vifaa bila ya shaka vitatumika na kuchoka, isipokuwa utaratibu mzuri ni kuwa na mfumo mzuri ambao kinachochoka kinapata *replacement* yake. Kwa hivyo, sisi kama shirika tunatambua kwamba vifaa hivi vinapotumika viweze kuwa na mbadala wake, suala liliopo hapa ni gharama za ununuzi wa vifaa hivyo ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumhakishia Mhe. Mwakilishi kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti kwamba dhamira yetu ni kuhakikisha kuwa tunakuwa na vifaa vyote vinavyoweza kutoa huduma. Tatizo liliopo ni kwamba inafika hapala gharama zinakuwa kubwa na kwa wakati mmoja hatuwezi kununua vyote. Kwa mfano tunahitajika kununua *tag*, *crane* pamoja na vifaa vyengine.

Vile vile, napenda nimhakikishie Mhe. Mjumbe, kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba kadri ya upatikanaji wa fedha utakavyokua basi ndivyo tutakavyoweza kuimarisha vifaa kwa ajili ya kuimarisha huduma kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, lini tutaweza kuwa na vifaa vyetu kwa ukamilifu, pale tu shirika litakapoweza kujikwamua vizuri katika shughuli zake za kibiashara na

bila ya shaka tutapata uwezo mzuri wa kifedha kuweza kununua vifaa vyote vya kutoa huduma hizo. *(Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Zanzibar inategemea sana bandari zake kwa kuingiza uchumi katika nchi hii ikiwa ni pamoja na mambo ya usafiri na kusafirisha. Kutokana na kwamba bandari yetu hivi sasa ni ndogo sana na haifanyi huduma za kuridhisha. Je, ile azma ya kufanya utanuzi wa bandari yetu katika eneo la Mpigaduri imefikia wapi, kwa sababu mpaka leo tunaona ni kimya.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, Bandari ya Malindi kama tulivyoeleza awali kwamba eneo lake ni dogo na sisi kama serikali tunao mpango wa muda mfupi na mrefu.

Katika mpango wa muda mfupi ni kuhakikisha kwamba eneo lile dogo tunaweza kulisanifu na kulitumia vizuri zaidi, ikiwa ni pamoja na kuhamisha mabanda mengi yaliomo mule kwa kuyavunja, kukamilisha ofisi yetu mpya katika jengo la *DP3*, ili kuweza kutoa sakafu kubwa kwa ajili ya utoaji wa huduma hasa uwekaji wa makontena na hii ni mipango ya muda mfupi.

Mipango ya muda mrefu azma ya serikali ya kutaka kujenga Bandari mpya kubwa ya Mpigaduri ipo katika hatua nzuri. Kwa hivyo, kipindi hiki serikali inaendelea kufanya mazungumzo na washirika wa maendeleo katika hatua ya awali, utaratibu wa kukamilisha *feasibility study* umefikia hatua nzuri, ambapo baada ya kukamilika hatua hiyo ya *feasibility study* itarudi serikalini, ili serikali kwa ajili ya kujipanga katika mpango wa utafutaji wa fedha kwa lengo la kukamilisha mradi huu mkubwa wa bandari, mradi ambao tunategemea utakuwa mkombozi kwa harakati za uchumi wa nchi yetu.

Nam. 33

Kutoimarishwa Kiwanja cha Ndege Pemba

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Kutokana na kuwa kiwanja cha Ndege cha Pemba mpaka hii leo bado hatujashuhudia kufanyiwa matengenezo na maboresho yoyote ili kiweze kukuza huduma na hapo hapo kukuza uchumi wa nchi hii.

Ni sababu zipi za msingi zilizofanya kiwanja hicho kutofikiriwa kuimarishwa kwa matengenezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam. 33 kama ifuatavyo:-

Zanzibar kwa ujumla hadi hivi sasa ina viwanja viwili vikubwa vya huduma za uwanja wa ndege, ambavyo ni Kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume kilichopo Unguja na Kiwanja cha Ndege cha Pemba.

Aidha kiwanja cha Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume kwa sehemu kubwa hivi sasa unatumika kutoa huduma za kitaifa na kimataifa na kwa upande wa uwanja wa Ndege wa Pemba hali kidogo ni tofauti, kwani umekuwa ukitumika zaidi kwa ajili ya utumiaji na utoaji huduma kitaifa. Kwa kweli hali hiyo inatokana na mapungufu kadhaa ikiwemo miundombinu pamoja na vifaa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuliona suala hilo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imekuwa ikifanya juhudi za makusudi katika kuimarisha kiwanja hicho cha Ndege cha Pemba kwa uboreshaji wa huduma kadhaa kwa kila mwaka wa bajeti.

Vile vile, pamoja na sababu ya msingi ya ukosefu wa fedha tayari Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wameweza kujipanga na kuyakamilisha mambo kadhaa katika mwaka huu wa kibajeti ikiwa ni pamoja na utanuzi wa maeneo ya kukaa abiria pamoja na kutenganisha maeneo ya kuhifadhi mizigo, yaani ile inayosafiri na ile iliyowasili. Pia, kuyapatia maofisi mashirika yanayotoa huduma za ndege, kurekebisha kumbi za watu mashuhuri pamoja na ukarabati nyumba ya wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka huu ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kipaumbele muhimu zaidi kwa uwanja huo wa Pemba ni suala zima la uwekaji wa taa, ili tuweze kutoa huduma za usafiri masaa 24, kuhuwisha matumizi ya usafiri wa ndege, kuimarisha harakati za utalii pamoja na kukuza uchumi wa nchi yetu kama lilivyo lengo la suala mama la Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Ni ukweli usiofichika kuwa Kiwanja cha Ndege cha Pemba kinahitaji matengenezo makubwa na gharama ni kubwa inayohitajika, kwa sababu huu ni mradi mkubwa na kutokana na uwezo wa serikali yetu ulivyo, basi naamini siku zote itakuwa ni maneno tu, lakini hakuna vitendo vinavyofanyika.

Kwa mfano suala la taa ni kipindi cha tatu hiki, miaka 15 mfululizo linazungumzwa na wala halijafanikiwa, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti nilisikia kuwa kuna mfuko wa Afrika ya Mashariki na kwa makusudi uliamua katika miradi yake mikubwa ni kukifanyia matengenezo makubwa Kiwanja cha Ndege cha Pemba na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitakiwa kupeleka baadhi ya mambo kule, ili kazi ifanyike.

Je, hii taarifa ni kweli na kwa nini kama ni kweli serikali imeshindwa kupeleka mambo yanayotakiwa, kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo makubwa ya kiwanja hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Pemba una mapungufu mengi, kama vile *fence*, *rainway* fupi, *terminal* yenyewe haiko katika kiwango kizuri zaidi, huduma za *fire* pamoja na huduma nyengine.

Vile vile, ni kweli kwamba wenzetu wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki walikuwa na dhamira hiyo ya kutaka tusaidiane katika uendelezaji wa mradi huu. Tatizo lililokuwepo kwamba kwa kipindi kile sisi kama serikali hatukuwa na *feasibility study* ambayo ilikuwa ikionesha mapungufu pamoja na muongozo mzima katika uimarishaji wa uwanja huu.

Kwa hivyo, kutokana na ukosefu wa *feasibility study*, basi mradi ule ukashindwa kusaidiwa na wenzetu wa *East Africa*. Mhe. Mwenyekiti, hadi leo hii bado suala la *study* tumetenga fedha na kuona kwamba tunaandaa utaratibu sasa wa kuweza kutafuta watu wa kuweza kulifanya.

Aidha katika mnasaba huo huo tayari sisi wizarani kwa maelekezo ya serikalini kuna wahisani wa shirika wa maendeleo ambao wameonesha dhamira ya kutaka kusaidiana na sisi katika uimarishaji wa uwanja mzima wa Ndege wa Pemba.

Lakini kwa kutambua umuhimu pekee wa uimarishaji hasa wa huduma za taa, sisi kama serikali tumechukua kipaumbele na hatua ya kwanza tulikuwa tumefikia pahali na kutangaza mpaka zabuni kwa bahati mbaya kwamba wazabuni wetu hawakukidhi yale matakwa na utaratibu wa Sheria ya Ugavi na Manunuzi kwa mujibu wa taratibu za sheria za Zanzibar.

Kwa hivyo, tumeelekezwa kwamba turejee tena katika kutafuta watu kutangaza tena zabuni ile, ili tupate watu watakaokidhi masharti ya sheria, ili sasa utaratibu wa uwekaji taa uwezekukamilika. Malengo yetu ni kwamba tunataka tuhakikishe kwamba tunaweka taa na watakapokuja wahisani au

washirika wa maendeleo taa ambazo zinaweza kuondoka ku-*extend* ili kuweza kupisha miundombinu kuweza kutanuliwa vyengine kama vile mahitaji yatakavyokuwa yanaruhusu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kuniona na kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, naomba niwape pole wafiwa waiofiliwa na aliyekuwa Mwakilishi wa zamani wa Jimbo la Micheweni ndugu Salim Hamad Saleh.Kwa hiyo, nawapa pole wazee, ndugu zake wote pamoja na wananchi wa Jimbo la Micheweni wote nawapa pole kwa kuondokewa na aliyekuwa kiongozi wao wa Jimbo la Micheweni. *(Makofi)*

Baada ya pole hizo, naomba nimuulize Mhe. Waziri, kwa kuwa Kiwanja cha Ndege cha Pemba ni kiwanja kimoja muhimu katika viwanja vyetu vya Zanzibar na kwa kuwa kiwanja kina muda mkubwa hakina taa na hivi karibuni nimeshuhudia ndege ya *Auric Air* ikichelewa na kufika saa 12 karibu na nusu Pemba na wakati abiria wameshasubiri kwa muda mkubwa mpaka wakakata tamaa, ndege ile ilipofika haikuzima hata engine watu wanatoka na wengine wanaingia, kwa ajili ya kuwahi kuruka mbio mbio.

Je, ni lini zitawekwa taa angalau za dharura ili ndege ziweze kuruka na kutua wakati wa usiku, kwa sababu tuliambiwa kwamba zitawekwa taa za dharura. Sasa je, taa hizo zimekwama wapi na lini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri, alisema kama taa hazijapatikana basi itawekwa japo mishumaa ya vita vya pili vya dunia. Kwa hivyo, ni lini itawekwa ili watu waweze kuona. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, inaonekana Mhe. Naibu Waziri, wakati alipokuwa akijibu hukumsikiliza tayari jawabu ya swali lako limeshajibiwa. Katibu tuendelee.

Nam. 3

Uchafuzi wa Bwawa la Msikiti Mabuluu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny. Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza:-
Mwanzo kabla ya yote Mhe. Mwenyekiti, natakakuwatoa wasiwasi wananchi wa Jimbo la Wawi kwa kutokumuona Mwakilishi wao kwa kipindi cha siku tatu, nne, Mwakilishi huyu hasa kwa Shehia ya Vitongoji, Uwandani, Umangani na Kibokoni niwaambie Mwakilishi wao hajisikii vizuri na yuko Dar es Salaam kimatibabu wasitie wasi wasi, Mwakilishi wao yuko makini kwa kuwatetea wananchi hao.

Kwa kuwa ndani ya eneo lililojengwa Msikiti Mabuluu mkabala na Hoteli ya Bwawani lipo bwawa kubwa la maji ambalo kwa sasa zaidi linatumika kwa kuoshea magari ambayo huchafua sana maji hayo na kuhatarisha maisha ya viumbe vinavyoishi ndani ya maji hayo. Na kwa kuwa uchafuzi wa maji hayo hufikia kiwango hata cha kubadilisha taswira ya maji hayo na hatimaye kubadilisha mandhari sio tu ya Bwawa hilo, lakini hata mandhari ya hoteli na msikiti wenyewe.

Je, bwawa hilo lipo hapo kwa dhamira gani.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-
Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma swali lake Nam. 3 naomba nitoe maelezo mafupi yafuatayo:-

Mabwawa yote yaliopo eneo la Bwawani yamejengwa sambamba na ujenzi wa Hoteli ya Bwawani kwa ajili ya kutoa huduma ya michezo ya majini ya Hoteli hiyo. Bahati mbaya sana dhamira hiyo njema haikuweza kuendelezwa na kufikia lengo lililokusudiwa. Hivyo, kwa sasa Mabwawa hayo yamekuwa yanapokea maji ya mvua kutoka sehemu mbali mbali za maeneo jirani na eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa kwa idhini yako tena naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Dhamira ya awali ya eneo hilo kutumika kwa ajili ya michezo ya kwenye maji kwa wageni wa Hoteli ya Bawawani, kwa sasa haipo tena. Hivi sasa serikali inafanya juhudi za kutafuta Wawekezaji wote wa eneo la Bwawani ili kuepusha taswira isiyo nzuri ya eneo hilo.

Kwa wakati huu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inafanya jitihada za kukutana na taasisi husika ili kushauriana jinsi ya kukabiliana na juu ya upigaji marufuku ikiwezekana shughuli za uoshaji wa magari katika eneo hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Zanzibar kufanikiwa kupiga hatua kubwa yakudhibiti kuondoa malaria, bwawa hilo linaweza ikawa ndio chanzo kikubwa cha mazalio ya mbu. Je, serikali ina mpango gani wa kuondosha bwawa hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyeki, katika kampeni ya kupambana na malaria na kujaribu kuiondosha hapa Zanzibar, sehemu zote ambazo zinakuwa ndio mazaliaji ya mbu wa

malaria zinashughulikiwa katika wakati unapofika wa upigaji dawa katika kuondosha mbu hao wasiweze kuzaliwa katika maeneo hayo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka kumuuliza Mhe. Waziri, swali la nyongeza. Hivi karibuni tulisikia kuwa pale Bwawani pote wanatafutwa wawekezaji wauweza kuitengeneza na kuondoa mabwawa hayo ili hao mbu wasizaliwe.

Je Mhe. Waziri, mpango huo anaujua, kama unaujua mpaka sasa hivi umefikia wapi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimshauri sana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, akalitafutia swali hili nafasi yake ya kuliuliza kwa sababu halina mahusiano kabisa na swali mama.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, amekiri kuwa ile azma hasa ya ujengwaji wa bwawa hili litumike kwa shughuli alizozitaja haiko tena na kwa sasa bwawa hili linapokea maji ya mvua. Vile vile, kakiri kuwa watu wanakosha magari yao pale. Kwa sababu maji ya mvua yanachukua kila uchafu na uoshaji wa gari unasababisha kuingiza mambo ambayo ni ya hatari katika maji.

a) Ni muda gani mpaka hivi sasa bwawa lile limetumika kwa kuoshea magari.

b) Nikwa kiasi gani wizara yake inafanya kazi ya kutiwa dawa katika maji yale machafu kwa uchafu unaoingizwa.

c) Mhe. Waziri, anaweza kutueleza kuwa maji yale yanamalizikia wapi na ikiwa ni kwenye baharí haoni pia kuna uharibifu wa mazingira katika eneo la baharí na kwa ufupi kama huyo mwekezaji hakupatikana nini hatima ya bwawa lile, likae vile vile lilivyo lihatarishe maisha au vipi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wananchi ambao wameanza shughuli za kukosha magari pale sina hakika sasa hivi ni mwaka gani hasa walianza, lakini ni kipindi hakipungui miaka mitano wapo pale kwa ajili ya shughuli hizo za kutumia maji yale kukosha magari yao.

b) Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, haihusiki na utiaji wa dawa za kuuwa vizalia vinavyosababisha mbu ambao wanaleta malaria kwa ajili ya kampeni ya kuzuia malaria. Suala hili linashughulikiwa na Wizara ya Afya.

c) Nimejibu katika jibu langu mama kwamba maji yale mengi yao yanakusanywa wakati mvua inapokuja kutoka katika mitaa ya jirani, mitaa ya pwani, mchangani, maji yote ndio yanashukia katika eneo hilo. Lakini pia, alitaka kujua, je, kama hakujapatikana mwekezaji serikali itachukua hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu kwamba, serikali ina imani kubwa kuwa mwekezaji wa kuendeleza eneo hili atapatikana kwa sababu ni eneo ambalo linaweza kutumika kwa shughuli muwafaka za kitalii na kama hakujapatikana mwekezaji basi serikali itafikiria njia nyengine ya kuweza kufanya, lakini kwa sasa serikali hairidhiki na mandhari iliyopo pale na inaishughulikia kikamilifu kuona kwamba eneo hilo linaendelezwa.

Nam. 9
Bajeti finyu kwa Chuo cha Mafunzo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny. Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza:-
Kwa kuwa Chuo cha Mafunzo ni miongoni mwa Vikosi vya SMZ chenye jukumu la kuhifadhi na kudhibiti wanafunzi wanaotumikia vifungo vyao, sambamba na kuhifadhi watuhumiwa (*Rumande*) wanaosubiria kesi zao Mahakamani na kwa kuwa mara nyingi bajeti ya kikosi hiki inakuwa ndogo kwani idadi ya wanafunzi na wa rumande hupanda na kushuka siku hadi siku jambo linaloleta usumbufu mkubwa katika utoaji huduma kwa watu hao.

Je, ni lini serikali itatoa umuhimu kwa kikosi hili kwa kupanua bajeti yao ili kuondosha usumbufu wa huduma unaojitokeza siku hadi siku katika vyuo vyetu vya mafunzo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:-
Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 9 kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na maoni ya Mhe. Mwakilishi kuwa idadi ya mahabusu na Wanafunzi katika Vyuo vya Mafunzo inapanda na kushuka, hali hiyo inasababisha kuwa mzigo mkubwa kutokana na ufinyu wa bajeti hasa wakati wa idadi ya mahabusu inapokuwa kubwa.

Kutokana na hali hiyo Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ imeshachukua hatua ya kuongeza bajeti katika kasma ya chakula kwa mahabusu na wanafunzi kwa mwaka 2013/2014 ambapo bajeti ya chakula imepanda kutoka 750,000,000/= hadi 863,992,000/= ambayo ni ongezeko la shilingi 113,992,000/= sawa na asilimia 15.2 ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana. Ili kupunguza tatizo hilo kwa upande mwengine tunawasiliana na vyombo vinavyohusika na uendeshaji wa kesi ili kesi zisichukue muda mrefu kabla ya kufikiwa maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, chuo pia kinajenga jengo jipya la kuishi ili kupunguza msongamano na kuimarisha huduma kwa wanafunzi na watuhumiwa. Aidha, jitihada zinafanywa za kuongeza uzalishaji wa chakula ili kupunguza kutegemea zaidi chakula cha kununua ambacho kinachukua sehemu kubwa ya bajeti ya chuo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru tena kwa mara ya pili Mhe. Waziri, kwa kukiri na kuona ukweli wa suala hili, huu ni mfano mzuri wa Mhe. Waziri. Serikali kwa nini inashindwa kununua chakula cha kutosha hasa kwa kuzingatia chakula chenyewe hakiozi na kinapikwa kwa mujibu wa wakati. Mhe. Waziri, haoni kuwa hiyo ni kukiuka msingi wa haki za binadamu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza serikali inanunua chakula cha kutosha kwa wafungwa kwa mujibu wa bajeti iliyotengwa katika kipindi hiki cha mwaka huu. Pili, hatuoni kwamba ni suala la kukiuka haki za binadamu kwa sababu wanafunzi na mahabusu wanapata chakula cha kutosha mara tatu kwa siku.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri, swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri, amesema kwamba bajeti kubwa ya Chuo cha Mafunzo huenda katika ujenzi wa majengo mapya ya chuo hicho Hanyegwamchana.

Je, Mhe. Waziri, haoni kwamba muda umefika sasa kwa kuwa *project* ile ni kubwa kushauri serikali kuu kuchukua *project* ile ku-*save* zile pesa zinazotumika kule na badala yake pesa zile zikatumika kuwalisha rumande na wanafunzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza sikusema kwamba bajeti kubwa inakwenda kwenye ujenzi wa jengo la chuo Hanyegwamchana, nilisema bajeti kubwa inakwenda kwenye ununuzi wa chakula na ndio maana tuna mpango wa

kuimarisha uzalisha wa chakula ili kupunguza bajeti hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa nafikiri nilipokuwa nikijibu swali langu hakuweza kunisikia vizuri.

Lakini hata hivyo, swali lake la ni kwa jinsi gani serikali mradi huu wa ujenzi wa Chuo cha Mafunzo unaondoshwa katika bajeti ya Chuo cha Mafunzo peke yake na uwe katika mpango wa kitaifa. Jambo hilo tayari serikali kupitia wizara yangu tumeshalifikisha serikalini na serikali kwenye mpango wa bajeti wa mwaka ujao jambo hili litaingizwa katika mpango wa taifa badala ya kuwepo kwenye bajeti ya Chuo cha Mafunzo peke yake.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Chuo cha Mafunzo kimefanya jitihada ya kujenga jengo lake la Ubago ili kulifanya lifikie hadhi ya kimkoa ili kuweza kuondosha usumbufu wa hasara za aina mbili.

Hasara ya kwanza ni hasara ya kuwachukua watu wa rumande wa Mkoa wa Kusini kuwaleta mjini na kuwatoa mjini kuwapeleka katika Mahakama za mbali za Kusini kama Makunduchi na Chwaka, inaonekana inapelekea gharama kubwa za mafuta za kuwachukua mahabusu wa Kusini kuwaleta mjini, tayari chuo kimeanza kuonesha jitihada ya kujenga jengo lile.

Gharama ya pili, kwamba eneo la Ubago la Chuo cha Mafunzo lina eneo zuri la kilimo, lakini linapata matatizo linakuwa na wanafunzi wachache kutokana na mazingira yake. Je, ni lini wizara yake itakamilisha jengo lile ili kuweza kuondosha usumbufu unaojitokeza.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba hasara, usumbufu na matatizo yote yanayokikabili Chuo cha Mafunzo, serikali inayaelewa na ndio maana ikadhamiria kuona iko haja ya kuweza kujenga jengo jipya hilo la Chuo cha Mafunzo cha Hanyegwamchana.

Kwa hivyo, serikali itaendelea kulifanyia kazi hasa ukizingatia kwamba katika kila Mkoa hatujawa na utaratibu wa kuwa kila mkoa tuna gereza kwa ajili ya kuwapeleka wanafunzi wetu, lakini angalau kwa Mkoa wa Kusini kuna maeneo maalum kwa ajili ya kuwahifadhi wanafunzi.

Suala la uchache wa wanafunzi na ukubwa wa maeneo ya kilimo, hiyo inategemea na maendeleo yaliyopo katika nchi yetu kwamba wahalifu sasa wamekuwa si wengi ambao wanahukumiwa kupewa vifungo. Sasa hilo liko

nje ya uwezo wetu, kama wahalifu wataongezeka na Mahakama zitawafunga kwa wingi maana yake sasa tutapata nguvukazi kubwa ya kuweza kuendeleza kilimo.

Utaratibu

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ni dogo tu labda Mhe. Waziri, hajanifahamu, kwamba kutokana na hayo mazingira yaliyojitokeza tayari Chuo cha Mafunzo kimefanyiwa ukarabati wa jengo la Gereza la Ubago na gharama kubwa imeshatumika na tayari wameshajenga karibuni maeneo mapya katika eneo lile. Tatizo lililojitokeza ni dogo la ujenzi wa *main gate* la kuweza kuweka ulinzi mzuri katika geti la nje, ndio nikauliza ni lini wizara itakamilisha ule ujenzi wa *main gate* ili kuweka usalama na kuweza kuwahifadhi wanafunzi wengi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa alikuwa na haraka, kama angeuliza swali moja kwa moja ningemjibu tu moja kwa moja, lakini unapotanguliza maelezo na mimi lazima nikupe maelezo, vyenginevyo mtaona kwamba naripua siwezi kuripua, ukitanguliza maelezo nitatoa maelezo, ukiuliza swali moja kwa moja nitakujibu. Sasa madhali hukuwa na haja ya kupewa maelezo kama ulivyotoa maelezo, naomba nimjibu kwamba Chuo cha Mafunzo tayari kimeshaweka *gate* katika Chuo cha Ubago.

Nam. 44
Viwanja vya Michezo Kufanywa Maegesho ya Gari

Mhe. Nassor Salim Ali – Aliuliza:-
Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa inatekeleza sera na ilani ya Chama cha Mapinduzi na ilani hiyo inaelezea kuendeleza michezo.

Je, sababu gani iliyofanya viwanja vya michezo kama vile kiwanja cha Lumumba, Binti Amran, Malindi na Kibanda Maiti kugeuzwa vituo vya kulaza gari na kuegeshwa daladala badala ya kutumika kwa shughuli za michezo ukizingatia viwanja vya michezo ni vichache hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:-
Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 44 kama hivi ifuatavyo:-

Kama alivyosema Mhe. Mwakilishi katika maelezo yake ya utangulizi wa swali lake kuwa ilani ya Chama cha Mapinduzi inaelekeza kuendeleza michezo. Mimi nakubaliana naye kwa asilimia mia moja. Aidha, mbali na ilani ya CCM ya mwaka 2010 iliyopata ridhaa ya wananchi kuiongoza nchi yetu, pia, mipango mikuu ya nchi yetu ukiwemo MKUZA, inaelezea umuhimu wa michezo katika kukuza uchumi wetu. Michezo inasaidia katika kuweka vyema afya zetu, kuimarisha utalii, kukuza urafiki na kujenga umoja baina yetu, majirani na kimataifa kwa ujumla.

Ili kufanikisha malengo hayo, ofisi yangu na taasisi zake iko makini sana katika kusaidia nchi yetu kuweka matumizi bora ya maeneo ya michezo kwa kufuata sheria, taratibu na miongozo ambayo tumejiwekea ili michezo isiwe ni chanzo cha vurugu na kuharibu utamaduni wetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kwa kutoa maelezo ya viwanja vinne vilivyotajwa kama ifuatavyo:-

Kiwanja cha Lumumba.	Kiwanja hiki kimevamiwa na watu wanaotengeneza magari, kuosha magari na upigaji wa matofali. Serikali baada ya kuona hali hiyo isiyoridhisha imeunda kamati ya mawaziri kulishughulikia suala la uvamizi huo ili maeneo ya Skuli ya Lumumba na uwanja wake wa michezo utumike kwa shughuli ambazo serikali imeziruhusu.
Kiwanja cha Binti Amrani.	Katika eneo hili kuna sehemu ndogo imetengwa kwa ajili ya maegesho ya daladala kwa muda tu na yataondoka ili kupisha mradi wa maendeleo ambao serikali imepanga kuutekeleza katika eneo hili. Hata hivyo, eneo linalotumika kwa maegesho si katika eneo la uwanja wa michezo.
Kiwanja cha Malindi.	Eneo hili linatumika kwa michezo, lakini baadhi ya watu wanalitumia kwa kushonea nyavu, kuuzia mifugo hasa mbuzi na kondoo. Na kwa upande mwengine kuweka magari ya abiria na mizigo. Utaratibu huu hauko katika matumizi bora ya eneo hilo na

	haujaruhusiwa kufanya hivyo. Serikali kwasasa inaandaa matumizi bora ya eneo hili na maandalizi hayo yatakapokuwa tayari na utafiti kukamilika matatizo niliyoeleza hapo awali yataondoka.
Kiwanja cha Kibandamaiti.	Eneo hili ni moja ya maeneo makubwa ya wazi na linatumika kwa shughuli mbali mbali za kijamii; ikiwemo mikutano ya kisiasa, michezo, sherehe za sikukuu, maegesho ya magari na kadhalika. Kwa sasa ni vigumu kutenga eneo hili kwa matumizi ya michezo peke yake. Ofisi yangu ikishirikiana na taasisi nyengine husika itapanga utaratibu bora wa zaidi wa matumizi ya viwanja vya Kibandamaiti kwa kufuata mipango ya miji yetu.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b). Namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri yenye maneno mazuri yenye kupendeza, nina imani kwamba wanamichezo leo watafurahi sana.

a) Katika majibu yake kwa Kiwanja cha Malindi ameeleza kwamba serikali ina mpango na ifanye utafiti ili kuweka mambo sawa pale. Lakini ukizingatia kiwanja cha Malindi kuna sehemu ambayo kuna kiwanja cha *Basket Ball* ambacho kimejengwa kwa ajili ya kuendeleza mchezo ule na pale ndipo panapotumika zaidi kuegesha magari. Je, ni lini hasa au serikali itatoa amri ya kuondoa magari yale katika eneo lile.

b) Katika Kiwanja cha Lumumba serikali ina mpango gani kujenga ukuta katika eneo lile kama maeneo ya pale Maruhubi ili kuweka mandhari na haiba nzuri katika eneo lile.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, (a) Serikali kama nilivyosema ina mpango wa kuliendeleza eneo zima la Darajani *corridor* likiwemo eneo la viwanja vya Malindi. Serikali inaegesha magari nje yaani wanaruhusiwa wananchi kuegesha magari mpaka hapo mpango miji utakapokamilika katika nje ya viwanja vya michezo kikiwemo kiwanja cha *basket ball*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe nimekuwa nikipita kila mara kuona hivi kweli katika viwanja vile magari yanaegeshwa? Kwa hivyo, katika viwanja viwili vya michezo wa mpira wa miguu na Kiwanja kimoja cha *basket ball* haviegeshwi magari hata wakati ambapo michezo hiyo haifanyiki. Kwa hiyo, nafasi ya kufanyika michezo ipo na nafasi ya kuweza kuegesha magari ipo.

b) Serikali kama nilivyosema kuwa imeunda kamati ya mawaziri kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi wa kuondosha kadhia iliyopo pale ya magereji, magari pamoja na upigaji wa matofali. Hapo wakati itakapokamilisha kazi yake kamati itafikisha serikalini na serikali haitakuwa na tatizo kuweza kulihifadhi eneo lake kwa kulijengea ukuta.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii na mimi kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri ambaye ni mramu wangu. Pamoja na majibu yake mazuri sana amesema kuwa katika viwanja vya Biti Amrani kunataka kujengwa Hospitali ya Wilaya. Lakini mimi nafahamu hiyo Mpendae haina masafa makubwa kati ya Biti Amrani na hiyo Mpendae yenyewe kuna hospitali moja kubwa sana na sheria za ujengaji wa vituo vya afya havitakiwi viwe hapo kwa hapo.

Je, Mhe. Waziri, kwa nini asiweze kuitengeneza zaidi hiyo hospitali ya Mpendae ikawa kubwa zaidi ikalingana na wilaya.

Lakini vile vile, Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mchezo sasa hivi Zanzibar unaleta faida na mchezo ni kujenga afya na sasa hivi viwanja tushakuwa tuna mpango huo wa kuwekeza vitu kama vya aina hiyo. Haoni Mhe. Waziri, ni kupoteza haiba ya mchezo wa mpira wa Zanzibar na kunyima haki za wachezaji wa mpira.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza sikusema kwamba serikali inataka kujenga hospital, sasa tarifa za kujenga hospital azitafute kwa hao ambao wanataka kufanya mradi. Mimi nimesema serikali inataka kupatumia kwa miradi ya maendeleo.

Pili, mimi nadhani wakati nikijibu swali langu nilisema wazi, kwamba hatuwanyimi haki wanamichezo kwa sababu pahala ambapo sasa hivi panatumika kwa ajili ya kuegesha magari ijapokuwa hayo magari yenyewe hayendi, ni tofauti na ule uwanja unaotumiwa kwa ajili ya kucheza mpira. Kwa hivyo, pahala ambapo serikali imepanga si pahala ambapo panachezewa mpira. Ahsante.

Nam. 26
Uchakavu wa Nyumba za Mji Mkongwe

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-
Nyumba za Mji Mkongwe zinakabiliwa na uchakavu na kuhatarisha usalama wa wananchi wakati uwezo ni mdogo wa kuzifanyia matengenezo makubwa.

(a) Nyumba ngapi hadi sasa ndani ya Mji Mkongwe hazikaliwi na watu kutokana na kukabiliwa na uchakavu.

(b) Baadhi ya nyumba zilikuwa zikifanyiwa matengenezo na Taasisi ya *Aga Khan* mradi huo umeishia wapi.

(c) Kama serikali uwezo wake mdogo kwa nini nyumba zilizotaifishwa wasirudishiwe wahusika badala ya majengo kuendelea kutishia usalama wa wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-
Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 26 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, idadi ya nyumba ambazo hazikaliwi katika maeneo ya Mji Mkongwe ni nyumba 40.

(b) Mradi huu ulianza mwaka 1999 na kumalizika 2005 mwanzoni. Mradi huu ulikuwa ukijulikana kwa jina la *"Community Based Rehabilitation Program"* ambao ulifadhiliwa na *SIDA*. Na *Aga Khan* walikuwa ni wawakilishi tu ambao wanasimamia upatikanaji wa fedha hizo kutoka *SIDA*.

(c) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu ina wajibu wa kutafuta uwezo wa kuzifanyia matengenezo nyumba hizo, tutajitahidi kutafuta wahisani wa kuzifanyia matengenezo nyumba hizo wakiwemo *UNESCO* na wengineo ili kuzinusuru nyumba hizo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya kusikitisha ya Mhe. Naibu Waziri, kuna taarifa aliyekuwa wakala wa mradi huu *Aga Khan Culture Services Zanzibar*, inasemekana amesitisha miradi yote ya Zanzibar tangu kunyang'anywa eneo la uwekezaji ukanda wa Forodhani ikiwemo Mambomsiige.

a) Je, nini ukweli wa suala hili.

b) Serikali kurejesha nyumba hizo kwa wahusika, imefanya utafiti kuhusu uwezo wa kuzingatia matengenezo au kuepusha hali ya hatari kwa wananchi wanaoishi karibu na nyumba hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, swali la pili ni kama nilivyoeleza hapo awali serikali ina nia ya kuzitengeneza nyumba hizi na ndio maana tukasema kwamba serikali kupitia wizara yangu itajitahidi kutafuta wahisani ili tuhakikishe kwamba nyumba hizi tunazifanyia matengenezo. Swali la kwanza sikulifahamu vizuri naomba arejee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kuna taarifa aliyekuwa wakala wa mradi huo *Aga Khan Culture Services Zanzibar*, inasemekana amesitisha miradi hiyo Zanzibar tangu kunyimwa eneo la Mambomsiige. Je, ni kweli kuhusu suala hili. Naiomba serikali itoe kauli yake kuhusu suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu kuwa taarifa hiyo nitamjibu kwa maandishi.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mbali na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kuhusiana na majumba ya Mji Mkongwe. Lakini Mhe. Mwenyekiti, pale Darajani kuna nyumba maarufu inaitwa nyumba ya treni au jumba la Barghash.

Jumba lile Mhe. Mwenyekiti, halipo katika hali nzuri. Je, serikali ina mpango gani wa kulifanyia ukarabati jumba lile au kulijenga upya ili kuja kuondoa hasara ya wananchi wa pale kwa sababu ukizingatia jumba lile ni refu na kubwa, lakini hapo hapo jumba lipo katika hali ya ubovu na linaweza kuhatarisha hasara wakati wowote.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kama kweli jumba hilo lipo katika hali isio nzuri, serikali tumeiona hali hio na lengo na madhumuni ya serikali kama nilivyoeleza hapo awali ni kuzifanyia matengenezo nyumba zote.

Lakini tunaangalia hali ya uchumi na hali ya bajeti yetu, ndio tukasema tunatafuta wahisani. Pindi tukipata wahisani basi aidha jumba hilo tutalifanyia ukarabati au tutajenga jengine jipya kabisa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR)Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba

kuongezea majibu juu ya jengo ambalo Mhe. Mwakilishi ametaka kulifahamu.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imeshafanya maamuzi juu ya jengo lile, kulifanyia ukarabati wa hali ya juu ili liweze kunusuru maisha ya watumiaji wa jengo lile. Tumeshafanya kikao cha kwanza na taasisi mbali mbali za fedha na wameonesha nia ya kulikarabati jengo lile na hivi leo saa nane tutakuwa na kikao cha pili ambacho kitatoa muongozo juu ya kuanza kufanya michoro ya ukarabati juu ya jengo lile ili tuweze kupata makisio halisi yanayohitajika.

Ni matarajio yangu kwamba sio muda mfupi tutakamilisha hiyo michoro kutoka kwa wenzetu wa Idara ya Ujenzi na taasisi za fedha zipo tayari ili tuanze kulifanyia ukarabati jengo lile. Tunachowaomba wananchi ambao wanaotumia jengo lile ni kwamba waanze kufanya maamuzi sasa hivi ya kuondosha shughuli zao ndani ya jengo lile, kwa sababu jengo lipo katika hali ambayo si nzuri ili kuruhusu serikali kuendelea na ukarabati wa jengo hilo, na baadae serikali imeshafanya maamuzi kwamba wao watapewa nafasi za kwanza kurudi ndani ya jengo hilo kwa matumizi ya biashara zao.

Namuomba Mhe. Mwakilishi avute subra lakini katika kipindi kifupi tutaweza kukamilisha hiyo hatua ambayo niliomuelezea.(*Makofi*).

Nam. 43
Wastaafu Kulipishwa Kodi ya Mapato Katika Ajira Nyengine

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa (Kny: Mhe. Mgeni Hassan Juma)- Aliuliza:-
Kwa nini wastaafu waliomaliza kufanya kazi serikalini wakiajiriwa katika taasisi nyengine wanaendelea kulipa kodi yaani *(income tax).*

Je, kwa sheria ipi inawataka wastaafu hawa kuendelea kulipa kodi wakati tayari wameshalipa kodi kipindi kirefu katika utumishi wao Serikalini.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR)Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kujibu swali la Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato Nam. 11 ya 2004 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inawataka waajiri wote waliopo katika sekta ya umma na binafsi kuwakata kodi ya mapato *(income tax)* watumishi wao walioajiriwa ambao kipato chao ni zaidi ya kima cha chini cha mshahara kwa mwezi.

Aidha, sheria hii haijatenganishwa ulipaji wa kodi ya mapato kutokana na ajira kwa mtu ambaye amestaafu na kuajiriwa upya au kwa mtu ambaye anaajiriwa kwa mara ya kwanza. Hii imetokana na kwamba kodi hii ni ya mapato.

Mhe. Mwenyekiti, wastaafu wanapoajiriwa tena katika taasisi nyengine ya umma au binafsi wanapaswa kulipwa kodi ya mapato *(income tax).* Sababu kuu ya kufanya hivyo ni kwamba wamepata kipato chengine ambacho kwa mujibu wa sheria hupaswa kulipiwa kodi ya mapato.

Halikadhalika Sheria ya Kodi ya Mapato haijaweka muda maalum (ukomo) kwa muajiriwa kuacha kulipia kodi ya mapato.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema ikafahamika kuwa ulipaji wa kodi ni kwa ajili ya maendeleo na sio vyenginevyo. Kwa maana hiyo kila kodi inayolipwa ina maana yake na ipo kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae ametuwezesha kufika katika Baraza hili tukufu kwa usalama na afya njema. Lakini pia na mimi nichukue nafasi hii Mhe. Mwenyekiti, nitoe pole kwa watu wa Micheweni kwa kifo cha ndugu yetu Salim Hamad ambae alikua ni Mwakilishi wa Baraza hili, lakini pia alikuwa ni mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa suala hili linahusiana na mambo ya ustaafu. Nitaomba nimuulize Mhe. Waziri, ni lini serikali itaongeza kima cha wastaafu ambao ni pencheni, ukiangalia kwa kweli pencheni ya wastaafu haikidhi haja. Nitamuomba Mhe. Waziri, pamoja na ukwasi tulionao katika serikali lakini wakae wazingatie ili pencheni hizi ziongezwe. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kujibu kuwa serikali imeanza kulitafakari suala hili na tumeanza kulifanyia kazi suala hili, pengine panapomajaaliwa tunategemea wakati wowote katika kipindi chochote kwenye bajeti ijayo tutaanza kulifikiria hili suala la kuongeza pencheni za wafanyakazi waliostaafu. (*Makofi*).

Nam. 48
Utamaduni wa Mavazi ya Akinamama

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Hivi sasa umeingia utamaduni wa Akinamama kuvaa mavazi ya kiume kama vile suruali na shati hali inayosababaisha jamii kushindwa kuwatofautisha ukiachilia mbali tofauti za maumbile zinazoonekana wazi.

(a) Je, utamaduni huu umetokea wapi.

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuna kasoro zinazojitokeza katika kutazama mavazi hayo.

(c) Je, huu ndio utamaduni wa maendeleo ya Akinama wa Kizanzibari.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-
Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 48 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Lakini kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi niruhusu Mhe. Mwenyekiti, niseme mambo mawili.

La kwanza, jibu hili limeshughulikiwa na Kamisheni ya Utamaduni na Michezo ambayo Bodi ya Sensa ya Filamu ya Muziki na Sanaa za Maonesho ni sehemu ya kamisheni hiyo na kama ulivyoarifiwa hapa na Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Salim Hamad Saleh, ambaye amefariki jana na anazikwa leo alikuwa mwenyekiti mstaafu wa Bodi ya Sensa, Filamu na Maonesho. Marehemu alipokuwa mwenyekiti wa Bodi ya Sensa alitoa mchango mkubwa katika kulinda mila, silka na utamaduni wa Wazanzibari. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aiweke mahali pema roho yake.

Lakini la pili, Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa niaba ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo nimpe pongezi nyingi ambae ameuliza swali hili Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwa namna ambavyo anashirikiana na wizara yangu katika kulinda silka, mila na utamaduni wa Wazanzibari hasa katika Jimbo lake la Muyuni ambako kwa kweli amekuwa mstari wa mbele sana katika maeneo ya Paje, Bwejuu na Jambiani kuhakikisha kwamba mila, silka na utamaduni wa Wazanzibari zinalindwa.

Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waige mfano wa Mhe. Jaku katika kushirikiana na wizara yangu katika kuona kwamba kwenye majimbo yao basi mila, silka na utamaduni wa Wazanzibari yanadumishwa.
Baada ya maneno hayo Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kujibu swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Utamaduni huu wa wanawake wa Kizanzibari kuvaa mavazi ya kiume yametokana na Wazanzibari kuwa wepesi wa kuiga tamaduni za nchi za nje.

(b) Serikali na jamii inaona ipo kasoro katika kutazama akinamama waliovaa mavazi ya kiume hasa suruali zenye kubana na shati zenye kubana.

(c) Kuvaa suruali zenye kubana na shati zenye kubana sio maendeleo na utamaduni wa Mzanzibari.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ama nitakuwa mwizi wa fadhila na mimi binafsi hasa sisi Waislamu kama sikumshukuru Mhe. Waziri, kwa uwezo, umakini, kipaji chake, busara zake, na fikra na mawazo yake.

Mhe. Waziri wananchi wa Jimbo la Muyuni hasa Shehia ya Paje, Jambiani na Bwejuu wanakushukuru sana, tena sana kupita kiasi.Baada ya shukurani hizo naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

a) Serikali ina mpango gani kupiga marufuku mavazi yanayokwenda kinyume na mila, utamaduni wa Mzanzibari ikiwemo nguo zinazoonesha vazi la ndani, maarufu zinaitwa majanga.

b) Serikali ina mpango gani wa kukagua bidhaa za nguo kabla ya kuingiza katika soko kutokana na nguo nyingi zinazokwenda kinyume na mila na utamaduni ambapo ni chanzo cha wanaume kuingia katika matamanio ya suruali za akinamama *(skin tight).*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, kwanza kuna sheria ambayo inakataza mambo haya, Sheria Nam. 1 ya 1973, ni sheria kongwe kidogo. Lakini katika sheria hii msimamizi wa sheria hii ni wananchi wenyewe. Naomba Mhe. Mwenyekiti, uniruhusu kunukuu kifungu kimoja ambacho labda kitawapa faida Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi kwa jumla katika usimamizi wa sheria hiyo.

Kifungu cha 7 naomba nikinukuu kama kilivyo:-

> *"A person who are suspected or contravenial the provision of this decree may be arrested by a citizen in the presence of two*

respectable witnesses who agree that an offence has been committed, the person arrested shall immediately be taken to nearest Police Station a company by two witnesses", mwisho wa kunukuu.

Ninachokusudia kusema ni kwamba sheria tunayo na wasimamizi wa sheria hii ni wananchi wenyewe wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo yapo mambo ya kufanya kwa wananchi wenyewe kwa sababu kama unamuona mwananchi mwanamke wa Kizanzibari amevaa nguo ambayo ni kinyume na utaratibu wa sheria hii, mwananchi yeyote kwa mujibu wa *decree* hii anaruhusa ya kutafuta wenzake wawili wa kumkamata na kumpeleka Polisi. Kwa hivyo, bado ni jukumu letu pamoja si la serikali pekee.

b) Kuhusu suala la kuingiza au kukataza nguo zisizokubaliwa Mhe. Mwenyekiti, ninadhani kwamba suala hili halipaswi kuingiza kukataza uingizaji wa nguo, kwa sababu linaweza kutumiwa kwa matumizi mapana. Ninachotakiwa kufanya ni kukataza uvaaji wa nguo zenyewe. Kwa hivyo hilo ndilo la kulifanyia kazi zaidi.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kwa kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.Kwa kuwa wapo pia akinababa siku hizi wanaosuka nywele na pia wapo wanaovaa herini. Je, nao huu ndio utamaduni wa maendeleo ya akinababa wa Kizanzibari.

Lakini swali la (b) kushughulikia suala hili la upotevu wa mila na desturi kwa upande wa akinamama tu, hatuoni kuwa ha-*solve* tatizo wakati wapo akinababa pia ambao wanakwenda kinyume na mila na desturi za Mzanzibari.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, katika sheria ambayo nimeitaja nalo hilo Mhe. Wanu amelizungumza ni kosa kwa mwanamme kuvaa mavazi ya mwanamke. Kwa hivyo, ni jukumu tena la sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilshi na wananchi kwa jumla ukimuona mwananchi wa kawaida, akimuona mwanamme amevaa herini basi sheria hii imempa nguvu ya kutafuta wenzake wawili wa kumkamata na kumpeleka Polisi.

Kwa hivyo, bado suala lipo sisi wenyewe Wazanzibari kuisimamia sheria hii ili kulinda, mila na utamaduni wa Wazanzibari.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanaridhisha. Mimi nilikuwa ninataka tu nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na mkanganyiko wa mawazo namna ya mavazi ya Kizanzibari. Sasa Waingereza wao mavazi yao makubwa ya utamaduni wanavaa sketi wanaume. Sasa sijui kwa sisi Wazanzibari kivazi halisi cha utamaduni wa Zanzibar kwa mwanamme avae vipi. Vile vile, kwa mwanamke avae vipi ili kuweza kujua hasa kwamba yule mwananchi wa Zanzibar amevaa kivazi ambacho kinachotambulika kiserikali, lakini vile vile kiutamaduni wa Zanzibar.

Na kwa upande wa Oman wao huwa wanavaa kanzu na lemba. Sasa labda kwa upande wa Zanzibar kivazi chetu hasa ni kivazi kipi. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa *decree* hiyo ambayo nimeitaja, vazi la utamaduni wa Mzanzibari ni vazi la heshima. Vazi lolote lile ambalo lina heshima basi hilo ndio vazi la utamaduni wa Mzanzibari.

Kwa hivyo, katika sheria hiyo kuna mambo yametajwa kama haya, nguo hii ukivaa itakuwa si nguo ya heshima kwa mwanamme. Kuna vifungu vitano na kwa wanawake kuna vifungu vinne ambavyo vinaonesha kwamba nguo hii ukivaa itakuwa ni nguo ya heshima kwa mwanamke.

Kwa hivyo, mavazi hayo ndio mavazi ya utamaduni wa Mzanzibari. Sheria hiyo imeweka vizuri na imeelekeza. Kwa hivyo, ningeomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wairejee decree Na. 1 ya 1973 watajua lipi vazi la heshima la Mzanzibar ambalo litakuwa ndio ni vazi la utamaduni wetu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, wale ambao wapo nje tunaomba waiingie ndani ili Mwenyekiti atakaposoma taarifa yake waweze kupata mustakabali mzuri na wajipange vizuri katika kuchangia ili Wajumbe wasije wakatoka nje ya mada yetu.

HOJA ZA KAMATI TEULE

Mhe. Ali Mzee Ali (Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi): Mhe Mwenyekiti, ninapenda kuchukua nafasi hii adhimu kukwambia kwamba leo utaweka historia ya kuongoza Baraza kwenye jambo ambalo ni jambo nyeti katika nchi hii. Ninapenda kukupa hongera kwa hilo.(*Makofi*).

Waheshimiwa Wajumbe wenzangu ninatumai nyote ni wazima na ninaomba munisikilize. Mhe. Mwenyekiti, ninakuomba sana uwape nafasi ya kutosha Wajumbe wa Baraza hili kuichangia, kuichambua hatimaye tufike pahala pema. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninaanza.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2012 ambayo inatoa uwezo kwa Baraza kuunda Kamati Teule kwa ajili ya jambo fulani, Baraza liliunda Kamati Teule kwa ajili ya kuchunguza baadhi ya migogoro ya ardhi hapa Zanzibar. Migogoro hiyo iliibuliwa na Wajumbe mbali mbali wakati wa Mkutano wa Bajeti wa mwaka wa Fedha 2012/2013 na baadhi ya migogoro hiyo ilitokana na taarifa ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi.

Baada ya wewe Mhe. Mwenyekiti, kutafakari kwa umakini na kwa busara kubwa siku ya tarehe 10 Agosti, 2012 uliwateua wajumbe wafuatao kuunda Kamati Teule hiyo:-

1. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
3. Mhe. Ali Mzee Ali
4. Mhe. Fatma Mbarouk Said
5. Mhe. Nassor Salim Ali

Aidha Kamati ilisaidiwa shughuli zake na Makatibu wawili ambao ni Ndg. Mussa Kombo Bakari na Ndg. Khamis Hamad Haji. Barua za uteuzi kwa Wajumbe wa Kamati zilitolewa tarehe 22/08/2012 na Kamati ilikutana kwa mara ya kwanza tarehe 15 Oktoba, 2012 kwa ajili ya kumteua Mwenyekiti wa Kamati ambapo katika kikao hicho, wajumbe walimchagua Mhe. Ali Mzee Ali, kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

Pamoja na malalamiko mbali mbali yanayohusiana na migogoro ya ardhi kuwasilishwa mbele ya Kamati wakati Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake, Kamati ilifanya kazi zake kwa mujibu wa Hadidu Rejea ilizopatiwa na Baraza ambazo zilikuwa kama ifuatavyo:-

1. Maeneo ambayo yanalalamikiwa kuwa umiliki wake umefutwa kutoka kwa watu waliopewa umiliki wa maeneo hayo bila ya kufuata taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria;

2. Maeneo ambayo yalikuwa yanatumiwa na wananchi kwa shughuli zao za kuendesha maisha, lakini yamechukuliwa bila ya kuzingatia maslahi ya wananchi waliokuwa wanayatumia;

3. Wawekezaji wanaochimba mchanga kwenye maeneo ya fukwe;

4. Mgogoro wa ardhi baina ya serikali na wananchi (wakulima), Bambi;

5. Mgogoro wa Ardhi baina ya mfanyabiashara na wakulima, Tumbe;

6. Mgogoro wa maeneo ya ardhi ya wananchi yaliyonyang'anywa na kufanywa vitega uchumi, Makangale;

7. Mgogoro wa ardhi kati ya wananchi na viongozi wa serikali, Mchangamle, Kizimkazi;

8. Mgogoro wa ardhi kati ya wananchi, Vitongoji Makaani;

9. Mgogoro wa ardhi baina ya wanakijiji na Muekezaji, Pwani Mchangani;

10. Mgogoro wa ardhi baina ya wananchi na viongozi wakuu wa juu wa serikali, Tondooni Mkunguni, Pemba;

11. Mgogoro wa ardhi baina ya Idara ya Upimaji na Ramani na Wizara ya Kilimo, Tumbe, mgogoro ambao umepelekea wananchi kulivamia eneo hilo;

12. Mgogoro wa ardhi baina ya wananchi na muwekezaji, Shehia ya Mzwardini, Bwejuu.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema ikafahamika kuwa pamoja na hadidu rejea ilizopatiwa Kamati Teule kuwa kumi na mbili, hadidu rejea namba moja na namba mbili zilitajwa kwa ujumla jumla bila ya kuweka wazi migogoro yenyewe na hivyo Kamati ilifanya kazi ya kupitia *hansard* ili kupata migogoro mahsusi ambayo Kamati iliifanyia kazi. Hivyo, maeneo ambayo Kamati hii iliyafanyia kazi yaliongezeka kutoka kumi na mbili hadi kufikia maeneo ishirini na moja. Baada ya kupitia *hansard* kuhusiana na hadidu rejea namba moja, Kamati ilipata kadhia nane ambazo ilizifanyia kazi. Kadhia hizo ni hizi zifuatazo:-

1. Kadhia ya mgogoro wa ardhi Maruhubi unaomuhusisha Bw. Ali Muradi,
2. Kadhia ya mgogoro wa ardhi unaohusisha kampuni ya *Leisure Corp*,(*Al Nakheel*)

3. Kadhia ya mgogoro wa ardhi unaohusisha kampuni ya *Sovereign Sands Resort,*

4. Kadhia ya mgogoro wa ardhi unaohusisha kampuni ya *SAGO Palm,*

5. Kadhia ya mgogoro wa nyumba ya Mazizini ambayo nyumba hii ilikuwa apewe Balozi wa Oman,

6. Kadhia ya mgogoro katika kisiwa cha Kwale,

7. Kadhia ya mgogoro wa ardhi unaohusisha kampuni ya *Sunset Paradise Resort,*

8. Kadhia ya mgogoro wa ardhi unaomhusisha Bw. Bruno Conti.

Aidha katika hadidu rejea nambari mbili, Kamati baada ya kupitia *hansard* ilipata maeneo matatu ya kuyafanyia kazi chini ya hadidu rejea hiyo. Maeeneo hayo ni haya yafuatayo:-

1. Mgogoro wa mashamba ya Selem

2. Mgogoro wa mashamba ya Kijichi

3. Mgogoro wa mashamba ya Dole

Kamati hiyo ilianza rasmi kazi ya kuchunguza migogoro ya ardhi iliyotajwa tarehe 29 Oktoba, 2012. Kamati iliwahoji wahusika mbali mbali wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walioibua hoja hizo ndani ya Baraza, watendaji wa taasisi mbali mbali, wananchi wanaohusika na migogoro hiyo na watu wengine mbali mbali. Aidha Kamati ilitembelea maeneo mbali mbali yenye migogoro na kupata maelezo kutoka pande zilizohusika na migogoro hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati katika kuchunguza migogoro hiyo ya ardhi ilifanya kazi zake kwa muda wa siku ishirini ambapo kwa upande wa Unguja Kamati ilifanya kazi kwa siku kumi na tano na kwa upande wa Pemba ilifanya kazi kwa siku tano za kazi. Hatimae Kamati ilikutana kwa muda wa siku saba kwa ajili ya uchambuzi wa hoja na vielelezo vilivyowasilishwa mbele ya Kamati pamoja na kupitia ripoti ya Kamati na kufanya maamuzi kwa kila jambo lililoshughulikiwa na Kamati.

Kamati katika kutekeleza majukumu yake ilizingatia misingi ya sheria ya Kinga, Nguvu na Uwezo ya Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2007 na Kanuni

za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2012. Kwa mfano Kamati ilizingatia Kanuni ya 108(17) inayotaka Kamati kutoshughulikia jambo lolote linalosubiri uamuzi wa mahakama. Baada ya kupata taarifa za kuwepo kwa kesi mahakamani katika baadhi ya migogoro, Kamati ilifuatilia kwa kuandika barua kwa taasisi zinazohusika ili kupata ufafanuzi juu ya kuwepo kwa mashauri katika mahakama kuhusiana na jambo ambalo lina uhusiano na hadidu rejea za Kamati Teule na baada ya kuthibitishiwa kuwepo kwa kesi katika kadhia hizo, kamati ilisita kushughulikia masuala hayo.

Aidha, kamati ilizingatia kanuni ya 123 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi inayoelekeza kuwa Kamati Teule kuwasilisha taarifa yake pamoja na vielelezo. Kamati hii kwa kuelewa matakwa hayo ya kanuni, ilijitahidi kukusanya vielelezo kwa kuwasiliana mara kwa mara na baadhi ya wafanyakazi wa serikali pamoja na kuweka msisitizo kwa taasisi hizo kuipatia kamati vielelezo vilivyohitajika. Kamati ilifanikiwa kupata baadhi ya vielelezo hivyo ambavyo vinaambatanishwa na ripoti hii na ambavyo vinafafanuliwa katika hadidu rejea husika. Hata hivyo, kamati ilishindwa kupata baadhi ya vielelezo ilivyohitaji pamoja na hatua zilizochukuliwa za kuzungumza na watendaji na kuwaandikia barua kuhitaji vielelezo hivyo.

Historia Fupi ya Ardhi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ardhi imekuwa ni tatizo kubwa kwa nchi nyingi zilizotawaliwa duniani. Kwa hapa Zanzibar ardhi ilimilikiwa na watawala chini ya Sultan na wageni walipoingia ndani ya nchi walitafuta ardhi yenye rutuba. Kwa hivyo, ardhi yenye rutuba kwa kiasi kikubwa wakati wa ukoloni ilimilikiwa na watu wachache na wananchi waliokuwa wengi hawakuwa na ardhi hasa ile yenye rutuba.

Kwa mfano mashamba makubwa 745 yaliyokuwepo Unguja na Pemba wakati wa Sultan yalimilikiwa na makabaila na mabepari 73 tu. Orodha ya mashamba makubwa na mabepari na makabaila waliokuwa wakiyamiliki inaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho namba KTA 1A.

Ahadi ya Chama cha Afro Shiraz Kuhusu Ardhi.

Kutokana na hali hiyo ya kutokuwepo kwa usawa katika umiliki wa ardhi hapa nchini, harakati za kuwakomboa wananchi wa Zanzibar kwa kuwafanya nao wamiliki rasilimali za nchi na hivyo kuondokana na unyonge waliokuwa nao zilianza hata kabla ya Mapinduzi ya 1964.

Tarehe 8 Machi, 1959, hapo Machui, Kiongozi Mkuu wa Chama cha Afro Shiraz Marehemu Sheikh Abeid Aman Karume, alitangaza kuwa Afro Shiraz

ikipata serikali, ardhi yote itakuwa mali ya wananchi wa Zanzibar. Kutokana na ahadi hiyo kulikuwa na madhila na unyonge waliofanyiwa wakulima waliokuwa chama cha Afro Shiraz na kuondolewa katika mashamba waliokuwa wakilima na hatimae Chama cha Afro Shiraz kikanunua shamba la Kilombero na kuwakabidhi wanachama wake ili waweze kuendesha maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, Mapinduzi matukufu yalifanyika tarehe 12 Januari mwaka 1964 na Rais mstaafu wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, tarehe 8 Machi, 1964 alitangaza na kutekeleza ahadi ya *ASP* iliyotolewa Machui mwaka 1959, kwa kutoa taarifa muhimu ambayo ni Azimio la Jamhuri ya Zanzibar. Azimio hilo lilikusudia kuiweka ardhi yote mikononi mwa serikali kwa ajili ya kuigawa kwa wananchi kwa usawa. Nakala ya Azimio hilo inaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho KTA 1B.

Azimio hilo lilifuatiwa na sheria mbali mbali ikiwemo Sheria ya ‘’*The Confiscation of Immovable Property Decree*, 1964’’ na Sheria ya Ugawaji wa Ardhi ‘’(*The Land (Distribution) Decree, 1966*’’ ili kutekeleza azma ya kuiondoa ardhi mikononi mwa makabaila na mabepari wachache na kuwapatia wananchi walio wengi ardhi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya kugawa ardhi ilianza rasmi kwa Unguja tarehe 8/11/1965 kwa shamra shamra na sherehe kubwa sana katika ardhi ya Dole, Wilaya ya Magharibi katika Shamba la Mfalme Hemed bin Thuwein ambapo hadi mwaka 1973, eka 24,000 ziligaiwa kwa wananchi. Kwa upande wa Pemba kazi hiyo ya kugawa ardhi kwa wananchi ilianza Mbiji, Wilaya ya Mkoani, na hadi kufikia mwaka 1972, eka 72,000 zilishagaiwa kwa wananchi.

Aidha, katika kudhihirisha azma yake ya kuwanyanyua wananchi hao kiuchumi, serikali iliwasaidia kwa kiasi kikubwa wananchi waliojishughulisha na kilimo, kwanza kwa kutowatoza kodi yoyote kwa maeneo waliyopewa tofauti na ilivyokuwa kabla ya Mapinduzi ambapo wananchi hao walipaswa kulipa kodi kwa maeneo waliyokuwa wakilima. Aidha, baada ya kuwapatia wananchi eka tatu, serikali ilianza kuwatoza wananchi shilingi 28 kwa eka moja kwa kuchimbuliwa na kuburugiwa tofauti na ilivyokuwa kabla ya Mapinduzi ambapo wananchi hao walilipa Shilingi 75 kwa kuchimbuliwa tu bila ya kuburugiwa.

Baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964, zilitungwa sheria zilizoweka misingi ya Mapinduzi. Sheria hizo zinajumuisha *The Legislative Powers Law*, 1964 ambayo ilitoa mamlaka kwa Baraza la Mapinduzi kutunga sheria, *The Constitutional Government and the Rule of Law Decree, 1964, The Equality, 1964, High Court Decree*, 1964 na Sheria Nam. 6 ya mwaka 1964

inayojulikana kama ‘’*Reconciliation and Unity of Zanzibar Peoples Decree*’’ ambayo nakala ya Kiswahili inaambatanishwa na ripoti kwa ajili ya rejea kwa Waheshimiwa Wajumbe kama Kiambatanisho Nam KTA 1C.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hizi ziliweka misingi ya utawala wa sheria katika nchi na kuweka misingi ya usawa na utu miongoni mwa wananchi na kuondokana na misingi ya kubaguliwa kutokana na rangi, ukabila, jinsia au kwa namna yoyote. Sheria hizi pia ziliimarisha miongoni mwa wananchi usawa, umoja na kujenga muafaka baina yao. Aidha, sheria hizo ziliweka misingi hiyo ya usawa kwa kutangaza rasmi kuwa kila raia wa Zanzibar ana haki iliyo sawa katika kupata

Waheshimiwa Wajumbe, jana sijalala na hizi ndio ishara zake. Lakini namshukuru Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amenipa hii tasbihi.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Mhe. Ali Mzee Ali: Aidha, sheria hizo ziliweka misingi hiyo ya usawa kwa kutangaza rasmi kuwa kila raia wa Zanzibar ana haki iliyo sawa katika kupata haki, fursa na ulinzi kwa uraia wake.

Mhe. Mwenyekiti, ili kufahamu umuhimu na uzito wa sheria Nam. 6 ya mwaka 1964, tunaomba kunukuu baadhi ya vifungu vya sheria hiyo kama ifuatavyo:-

Kifungu cha 2.	"Madhumuni makuu ya Mapinduzi ya Watu wa Zanzibar ni kutokomeza upendeleo wa kiuchumi, kijamii au upendeleo wa kisheria na mapungufu yote yaliyopita yaliyokuwa yanawagawa wananchi na makundi mbali mbali ya raia kwa njia ya ukabila, jinsia, dini au uasili wa mtu, na madhumuni hasa ya Mapinduzi ni kukuza usawa, maridhiano na umoja kwa Watu wa Zanzibar.
Kifungu cha 3.	"kwa msingi huo, kila raia wa Zanzibar anatangazwa kuwa ana haki sawa, fursa na hifadhi ya uraia wake kama vile ambavyo anatekeleza majukumu na wajibu wake wa uraia. Hakuna haki, fursa au hifadhi inayoweza kufutwa kisheria kwa raia yeyote kwa kutumia vyombo vya

dola au kwa kutumia hatua za mtu binafsi kwa sababu ya msingi au kisingizio cha ukabila, dini, jinsia au uasili wa raia huyo''.

Kifungu cha 4. "hakuna kifungu chochote ndani ya sheria hii kitakachoizuia serikali kutunga sheria itakayotoa nafuu maalum au upendeleo wa kiuchumi, kiutamaduni au kijamii kwa raia waliokosa haki za msingi kwa madhumuni ya kuwaletea usawa kama raia''.

Mhe. Mwenyekiti, misingi ya Mapinduzi ya mwaka 1964 ni kuwakomboa wananchi na kuimarisha hali za wananchi wote wa Zanzibar na kuondoa tofauti kubwa ya kipato iliyokuwepo wakati wa ukoloni. Kwa msingi huo, ndio maana mageuzi ya ardhi (*Land Reform*) yaliyofanywa Zanzibar yalikusudia kugawanya ardhi kwa wananchi masikini wa Zanzibar na kuitoa ardhi hiyo mikononi mwa mabepari wachache. Azma hii inathibitishwa na maneno ya Marehemu Sheikh Abeid Aman Karume aliyoyatoa mara baada ya mapinduzi ya mwaka 1964 na Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu baadhi ya maneno hayo kama ifuatavyo:-

"Sisi tumejitawala ili uchumi wa nchi hii uwe mikononi mwetu. Ikiwa yupo kiongozi anayewapa wageni fursa ya uchumi wa nchi, basi hafai. Tunataka pato la nchi hii liwarejee wenyewe wananchi''.

Anaendelea.
"Mwenyezi Mungu katujaalia mambo mawili makubwa sana katika nchi yetu. La kwanza sisi ni kidogo, na la pili tunayo ardhí nzuri yenye rutuba ambayo watu wengi duniani hawana''.

Anaendelea.
"Kama tulivyoupindua usultani sasa tunaupindua ubepari. Mtu mmoja kuwa na eka elfu tatu peke yake, na watu wengine wakawa hawana kitu, hapa kwetu mpango huo basi''.

Hayo ndio maneno ya Jemedari Mkuu wa Mapinduzi, ambayo kesho kutwa tuna sherehekea miaka 50.

Inabidi nirejee tena.

> "Kama tulivyoupindua usultani sasa tunaupindua ubepari. Mtu mmoja kuwa na eka elfu tatu peke yake, na watu wengine wakawa hawana kitu, hapa kwetu mpango huo basi''.

Maneno haya mazito na yaliyojaa uzalendo yanafaa kuenziwa kwa vitendo, wakati tukikaribia kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi yetu kwa kuzingatia kuwa suala la serikali kuichukua ardhí na kuigawa kwa wananchi ilikusudia kurejesha utu kamili. Marehemu Sheikh Abeid Aman Karume alisema na namnukuu;

> "Katika mwaka 1964, tulichukua hatua ya kurejesha utu kamili, kwa kufanya ardhí ni mali ya wananchi wote''

Mhe. Mwenyekiti, katika usimamizi wa suala la ardhi, sheria nyingi zimetungwa toka wakati wa utawala wa Sultan ili kuratibu usimamizi huo. Katika kipindi cha miaka ya 1963 kabla ya Mapinduzi ya mwaka 1964 kuanzia mwaka 1900 hadi mwaka 1963, sheria 8 zinazohusiana na masuala ya ardhi zilitungwa. Orodha ya sheria hizo inaambatanishwa na ripoti hii kama kiambatanisho Nam. KTA 1D, yaani tangu 1900 mpaka 1963 sheria 8 zilitungwa na zote tumezitia ndani.

Katika kipindi cha miaka arobaini na tisa baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 hadi sasa, sheria 17 zinazohusiana na masuala ya ardhi zimetungwa. Orodha ya sheria hizo inaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho Nam. KTA 1E.

Kutungwa kwa sheria hizi kunadhihirisha uzito wa suala hili la ardhi hapa Zanzibar ambapo pamoja na kuwepo kwa sheria zote hizo zinazosimamia ardhi, bado migogoro ya ardhi imejitokeza na inaendelea kujitokeza katika sehemu mbali mbali hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, historia inaonyesha kuwa migogoro hii imeanza muda mrefu toka enzi ya ukoloni na kamati hii ilipata fursa ya kupitia ripoti ya Bw. R.H.W Pakenham ya mwaka 1946.

Haya mambo hajayaanza na Ali Mzee Ali tu, hapana. Mwaka 1946 mgogoro wa ardhi na uliongozwa na Bw. Pakenham. Inayoonyesha namna alivyofanya uchunguzi katika mgogoro wa ardhi miongoni mwa wahadimu huko Chwaka, mgogoro ambao ulihusisha vijiji vya Shahafi na Mkanjani. Bw Pakenham aliteuliwa kuchunguza mgogoro huo, tarehe 5 Febuari,1944 kupitia Gazeti Rasmi la Serikali na kutakiwa kutoa ripoti si zaidi ya tarehe 30 Juni, 1944.

Mhe. Mwenyekiti, mgogoro mwengine wa ardhi uliojitokeza Zanzibar na kufanywa uchunguzi maalum ni ule wa Vitongoji katika Mudiria ya Chake Chake, Pemba ambapo tarehe 29/08/1955 Sir John Gray aliteuliwa kuchunguza mgogoro huo na kutakiwa kuangalia watu wenye haki katika maeneo hayo. Mgogoro huo uliwahusisha Sheikh Abdulla bin Mbarak el-Mauli na familia yake, Khamis bin Faki Shiraz na wenzake 13, Hassan bin Ali na Nassor bin Khalfan el- Yorubi. Kamati inapenda kuambatanisha sehemu ya utangulizi na mapendekezo ya ripoti hiyo ya Sir. John Gray ili wajumbe waweze kufanya rejea.

Ripoti nyengine zilizowahi kuelezea masuala ya ardhi ni pamoja na *Land Tenure System and Land Reform in Zanzibar, 1830- 1870,* ya Prof. Ibrahim Fokas Shao, utafiti uliofanywa na *W.R. McGeagh and W. Addis, Review of the Systems of Land Tenure in Zanzibar and Pemba, Zanzibar* 1934 na ripoti ya *Land Tenure in Zanzibar ya mwaka 1961* ya John Middleton na nyingi nyenginezo.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tu nilikuwa nawaonesha namna gani mambo ya ardhi na matatizo yake, ripoti kama 5 hivi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo pamoja na historia fupi ya masuala ya ardhi hapa Zanzibar, sasa naomba kuwasilisha taarifa ya namna hadidu rejea zilivyoshughulikiwa, pamoja na uamuzi na mapendekezo ya kamati kama inavyoainishwa katika bango kitita hapa chini.

Waheshimiwa Wawakilishi, ndugu zangu nafikiri tangu asubuhi tumepata hii ripoti na wengi nimewaona wakisoma soma na wengine walikaa vikundi wanafanya mjadala, nawapongeza. Sasa naanza kazi ambayo tulitumwa.

Katika hadidu rejea hii kamati ilizingatia hoja mbali mbali ambazo Hadidu Rejea ya kwanza Maeneo ambayo yanalalamikiwa kuwa umiliki wake umefutwa kutoka kwa watu waliopewa umiliki wa maeneo hayo bila ya taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria.Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati Katika Hadidu Rejea hii, kamati ilizingatia hoja mbali mbali ambazo zilizungumzwa na wajumbe wa Baraza ambazo zilihusu maeneo yanayolalamikiwa kuwa umiliki wake umefutwa na kupewa wengine bila ya kufuata utaratibu wa kisheria. Narudia tena, bila ya kufuata utaratibu wa kisheria. Hoja kuhusu maeneo hayo zinafafanuliwa hapa chini:-

1. Kadhia ya Bw. Ali Muradi

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati

Kamati katika kushughulikia suala hili ilimualika Mjumbe wa Baraza aliyeibua hoja hii ndani ya Baraza, Mheshimiwa Ali Salum Haji.

Mjumbe huyo aliieleza kamati kuwa aliibua hoja hii baada ya kupata malalamiko ya Bw. Ali Muradi kuwa amenyang'anywa eneo alilopatiwa kwa mujibu wa sheria akiwa na hati na kupewa mtu mwengine.

Mjumbe huyo aliendelea kuieleza kamati kuwa pamoja na waziri anayehusika na ardhi, kulieleza Baraza kuwa suala hilo limeshamalizika baada ya kumpatia Bw. Ali Muradi eneo jengine, mgogoro huo bado upo kutokana na kutokuwepo kwa makubaliano baina ya pande zinazohusika.

Aidha, kamati ilitembelea eneo linalodaiwa kuchukuliwa kutoka kwa Bw. Ali Muradi na kupewa kampuni ya *Zanzibar Dairy Products* kwa makusudio ya kumpatia eneo jengine Bw. Ali Muradi kama ilivyoelezwa na Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati wakati wa bajeti ya wizara yake mwaka 2012/2013, kwa mujibu wa Hansard ya tarehe 13 Julai, 2012, ukurasa wa 73.

Mhe. Mwenyekiti, katika ziara hiyo kamati ilifuatana na watendaji wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, wakiongozwa na Mkurugenzi wa Ardhi na Usajili.

Watendaji hao wa wizara waliionyesha kamati eneo ambalo Bw. Ali Muradi alikuwa akilimiliki, na kueleza kwamba eneo hilo lilionekana kufaa sana kuongeza (*extension*) eneo la kiwanda cha *Zanzibar Diary Products*, na hivyo Bw. Ali Muradi kupatiwa eneo jengine ili kupisha utanuzi wa eneo la Kiwanda hicho cha Maziwa.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na Bw. Ali Muradi kutokuwepo katika ziara hiyo iliyofanywa, kamati ilifanya juhudi na kukutana na Bw. Ali Muradi ambaye mara nyingi amekuwa nje ya Zanzibar kutokana na shughuli zake. Kikao hicho baina ya kamati na Bw. Ali Muradi kilifanyika katika Afisi ya Baraza la Wawakilishi, tarehe 16/07/2013.

Bw. Ali Muradi aliieleza kamati kuwa alikiomba kiwanja hicho kilichokuwa kikimilikiwa na Wizara ya Kilimo kwa barua, na baada ya mashauriano baina ya Wizara ya Kilimo na wizara iliyokuwa inashughulikia ardhi, alikabidhiwa rasmi kiwanja hicho kwa hati, tarehe 10/12/2003. Hati hiyo ni sehemu ya ripoti ya kamati, Kiambatanisho nam. KTA 1.

Bw. Ali Muradi aliendelea kuieleza kamati, kuwa eneo hilo alilopewa kwa wakati huo alipopewa lilikuwa halijengeki, kutokana na kupita waya za umeme wa *voltage* kubwa na kuhitaji kufukiwa. Mambo yaliyomlazimu kutumia fedha nyingi na muda mwingi ili kurekebisha mazingira ya eneo hilo.

Aidha, Bw. Ali Muradi alilieleza kamati kuwa alipata kibali cha ujenzi wa ukuta kilichotolewa 3/10/2011, kutoka Baraza la Manispaa Zanzibar. Kibali hicho kinaambatanishwa na ripoti kama Kiambatanisho nam. KTA2.

Kamati pia ilielezwa na Bw. Ali Muradi kuwa baada ya marekebisho kadhaa aliyoyafanya katika kiwanja hicho, ili kiweze kutumika kwa matumizi aliyoyakusudia ambayo ni kuweka kontena (*Container Terminal*), eneo hilo lilibadilika ikiwemo ukubwa wa eneo hilo.

Bw. Ali Muradi alidai kuwa wakati akiendelea na ujenzi, aliamriwa kusitisha ujenzi huo na Idara ya Ardhi na Usajili, kwa kudaiwa kuwa umiliki wa eneo hilo ulishafutwa kwa barua iliyoelekezwa kwa Bw. Ali Muradi, ambaye hata hivyo alikanusha kuwa aliipata barua hiyo. Bw. Ali Muradi aliwasilisha mbele ya kamati, nakala ya barua ya kusitisha ujenzi huo ya tarehe 19/03/2012 ambayo ilieleza kuwa umiliki wa eneo hilo umesitishwa tokea tarehe 29/02/2012. Barua hiyo inafanya sehemu ya ripoti hii kama Kiambatanisho nam. KTA3.

Bw. Ali Muradi aliijibu barua hiyo kupitia kwa wakili wake na kueleza kuwa hakuwahi kuipata barua hiyo na pia hakuwahi kupewa notisi ya ufutaji wa haki ya kulitumia eneo hilo, kama sheria inavyoelekeza. Barua hiyo iliwasilishwa mbele ya kamati na hivyo inakuwa sehemu ya ripoti hii kama Kiambatanisho nam. KTA4.

Tarehe 21/03/2012 Wizara ya Ardhi ilimuandikia tena Bw. Ali Muradi ikimueleza kuwa aliwahi kupatiwa notisi ya kumfutia hati ya matumizi ya eneo hilo, kwa kushindwa kuliendeleza kwa kipindi kirefu na kuambatanisha barua hiyo na nakala ya ukurasa wa kitabu cha kupokelea barua yaani (*dispatch book*), kuthibitisha kuwa Bw. Ali Muradi alipokea barua hiyo, ambaye hata hivyo anakanusha na kudai kuwa saini iliyowekwa si yake. Barua hiyo iliwasilishwa mbele ya kamati na hivyo inafanya sehemu ya ripoti hii kama Kiambatanisho nam. KTA5

Aidha, Bw. Ali Muradi aliijibu barua hiyo siku hiyo ya tarehe 21/03/2012 kupitia kwa wakili wake, na kudai kuwa hakuwahi kufikishiwa barua ya kusitisha umiliki wa eneo hilo wala ya notisi ya kukusudia kusitisha umiliki huo na kudai katika barua hiyo, kuwa notisi ya kumtaka ajieleze ni kwa nini

asifutiwe umiliki wa eneo hilo, ilitumwa kwa tarehe ya mbele baada ya hati ya eneo hilo kuwa imeshafutwa, jambo ambalo lilionyesha kasoro. Barua hiyo pia iliwasilishwa mbele ya kamati na hivyo inafanywa kuwa sehemu ya ripoti hii kama Kiambatanisho nam. KTA 6.

Awali, Bw. Ali Muradi alieleza kuwa aliwahi kuitwa mbele ya Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Makatibu Wakuu wa wizara hizo, ili kuelezwa kuwa serikali ilifanya makosa kumpa eneo ambalo tayari lilikuwa likimilikiwa na mtu mwengine na kuomba asaidie ili kupatikana kwa ufumbuzi.

Bw. Ali Muradi aliieleza kamati kuwa alitoa masharti kuwa, ili aweze kusaidia, athibitishiwe kuwa eneo hilo kweli alishapewa mtu mwengine kabla yake, pamoja kumpatia eneo mbadala linalofanana na eneo alilonalo masharti ambayo anadai hayajatekelezwa.

Kwa upande wake, Wizara ya Ardhi iliieleza Kamati kuwa eneo hilo lenye mgogoro liliombwa na mwekezaji mzalendo aliyekuwa na azma ya kuweka kiwanda cha uzalishaji wa maziwa cha *Zanzibar Dairy Products.*

Mhe. Mwenyekiti, wizara ilieleza kuwa hati ya eneo hilo aliyopewa Bw. Ali Muradi ilifutwa, ili eneo hilo akabidhiwe mwekezaji wa *Zanzibar Dairy Products* na Bw. Ali Muradi kupewa eneo jengine mbadala.

Wizara iliwasilisha barua inayoonyesha kufutwa kwa hati hiyo, iliyosainiwa terehe 29/02/2012 na Mhe. Ali Juma Shamhuna akiwa Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, ambayo ilieleza sababu za kufutwa, ni kuwa Bw. Ali Muradi kushindwa kuliendeleza eneo alilopewa toka mwaka 2003, barua hiyo inaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho nam. KTA 7

Hata hivyo, Wizara iliwasilisha kielelezo chengine cha kufutwa kwa hati ya Bw. Ali Muradi, mbele ya kamati ambayo ni barua iliyosainiwa na Mhe. Ramadhan Abdalla Shabaan tarehe 6/08/2012, ikieleza sababu za kufutwa kwa hati ya kiwanja hicho, kuwa ni kuwapo kwa hati nyengine namba 195/95 ya tarehe 29/6/1995 kwa eneo hilo, iliyotolewa kabla ya eneo hilo kupewa Bw. Ali Muradi. Barua hiyo ya pili ya kufuta hati ya Bw. Ali Muradi inaambatanishwa na ripoti hii kama kiambatanisho namba KTA 8.

Baada ya kupata barua hiyo ya pili ya kufuta hati ya Bw.Ali Muradi, kamati iliiandikia barua Wizara ya Ardhi ya tarehe 12/11/2013, ya kuitaka wizara iipatie kamati hati hiyo namba 195/95, ambayo hata hivyo wizara ilishindwa kuwasilisha nakala hiyo ya hati.

Barua hiyo ya kamati kuhusu maombi ya kupatiwa hati hiyo kwa wizara, inaambatanishwa na ripoti hii kama kiambatanisho namba KTA 9.

Mnaona mambo hayo.

MAONI YA KAMATI

Katika eneo hilo hilo moja alilopatiwa Bw. Ali Muradi, inaonekana Mawaziri wawili wa Wizara inayoshughulika na Ardhi kwa wakati tofauti walitoa barua ya kufuta hati ya muda ya matumizi ya ardhi.

Katika barua ya awali ya ufutaji wa kiwanja hicho ya tarehe 29/02/2012 iliyosainiwa na Mhe. Ali Juma Shamuhuna, ambaye alikuwa Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa wakati huo, maelezo ya sababu ya kufutwa kwa kiwanja hicho ni kutokana na Bw.Ali Muradi kushindwa kuliendeleza eneo hilo.

Hata hivyo, hati hiyo ya muda ya Bw. Ali Muradi ilifutwa tena tarehe 06/08/2012 kwa barua iliyosainiwa na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa maelezo kuwa eneo hilo tayari lilishawahi kutolewa hati kwa mtu mwengine na kwamba wakati Bw. Ali Muradi anapatiwa eneo hilo, hati hiyo ya mwanzo yenye namba 195/95 ilikuwa haijafutwa.

Kamati iliomba kupatiwa hati hiyo iliyotolewa mwanzo kwa maandishi na hadi wakati wa kuwasilisha ripoti hii, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati imeshindwa kuwasilisha nakala ya hati hiyo.

Hata hivyo maelezo hayo yanapingana na kauli aliyoitoa Mkurugenzi wa Idara ya Ardhi wakati wa ziara katika eneo la tukio na pia maelezo ya Wizara ya maandishi; kwamba sababu ya kumuondoa Bw. Ali Muradi ni kufuatia muwekezaji wa *Zanzibar Dairy Products*, kuhitaji kuongeza eneo kwa shughuli za kiwanda. Aidha kwa mujibu wa *hansard* ya Baraza ya tarehe 13 Julai, 2012, Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati alilieleza Baraza kuwa mgogoro wa eneo hilo umemalizika kwa kampuni ya *Zanzibar Dairy Products* na Bw. Ali Muradi kila mmoja kupatiwa eneo. Utaratibu huu si wa kawaida kwa anayefutiwa hati kupatiwa eneo jengine.

Aidha Wizara ya Ardhi katika taarifa yake kwa Kamati ilieleza kuwa eneo hilo lilifutwa kutokana na eneo hilo kuwahi kupewa mtu mwingine na hivyo kuamua kufuta hati ya Bw. Ali Muradi kwa msingi huo.

Kamati iliitaka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuwasilisha mbele ya Kamati hati ya matumizi ya ardhi iliyotolewa awali kwa ajili ya kiwanja hicho kwa kuiandikia barua mara kadhaa, lakini hata hivyo Wizara ilishindwa kuwasilisha nakala ya hati hiyo hadi wakati wa kuwasilisha ripoti hii.

Kamati pia iliarifiwa kuwepo kwa Kamati ya Mawaziri wawili ambao ni Waziri anayeshughulikia Fedha na yule anayeshughulikia ardhi ambayo inajaribu kusuluhisha tatizo la eneo hilo la Maruhubi. Kamati hii inaamini utaratibu huu pia si wa kawaida na hauzingatii matakwa ya sheria ya ardhi.

Kwa kuwa katika suala hili sababu za kufuta hati ya muda ya matumizi ya ardhi zinatofautiana na kwamba Bw. Ali Muradi alifutiwa hati hiyo kabla ya kupatiwa notisi, ambapo alipatiwa notisi hiyo baada ya kufutiwa hati hiyo badala ya kupewa notisi hiyo kabla ya kufutiwa hati hiyo. Kamati inaamini kuwa taratibu za kufuta hati hiyo hazikufuatwa kwa ukamilifu na hivyo kamati inapendekeza kuwa ufutaji wa hati ya matumizi ya kiwanja hicho ubatilishwe.

Kadhia ya *Leisure Corp (Al-Nakheel)*

Namna ilivyoshughulikiwa

Katika kuishughulikia kadhia hii, Kamati ilimualika Mjumbe aliyeiwasilisha katika kikao cha Baraza Mhe. Hamza Hassan Juma ili kupata maelezo zaidi na vielelezo kuhusiana na hoja hiyo. Mjumbe aliieleza Kamati kuwa Kampuni ya *Al Nakheel* ilikodishwa eneo huko Matemwe kwa ajili ya uwekezaji wa hoteli na kampuni hiyo ilifutiwa eneo hilo kwa kushindwa kuliendeleza kwa mujibu wa sheria ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 1992.

Hata hivyo Mjumbe aliieleza Kamati kuwa wizara katika ufutaji wa hati ya ukodishaji wa eneo hilo, haikuzingatia masharti ya kifungu cha 48 cha Sheria ya Matumizi ya Ardhi ambacho kinaelekeza kutolewa kwa notisi ya miezi mitatu kwa aliyekodishwa ardhi kabla ya kumfutia hati hiyo. Ili kujiridhisha katika madai hayo kamati iliomba Wizara ya Ardhi, kuipatia nakala ya barua ya notisi kwa kampuni hiyo.

Mjumbe aliwasilisha nakala ya barua za malalamiko ya ufutwaji huo, kutoka kwa mwekezaji huyo kwenda kwa Waziri wa Ardhi na Mamlaka ya Uendelezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA). Nakala za barua hizo zinaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho nam KTA 10.

Wizara ya Ardhi iliieleza Kamati kupitia ripoti yake kwa kamati katika ukurasa wa 10, kuwa mwekezaji huyo alifutiwa hati ya ukodishaji ardhi

tarehe 14 Machi, 2011 baada ya kushindwa kuliendeleza eneo hilo toka mwaka 2007 alipopatiwa. Nakala ya ripoti hiyo inaambatanishwa pamoja na ripoti hii na kuwa kiambatanisho namba KTA 11.

Wizara iliendelea kueleza kuwa baada ya kufutiwa mkataba wa ukodishwaji kwa kampuni ya *Leisure Corp. LLC* eneo hilo lilikodishwa kwa kampuni ya *Penny Royal (Gilbraltar), AEACUS Ltd na Horizon Resort Ltd,* pamoja na kutoa hati ya matumizi ya ardhi kwa ndugu Saleh Mohamed Said na ndugu Elizabeth Mayala. Wizara iliwasilisha nakala ya barua ya ufutaji wa hati ya kukodishwa ardhi kwa kampuni hiyo na pia kwa makampuni ya *Supercab Hotel Development, Penny Royal Limited, Aeacus limited, Horizon Resorts Limited,* Ndg. Saleh Mohammed Said na Ndg. Elizabeth Lazaro Mayala.

Wizara ilieleza kuwa makampuni hayo matatu yalifutiwa mikataba ya ukodishwaji kutokana na miradi yao kutopitia na kuidhinishwa na *ZIPA.* Aidha hati za matumizi ya ardhi kwa ndugu Elizabeth Mayala na ndugu Saleh Mohamed Said, zilielezwa kufutwa kutokana na kutolewa katika maeneo ya uwekezaji.

Barua za kufuta mikataba ya ukodishaji ardhi ya Kampuni za *Supercab Hotel Development, Leisure Corp. LLC (Al Nakheel)* na kampuni tatu zilizopewa badala yake pamoja na hati za matumizi za ndugu Elizabeth Mayala na ndugu Saleh Mohamed Said zinaambatanishwa na ripoti hii kama kiambatanisho namba KTA 12.

Hata hivyo katika barua hizo za ufutaji wa mikataba hiyo, Kamati imebaini kasoro iliyokuwepo ambapo Kampuni ya *Leisure Corp* ilifutiwa mkataba siku moja na Kampuni hizo tatu zilizodaiwa kupewa eneo hilo baada ya Kampuni ya *Leisure Corp* kufutiwa. Hii inaonesha kuwa kampuni hizo tatu zilipewa eneo hilo wakati Kampuni ya *Leisure Corp* ikiwa haijafutiwa mkataba wa ukodishwaji.

MAONI YA KAMATI

Katika kadhia hii, pamoja na kamati kuhitaji kupatiwa nakala ya notisi kabla ya kufuta mkataba wa ukodishwaji wa ardhi kwa kampuni ya *Leisure Corp. (Al Nakheel)* kwa mujibu wa kifungu cha 48 cha Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 1992, Wizara ilishindwa kuipatia Kamati kielelezo hicho.

Hivyo, Kamati inapendekeza kuwa masharti ya Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 1992 chini ya kifungu cha 48 yazingatiwe. Kifungu hicho kinapiga marufuku kufuta mkataba wa ukodishaji isipokuwa kwa masharti yaliyotajwa

katika kifungu hicho ambayo yanajumuisha utoaji wa notisi ya miezi mitatu ili kumpa nafasi aliyepewa mkataba huo kurekebisha kasoro iliyojitokeza.

Aidha baada ya Kampuni hiyo ya *Leisure Corp* kufutiwa mkataba wa ukodishwaji wa ardhi, eneo hilo liligawanywa katika maeneo matano, ambapo makampuni mengine matatu yalipatiwa mikataba ya ukodishwaji kwa eneo hilo na watu wawili walipatiwa hati za matumizi ya ardhi.

Hata hivyo, Wizara ilikiri kuwa makampuni hayo yalifutiwa kutokana na miradi yao kutopitia na kuridhiwa na Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (*ZIPA*) kwa mujibu wa kifungu cha 46(3) cha Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 1992.

Kifungu hicho kinampa mamlaka Waziri anayeshughulikia ardhi kukodisha ardhi baada ya mradi kuridhiwa *na ZIPA.* Aidha Wizara ilifuta hati hizo za matumizi ya ardhi katika eneo hilo kutokana na eneo hilo kutengwa kwa ajili ya uwekezaji na hivyo kustahili kutolewa kwa kupitia mikataba ya ukodishwaji na si hati ya matumizi ya ardhi. Hivyo Kamati inapendekeza kufuatwa kwa masharti ya sheria katika utoaji wa mikataba ya ukodishwaji wa ardhi.

Kadhia ya *Sovereign Sands Resort*

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati.

Kadhia hii pia ilielezwa katika kikao cha Baraza na Mjumbe wa Baraza Mhe. Hamza Hassan Juma. Kamati ilipata fursa ya kuzungumza na Mjumbe ambaye aliieleza Kamati kuwa Kampuni ya *Sovereign* ambayo kiwango chake cha malipo kwa mwaka ni dola za Kimarekani 13,365 ilifutiwa hati ya ukodishaji wa eneo hilo na badala yake kupatiwa Kampuni ya *The Address* ambayo ilitakiwa kulipa Dola za Kimarekani 3,000.

Mjumbe aliwasilisha nakala ya bili ya malipo ya Kampuni ya *Sovereign* kwa mwaka 2011 ambayo ni US $ 13,365 pamoja na nakala ya hati ya kukodishwa kwa kampuni ya *The Address* katika eneo hilo hilo baada ya kufutiwa hati ya ukodishaji kampuni ya *Sovereign Sands* ambapo kampuni hiyo ya *The Address* inapaswa kulipa US $ 3,000. Nakala ya bili ya malipo ya kampuni hiyo inaambatanishwa kama Kiambatanisho Nam KTA 14.

Wizara ya Ardhi iliieleza Kamati kuwa kampuni ya *Sovereign Sands* ilifutiwa hati ya kukodisha eneo hilo kwa kutoliendeleza kwa kipindi cha zaidi ya miaka minne toka ilipokodishwa mwaka 2006.

Wizara iliwasilisha nakala za hati ya kukodishwa eneo kwa Kampuni ya *Sovereign Sands* iliyotolewa tarehe 07 Novemba, 2006, barua ya notisi ya miezi mitatu ya kufuta eneo hilo iliyotolewa tarehe 31/10/2011 na nakala ya kufuta hati ya ukodishaji wa eneo hilo kwa kampuni ya *Sovereign Sands* iliyotolewa tarehe 01/02/2012. Nakala hizo zinaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho nam KTA 15. Kamati pia ilipokea nakala ya mkataba wa ukodishwaji wa ardhi kwa kampuni ya *The Address* iliyotolewa tarehe 28/02/2012. Hati hiyo inaambatanishwa na ripoti hii kama kiambatanisho namba KTA 16.

Hata hivyo, kamati iliiandikia Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar ili kuthibitisha usajili wa Kampuni hiyo ya *The Address,* Ofisi hiyo iliipatia kamati nakala ya hati ya usajili wa kampuni hiyo ambayo inaonesha kuwa ilisajiliwa tarehe 11 Aprili, 2012. Nakala ya hati ya usajili inaambatanishwa pamoja na ripoti hii kama kiambatanisho namba KTA 17.

MAONI YA KAMATI

Katika kadhia hii kamati ilipatiwa nakala ya notisi ya miezi mitatu kwa mujibu wa sheria kwa kampuni ya *Sovereign Sands Resort* kabla ya kampuni hiyo kufutiwa mkataba wa ukodishwaji wa ardhi.

Notisi hiyo inaonesha kuwa ilitolewa tarehe 31/10/2011 ambapo kampuni hiyo ilifutiwa rasmi mkataba huo tarehe 1/2/2012. Hivyo, kwa mujibu wa vielelezo hivyo, Kamati imebaini kuwa utaratibu huu wa kisheria wa kutoa notisi kabla ya kufuta mkataba wa ukodishwaji wa ardhi ulizingatiwa.

Kamati imebaini kuwa kwa mujibu wa mkataba, kampuni hii ya *Sovereign Sands Resort* ilikodishwa eneo hilo tarehe 7/11/2006 na hivyo kutakiwa kwa mujibu wa sheria ya matumizi ya ardhi kuliendeleza eneo hilo ndani ya miezi 30 iliyomalizika mwezi Mei, 2009.

Hata hivyo, Kamati ilipata nakala ya risiti ya malipo ya kodi ambayo Kampuni hiyo imelipa kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar, kodi ambayo ililipwa mwezi Novemba, 2010 na ilikuwa inamalizika mwezi Juni, 2011, kipindi ambacho mwekezaji alishapindukia muda uliotajwa kwa mujibu wa sheria wa kuendeleza eneo hilo.

Kamati inapendekeza kuwa kuwepo na uratibu mzuri baina ya taasisi za Serikali ili inapotekezea ukiukwaji wa masharti ya Sheria kwa upande wa mwekezaji, taasisi inayohusika na ukusanyaji wa mapato isikusanye kodi hiyo kutoka kwa kampuni ambayo imekiuka utaratibu uliowekwa na sheria, na

hatua za kutoa notisi zichukuliwe haraka na hatimaye kufanya maamuzi ya kufuta endapo kasoro iliyojitokeza haikurekebishwa.

Kutokana na uthibitisho kutoka Ofisi ya Wakala wa Usajili na Mali, Kamati imebaini kuwa ukodishwaji wa ardhi kwa Kampuni ya *The Address* haukuwa sahihi kutokana na kampuni hiyo kukodishwa ardhi siku 42 kabla ya kuwepo kwake kisheria kwa maana kupata usajili.

Kamati imebaini kuwepo kwa kasoro katika ukodishwaji wa eneo hilo na inapendekeza kuwa ukodishwaji wa eneo hilo uzingatie masharti ya sheria kama yalivyoelezwa katika Sheria ya Matumizi ya Ardhi na Sheria ya *ZIPA.*

Kadhia ya *SAGO*

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati.

Katika kadhia hii, kamati ilibaini kuwepo kwa maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kama yalivyoainishwa katika *hansard* ya tarehe 13 Julai, 2012, ukurasa wa 75 kuwa suala linalohusu kadhia hii, Kampuni ya *SAGO PALM*, imefungua kesi katika mahakama ya Ardhi dhidi ya Kampuni ya *Coconut Resorts* & *Villa*.

Hivyo kamati iliandikia Mahakama ya Ardhi ili kuthibitisha kuwepo kwa kesi hiyo katika mahakama hiyo. Mahakama hiyo ilijibu barua ya kamati na kuijulisha kuwa kesi hiyo ilifunguliwa katika mahakama hiyo na baadae kufunguliwa shauri hilo katika Mahakama Kuu ya Zanzibar baada ya kuunganishwa katika kesi hiyo Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, na Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Barua hiyo kutoka mahakama ya Ardhi inaambatanishwa na ripoti hii kama kiambatanisho namba KTA 18.

Kamati ililazimika kusita katika kuishughulikia kadhia hii kutokana na masharti ya kanuni ya 108 (17) ya kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2012, kuamuru kamati kutoshughulikia jambo lolote linalosubiri uamuzi wa mahakama.

MAONI YA KAMATI

Kamati ilisita kuchunguza kadhia hii baada ya kugundua kuwepo kwa shauri mahakamani.

Kadhia ya Nyumba za Mazizini.

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati.

Kadhia hii ipo katika nyumba iliyopo katika kiwanja walichopewa Ubalozi wa Oman hapo Mazizini. Kamati ilimualika Mjumbe wa Baraza aliyetoa hoja ndani ya kikao cha Baraza Mhe. Mohammedraza Hassanali, ambaye aliieleza Kamati kuwa ubalozi wa Oman ulipatiwa eneo lililopo katika nyumba hizo za Mazizini lakini ubalozi huo umeshindwa kulitumia eneo hilo kutokana na kuwepo kwa wapangaji jambo ambalo halileti picha nzuri kwa serikali.

Kadhia hii ilianza mwaka 2009 baada ya serikali kukodisha eneo hilo kwa ubalozi wa Oman. Nakala ya barua ya makubaliano ya ukodishaji eneo hilo inaambatanishwa na ripoti hii kuwa kiambatanisho namba KTA 19.

Kamati ilitembelea eneo hilo na wapangaji hao wa familia mbili za Bi. Fatma Salum Nassor na Bw. Makame A. Muhajir walieleza kamati kuwa wapo tayari kuhama nyumba hiyo iwapo watapatiwa makaazi mbadala.Wizara ilieleza kuwa imeanza na inaendelea kuchukua hatua ili kuwahamisha wapangaji hao.

Wakati Kamati ikiendelea kuifanyiakazi kadhia hii, Wizara kupitia Idara ya Nyumba iliieleza Kamati kuwa iliwapa notisi ya kuhama wapangaji wa familia mbili katika nyumba hiyo kwa barua ya tarehe 6/3/2012 kwa Bi. Fatma Salum Nassor ambaye alijibu kwa barua ya tarehe 22/3/2012 akiomba kupatiwa makaazi mbadala na familia yake.

Wizara iliandika barua nyengine ya msisitizo wa kuwataka wapangaji hao wahame ya tarehe 27/3/2012. Barua hizo zinaambatanishwa pamoja na ripoti hii kama kiambatanisho namba 20. Hata hivyo, Wizara ilifanya jitihada ya kuwapatia wapangaji wote wawili makaazi mbadala katika *Block* nambari 10, Michenzani ambapo:-

i. Mpangaji wa kwanza Bi. Fatma Salum Nassor alipewa nyumba nambari 10/23, Michenzani, nakala ya barua ya tarehe 21/12/2012.

ii. Mpangaji wa pili, Bw. Muhajir, amepewa nyumba nambari 10/22, Michenzani kwa barua ya tarehe 08/01/2013. Barua hizo zinaambatanishwa na ripoti hii kama kiambatanisho namba KTA 21.

Aidha kamati iliarifiwa kwa barua ya tarehe 26/2/2013, kutoka Idara ya nyumba kuwa tayari Ubalozi wa Oman umeshakabidhiwa nyumba hiyo baada

ya kuwatoa wapangaji waliokuwamo. Idara hiyo iliwasilisha nakala ya barua hiyo kwa kamati na inaambatanishwa na ripoti hii kama kiambatanisho namba KTA 22.

MAONI YA KAMATI

Muda mrefu umepita tangu serikali ifanye uamuzi wa kuupatia ubalozi wa Oman kiwanja kwa ajili ya kujenga ubalozi wake. Suala hili limeanza mnamo tarehe 6 Mei 2009 wakati mkataba wa ukodishwaji wa eneo hilo ulipofungwa baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Ubalozi wa Oman hapa Zanzibar.

Kwa kipindi chote hicho, tokea mwaka 2009 hadi kufikia mwaka 2013 Wizara imeshindwa kusimamia uamuzi huo wa kulikabidhi eneo hilo kwa ubalozi wa Oman kwa kushindwa kuwahamisha wapangaji waliomo katika nyumba No.12, iliyopo katika kiwanja hicho. Kamati ilihoji sababu za kutotekelezwa kwa maamuzi hayo ambapo sababu kubwa iliyoelezwa ni kwa wapangaji wa nyumba hiyo kutokuwa na makazi mbadala.

Kutokana na maelezo hayo, Kamati ilihoji kwa nini Wizara haikuchukua jitihada za kuwapatia maeneo mengine ya kuwakodisha wapangaji hao kama vile nyumba za maendeleo za Michenzani ili kuweza kutekeleza maamuzi yaliyopitishwa ya kuukodisha eneo hilo Ubalozi wa Oman. Kutokana na msukumo huo wa Kamati, Wizara iliweza kuwahamisha Wapangaji hao, hapa tunataka tuwapongeze Katibu Mkuu na wenzake kwa kuchukua juhudi kubwa kulitatua jambo hili wakati Katibu Mkuu aliyepita alishindwa, na kuwapatia makaazi wapangaji hao katika nyumba hizo za Michenzani na kulikabidhi rasmi eneo hilo kwa Ubalozi wa Oman.

Kadhia ya Kisiwa cha Kwale

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati.

Katika kuishughulikia hoja hii, Kamati iliwaalika watendaji wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambao waliieleza Kamati kuwa Kisiwa cha Kwale ni miongoni mwa maeneo yaliyopo chini ya hifadhi ya Ghuba ya Menai. Eneo la kisiwa hiki lilikodishwa baada ya mashauriano mbalimbali kufanyika baina ya taasisi za serikali na kampuni ya *The Rihla* kwa hati ya ukodishwaji inayoonesha kuwa kampuni hiyo imekodishwa eneo hilo kwa muda wa miaka 33.

Hati ya ukodishwaji eneo hilo inaambatanishwa na ripoti hii kama kiambatanisho namba KTA 23. Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliipatia kamati vielelezo vinavyoonesha mawasilianao ya kitaasisi na vielelezo hivyo

vinaambatanishwa na ripoti hii kama kiambatanisho KTA 24. Vielelezo vya mradi huo vinaambatanishwa pamoja na ripoti hii kama kiambatanisho namba KTA 25.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatarajia kuingia katika Makubaliano na Kampuni ya *The Rihla (Memorandum of Understanding)* baada ya kukamilika kwa utafiti wa kimazingira *(Environment Impact Assessment)* ambao hivi sasa upo katika ngazi ya Idara ya Mazingira.

MAONI YA KAMATI

Kamati inapendekeza kuwa taasisi zinazohusika katika suala hili ziharakishe katika kuchukua hatua ili kulimaliza suala hili kwa manufaa ya nchi.

Kadhia ya *Sunset Paradise Resort*

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati.

Kamati ilimualika Mjumbe aliyetoa hoja hii katika mkutano wa Bajeti wa Baraza wa mwaka 2012/2013 Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, ambaye aliieleza Kamati kuwa Kampuni ya *Sunset Paradise* ilikodishwa ardhi eneo la Kama kwa hati ya ukodishwaji ambayo inaambatanishwa na ripoti hii kama kiambatanisho namba KTA 26. Kwa mujibu wa mkataba huu Kampuni hiyo inalipa kodi ya dola za Kimarekani 39,000 na Mheshimiwa aliwasilisha nakala ya bili ya kodi ya ardhi inayoonesha kiasi hicho ambayo inaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho nam. KTA 27.

Aidha Mjumbe huyo aliwasilisha nakala ya kibali cha ujenzi kwa Kampuni hiyo kilichotolewa tarehe 21/12/2010 ambayo inaambatanishwa na Ripoti hii kama Kiambatanisho nam. KTA 28. Mjumbe aliieleza Kamati kuwa tarehe 7 Machi, 2011, Kampuni hiyo ilifutiwa hati ya ukodishaji ardhi bila ya kupewa notisi kwa Kampuni hiyo kama Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya Mwaka 1992 inavyoelekeza.

Mjumbe pia aliieleza Kamati kuwa baada ya kufutwa kwa hati ya ukodishaji kwa Kampuni ya *Sunset*, eneo hilo lilikodishwa kwa Kampuni ya *Sea Rock Resort Ltd* kwa kodi ya Dola za Kimarekani 2,500.

Wizara iliieleza Kamati kuwa Kampuni ya *Sunset* ilifutiwa hati ya ukodishaji ardhi kutokana na kushindwa kuliendeleza eneo hilo ndani ya kipindi cha zaidi ya miaka mitatu. Aidha Wizara iliwasilisha nakala ya barua ya ufutaji huo na mikataba ya ukodishwaji mbele ya kamati na nakala hizo zinaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho namb. KTA 29.

MAONI YA KAMATI

Kamati ilihitaji kupatiwa notisi kabla ya kufutiwa kwa mkataba wa ukodishwaji wa ardhi kwa kampuni ya *Sunset Paradise,* lakini Wizara inayoshughulikia ardhi ilishindwa kuipatia Kamati nakala ya notisi hiyo hadi wakati wa kuwasilisha ripoti hii. Utaratibu huu wa kutoa notisi ni kwa mujibu wa matakwa ya kifungu cha 48(3) ambacho kinataka kabla ya Waziri kufuta hati ya ukodishwaji wa ardhi, mwenye hati hiyo apatiwe notisi ya miezi mitatu ya kurekebisha jambo ambalo litapelekea kufutiwa kwake mkataba wa ukodishwaji wa ardhi.

Kamati inashauri kuwa kwa vile utaratibu wa kufuta hati ya matumizi ya ardhi ni wa kisheria, basi ufutaji huo wa mkataba wa ukodishaji wa eneo hilo ufuate masharti ya Sheria. Aidha Kamati imebaini kuwa hakuna "*formula"* maalum ya malipo ya kodi ya ardhi kwa wawekezaji kinyume na inavyodaiwa na Wizara inayoshughulika na ardhi.

Katika taarifa yake kwa Kamati, Wizara hiyo inadai kuwa mwekezaji Mzalendo kikawaida hupaswa kulipa Dola za Kimarekani 500 kwa hekta moja kwa mwaka. Kwa mfano katika kadhia hii, na nyengine katika ripoti hii, inaonesha kinyume chake. Kampuni ya *Sea Rock Ltd* iliyopewa eneo walilofutiwa *Sun Set Paradise,* wanalipa dola za Kimarekani 3000 kwa hekta 8.20, wakati kwa kiwango kilichotajwa na Wizara, wangetakiwa kulipa kiasi cha dola 4100.

Zipo pia kampuni ambazo zimekodishwa kwa viwango tofauti licha ya kuwepo maeneo yenye ukubwa unaofanana, mfano hekta 2.57 zimekodishwa kwa dola za kimarekani 3000 na nyengine hekta hizo hizo kwa dola 5000.Kamati inapendekeza kuwepo kwa mpango maalumu wa kuwekwa viwango vya kodi vya ardhi kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana na mambo ya Fedha, vitakavyowekwa kwa uwazi ili vifahamike kwa urahisi na mwekezaji au mwanachi yeyote.

1. Kadhia ya Bruno Conte

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati

Kamati ilipata maelezo kutoka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuwa Mnamo tarehe 04/08/2000 Bw. Bruno Conte alikodishwa eneo la ardhi lililopo Uroa kwa muda wa miaka 33 kwa hati yenye nambari ya usajili *DP* 431/2000 ambayo inatolewa kama sehemu ya ripoti hii, Kiambatanisho nam. KTA 30.

Eneo hilo lenye ukubwa wa Hekta 0.39 lilikodishwa kwa madhumuni ya ujenzi wa ofisi na makaazi kwa kodi ya ardhi ya Dola za Kimarekani mia saba na thamanini (*USD* 780).

Mbali na maelezo hayo, Kamati ilipatiwa maelezo ya upande wa pili wa kadhia hii kupitia kwa *congress* Mheshimiwa Hamza Hassan Juma Mwenyekiti wa Wenyeviti. Mheshimiwa Hamza aliikabidhi Kamati vielelezo mbali mbali vya Bw. Bruno Conte ikiwemo barua ya malalamiko kupitia Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar kwenda kwa Makamu wa Pili wa Rais.

Katika barua hiyo ya tarehe 16/08/2011 ambayo kamati inaitumia kuwa sehemu ya ripoti yake na kuwa Kiambatanisho nam. KTA 31, Bw. Bruno Conte anaeleza kadhia nzima ya kufutiwa eneo hilo.

Bw.Bruno ameeleza kuwa taratibu zote za kufuta mkataba zimefanywa siri, kinyume na sheria wala yeye hakujulishwa. Kwa maelezo ya barua hiyo, Wizara ikubali kuwa mkataba wa ukodishwaji ulifutwa tarehe 13/06/2011, kamati imepata barua ya tarehe 6/06/2011 iliyofuta mkataba wa ukodishwaji wa eneo hilo ambayo imetolewa na aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Mheshimiwa Ali Juma Shamuhuna, (Kiambatanisho nam. KTA 32).

Kwa mujibu wa maelezo ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, eneo hilo alilofutiwa Bw. Bruno, amepewa Bw. Said Ali Juma Shamuhuna. (Tafadhali rejea kiambatanisho namba 11 katika ukurasa wa 16)

Bw. Bruno Conte katika barua yake kwa Makamu wa Pili wa Rais, kupitia kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar anaeleza kwamba, mnamo tarehe 13/06/2011 watu wasiojulikana walivamia eneo hilo na kuanza kuvunja ukuta wa fensi, ghala pamoja na vitu kadhaa ambavyo mpaka leo havijulikani vilipo.

Aidha ilielezwa kuwa, wakati hayo yote yanafanyika siyo Bw. Bruno Conte wala Mwakilishi wake Bw. Mzee Mwinyi (kwa hati ya uwakala inayoambatanishwa KTA 33) waliopewa taarifa (notisi) ya hatua yoyote inayoendelea. Hivyo, si Sheha wala Ofisi ya Halmashauri iliyokuwa na taarifa ya uvunjwaji na ujenzi mpya uliokuwa unaendelea.

Kutokana vielelezo vya Bw. Bruno Conte, wakati Wizara ikidai kumfutia Mkataba wa ardhi wa eneo lake kwa madai ya kutoliendeleza na kulitelekeza eneo hilo, Bw. Bruno Conte ameonesha kuwa ameliendeleza eneo hilo isipokuwa alivunjiwa majengo aliyoyaendeleza. Aidha kamati ilipatiwa kielelezo kinachoonesha kuwa Bw. Bruno Conte alikuwa akilipa kodi ya ardhi

serikalini na kielelezo hicho kinaambatanishwa kama kiambatanisho namba KTA 34.

MAONI YA KAMATI

Katika kadhia hii, Kamati ilitaka kupatiwa vielelezo kadhaa ikiwemo nakala ya notisi ya kufuta mkataba wa ukodishwaji kutoka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati lakini hata hivyo hadi wakati wa kuwasilisha ripoti hii, Wizara ilishindwa kuipatia Kamati kielelezo hicho.

Aidha Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati iliieleza Kamati kuwa eneo hilo baada ya kufutiwa mkataba wa ukodishwaji Kampuni ya Bruno Conte, alipatiwa Ndg. Said Ali Juma Shamuhuna kwa hati ya matumizi ya Ardhi.

Kamati iliagiza kupatiwa vielelezo vyenye kuonesha uhalali wa matumizi na ukweli wa jambo hilo na haki ya matumizi ya ardhi kwa Ndg. Said Ali Juma Shamuhuna pamoja na nyaraka nyengine zilizotumika katika hatua za uombaji na hadi kupewa eneo hilo Ndg. Said Ali Juma Shamuhuna. Hata hivyo pamoja na jitihada za Kamati kufuatilia kwa mazungumzo na viongozi wa wizara na hata kwa kuiandikia wizara barua mara kadhaa kuhusu vielelezo hivyo, wizara ilishindwa kuipatia vielelezo na ilishindwa kuthibitisha hilo.

HADIDU REJEA NAM 2

Maeneo ambayo yalikuwa yanatumiwa na wananchi kwa shughuli zao za kuendeleza maisha, lakini yamechukuliwa bila ya kuzingatia maslahi ya wananchi waliokuwa wanayatumia;

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati

Katika Hadidu Rejea hii, Kamati baada ya kupitia taarifa ya *Hansard* wakati wa Mkutano wa Bajeti wa mwaka wa fedha 2012/2013, iliainisha maeneo ya Kijichi, Selem na Dole kuwa ni miongoni mwa maeneo ambayo yalikuwa yanatumiwa na wananchi kuendeleza maisha na kuchukuliwa bila ya kuzingatia maslahi ya waliokuwa wanayatumia.

Wizara imeieleza Kamati kuwa kutokana na kuwepo kwa mgogoro katika maeneo hayo, suala hilo limeundiwa Kamati inayohusisha Makatibu Wakuu watatu kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Wizara ya Kilimo na Maliasili. Kamati hiyo ya Makatibu Wakuu imemaliza kazi yake kwa upande wa Kijichi Nguruweni na kazi ya kugawa ardhi kwa wakulima kwa eneo hilo imefanywa kwa kiasi kikubwa.

Kamati Teule iliomba kupatiwa ripoti inayohusu wakulima wa eneo hilo kupatiwa maeneo hayo pamoja na orodha ya wananchi waliopewa maeneo hayo. Hata hivyo hadi wakati wa kuwasilisha ripoti hii, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ilishindwa kuwasilisha vielelezo hivyo mbele ya Kamati.

MAONI YA KAMATI

Kamati inapendekeza kurahisisha kwa hatua za kutatua mgogoro wa ardhi uliopo katika maeneo hayo na hatimae kuwapatia wananchi wanaostahili haki ya kutumia maeneo hayo.

HADIDU REJEA NAM. 3

Wawekezaji wanaochimba mchanga kwenye maeneo ya fukwe.

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati

Katika kadhia hii, Kamati ilielezwa kuwa msingi wa tatizo hilo ni ujenzi wa jeti unaokusudiwa kufanywa na Hoteli ya Palumbo iliyopo huko Uroa na matumizi ya fukwe kwa wageni wa hoteli hiyo.

Suala hilo ambalo limejadiliwa kwa pamoja baina ya taasisi mbali mbali za serikali zikiwemo Afisi ya Mkuu wa Wilaya, Idara ya Ardhi, Idara ya Mazingira na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na kukubaliana juu ya haja ya kufanya Uchambuzi wa Kimazingira (*EIA*) utakaotoa muelekeo wa kukubaliwa au kukataliwa kwa ujenzi wa jeti baada ya kwanza kufanya utafiti katika jamii inayozunguka kuona namna wanavyopokea suala hilo.

MAONI YA KAMATI

Kamati inakubaliana na uamuzi wa kuwashirikisha wananchi katika kufikia maamuzi juu ya namna ya kulishughulikia suala hilo na hatimaye kufanya Uchambuzi wa athari za kimazingira, na inapendekeza kuwa mambo hayo yaharakishwe ili kuondosha mgogoro huo.

HADIDU REJEA NAM. 4

Mgogoro wa Ardhi baina ya serikali na wananchi (wakulima), Bambi

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati

Kamati Teule ilikutana na watu mbali mbali wanaohusika na hoja hii akiwemo *Congress* Mhe. Hamza Hassan Juma Mwenyekiti wa Wenyeviti, ambaye aliibua hoja hii ndani ya Baraza la Wawakilishi. Kamati pia ilifanya ziara katika bonde la Matora Bambi ambapo iliambatana na Mkuu wa Wilaya ya Kati, Mkurugenzi wa Ardhi na wasaidizi wao.

Kamati ilipata maelezo kutoka kwa wakulima wanaolitumia bonde hilo ambao walieleza kuwa wamekuwa wakilitumia eneo hilo kwa muda mrefu katika shughuli za kilimo na ufugaji na kwamba hawakushirikishwa katika hatua za awali katika maamuzi ya kulitumia eneo hilo kwa shughuli za uwekezaji wa ufugaji wa ng'ombe kwa ajili ya kiwanda cha maziwa kiitwacho *Zanzibar Dairy Products.*

Watendaji wa Wizara ya Ardhi walieleza kuwa walipewa kazi ya kulipima Bonde la Matora na wakulima wa eneo hilo waliwazuia watendaji hao kufanya shughuli hiyo kwa kupinga kuchukuliwa kwa eneo hilo. Baada ya hatua hiyo, Kamati ilielezwa kuwa timu ya mawaziri watatu wa serikali ilifika Bambi ili kuwanasihi wakulima hao kukubali eneo hilo kupewa mwekezaji. Mawaziri hao ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Wakulima hao hawakuridhika hasa kutokana na kulitegemea bonde hilo la Bambi kwa ajili ya shughuli za kujitafutia maisha yao na kwamba kumpatia mwekezaji eneo hilo kungewaathiri kimaisha. Pamoja na mawaziri hao kuwaahidi wakulima kuwa uwekezaji huo ungewapatia ajira wakulima hao, wananchi hawakuridhika kutokana na kutohakikishiwa kama wakulima wote wa bonde hilo wangepatiwa ajira kutoka kwa mwekezaji huyo.

Aidha Kamati ilijulishwa kuwa Serikali katika ngazi ya masheha na Mkuu wa Wilaya hawakushirikishwa katika hatua za awali juu ya kubadili matumizi ya bonde hilo kutoka kwa wananchi na kumpatia mwekezaji kwa ajili ya mradi huo.

MAONI YA KAMATI

Ingawa eneo hilo la bonde la Matora ni la Serikali lakini bado hakukuwa na utaratibu wa uwazi wa kulihamisha matumizi yake kutoka kilimo kwenda kwenye uwekezaji wa mifugo kwa kuipatia Kampuni ya *Zanzibar Diary Products.* Taasisi zinazohusika na uwekezaji hazikushiriki kikamilifu katika kusimamia mradi huu wa uwekezaji, badala yake sehemu kubwa ya uwekezaji huu imeratibiwa na Serikali Kuu.

Pamoja na jitihada za Mawaziri watatu ambao ni Waziri anayeshughulikia masuala ya fedha, Waziri anayeshughulikia masuala ya ardhi na Waziri katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuwashauri wananchi kuhusu mradi huo, jitihada hizo hazikufanikiwa.

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na watu wake walieleza kuwa ushiriki wake katika suala hili kuwa haifahamu kwa kina suala hilo kutokana na kutoshirikishwa kikamilifu.

Kamati inapendekeza kuwa Serikali ichukue hatua za kulimaliza tatizo hilo kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali zikiwemo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kati na *ZIPA* kwa ajili ya manufaa ya nchi na wananchi.

HADIDU REJEA NAM. 5

Mgogoro wa Ardhi baina ya mfanyabiashara na wakulima, Tumbe.

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati

Sehemu ya kwanza ya mgogoro huu inahusu wananchi wa Kijiji cha Kijichame; Tumbe, ambao walikuwa wakilima maeneo ya mashamba ya serikali ambayo serikali imeyapima viwanja bila ya wao kupatiwa viwanja hivyo.

Kamati ilipata maelezo ya Mjumbe wa Baraza aliyeiibua hoja hii ndani ya Baraza, Mheshimiwa Rufai Said Rufai wa Jimbo la Tumbe ambaye aliieleza Kamati kuwa Idara ya Ardhi ilipima eneo lililokuwa likitumiwa na wananchi wa Chwaka; Tumbe linalowahusu wananchi wa Kijichame. Aidha Mjumbe huyo wa Baraza aliendelea kuieleza Kamati kuwa eneo hilo lilipimwa bila ya kuwapa taarifa wananchi waliokuwa wanayatumia maeneo hayo kwa muda mrefu.

Mjumbe huyo pia aliieleza Kamati kuwa mwaka 2010, Kamati ya Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi ilitembelea eneo hilo na kutoa agizo

kuwa wananchi waliokuwa wanalitumia eneo hilo wapatiwe asilimia 70 ya eneo lililopimwa na kueleza kuwa Wizara ilikubali kuwapatia wananchi sehemu ya eneo hilo

Kamati ilipewa orodha ya watu waliopewa maeneo huko ambao ndani yake wamo viongozi wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mikoa miwili ya Pemba, Maafisa Wadhamini, Maafisa Tawala Wilaya na Mikoa Pemba, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu wa Mabaraza ya Mji na Halmashauri Pemba, Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na watu wengine mbali mbali ambao orodha yao inaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho Nam. KTA 34A

Kamati ilielezwa kuwa baada ya wananchi hao kulalamika, Wizara ya Ardhi ilikubali kukaa nao pamoja kuwasikiliza. Aidha Kamati pia ilielezwa kuwa Idara ya Ardhi ilikubaliana na Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi kutenga viwanja kwa ajili ya wananchi wa eneo la Tumbe wakati maeneo hayo yatakapopimwa kwa awamu nyengine.

Kamati ilielezwa kuwa katika kikao hicho, Wizara ya Ardhi iliongozwa na Naibu Waziri wa Wizara hiyo kwa wakati huo Mhe. Tafana. Kutokana na kikao hicho Idara ya Ardhi ilitoa barua ya tarehe 12/05/2010 ambayo iliwahakikishia wananchi hao kutengewa asilimia 70% ya viwanja vitakavyopimwa katika awamu ya pili. Barua hiyo pia iliwahakikishia wanakijiji hao kupata haki ya fidia ya vipando vyao katika viwanja vilivyopimwa awamu ya mwanzo, isipokuwa kwa wale tu waliopatiwa viwanja hivyo.

Aidha katika barua hiyo wananchi hao wamehakikishiwa kupatiwa viwanja hivyo ndani ya siku 60 kuanzia tarehe ya barua hiyo. Nakala ya barua hiyo ambayo Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi ilinakiliwa inaambatanishwa na ripoti hii kama kiambatanisho namba KTA 35.

Viwanja vyote vilivyopimwa katika awamu ya pili ni 109, ambapo viwanja 106 ni vya makaazi. Kamati Teule ilielezwa kuwa, Wanakijiji wa Kijichame walitakiwa kupeleka orodha ya majina ya wanaohitaji kupatiwa viwanja hivyo, orodha ilipelekwa na kuonekana na majina mengi kuliko idadi ya viwanja vilivyopo na Idara iliirudisha orodha hiyo na kutaka orodha sahihi.

Orodha nyengine iliwasilishwa ambayo nayo ilionekana kutokuwa na uhusiano wowote na ile orodha ya awali. Kwa mujibu wa Idara ya Ardhi, hatimaye makubaliano yalifikiwa. Hata hivyo, utaratibu ulihitajika kwa wananchi hao kujaza fomu ya maombi, na vitambulisho vya ukaazi na Tsh.

200,000/= ambapo kwa mujibu wa maelezo ya Wizara wananchi wemeshindwa kukamilisha kwa kushindwa malipo hayo.

Vile vile, wanakijiji hao walilalamika mbele ya Kamati Teule kuwa maeneo wanayokusudiwa kupewa katika awamu ya pili ya viwanja hivyo hayapo katika mazingira mazuri, ni maeneo ya maji maji na ujenzi wake ni mgumu kwa watu wa kipato cha chini.

Kamati ilipatiwa nakala ya hati za matumizi ya ardhi kwa watu mbali mbali ambayo imejumuisha viongozi mbali mbali. Nakala ya hati hizo za matumizi ya ardhi pamoja na barua za kuombwa viwanja hivyo kwa viongozi hao zinaambatanishwa kwa pamoja kama kiambatanisho namba KTA 36.

Kwa kuwa baadhi ya nakala za hati za matumizi ya ardhi ambazo kamati ilipatiwa hazikuwa na saini za waliopewa na baadhi saini za waliopewa kutoonekana vizuri, kamati iliomba kupatiwa uthibitisho kutoka Wizara ya Ardhi, endapo watu waliotajwa walipatiwa hati hizo.

Wizara ilithibitisha kuwa hati hizo zote zilichukuliwa na wahusika waliopewa maeneo hayo na barua hiyo ya uthibitisho inaambatanishwa na ripoti hii kama kiambatanisho namba KTA 37.

Sehemu ya pili ya mgogoro huu, unahusu wananchi wa Tumbe, katika eneo la Mwanasoza kwa Mzigua, ambao wanadai kuwa Idara ya Ardhi, imeyapima maeneo yao bila ya ridhaa yao na kuwapa watu wenye uwezo kujenga.

Wananchi hao wa Tumbe waliieleza Kamati Teule kuwa ardhi hiyo ni yao tokea asili. Mkuu wa Idara ya Upimaji na Ramani, aliieleza Kamati Teule kuwa wakati wakipima eneo hilo hakukuwahi kuwa na malalamiko ya umiliki kwa kuwa shamba la Serikali.

MAONI YA KAMATI

Kamati inashauri Wizara inayohusika na ardhi kutekeleza majukumu yake kwa kuongozwa na sheria na kanuni.

Kamati inashauri kuwa ni vyema Wizara ikakutana na wananchi wa maeneo hayo ya Tumbe na kusikiliza kilio chao na hatimaye kuwapa haki ya kutumia maeneo hayo ambayo wamekuwa wakiyatumia kwa muda mrefu ili waendelee na shughuli zao za kujiletea maendeleo.

Mgogoro wa maeneo ya ardhi ya wananchi yaliyonyang'anywa na kufanywa vitega uchumi, Makangale.

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati

Wakati Kamati Teule inafuatilia hadidu rejea hii iliambatana na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini na watendaji wake, Watendaji wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Mheshimiwa Rufai Said Rufai ambaye ndiye aliyetoa hoja katika Mkutano wa Baraza.

Kamati ilipata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Rufai na wananchi walalamikaji kuwa mgogoro huo umeanza tokea mwaka 2004 baada ya Idara ya Ardhi kulipima eneo hilo, kwa nia ya kupewa mwekezaji, eneo ambalo wananchi hao wanadai kulimiliki wakiwa na nyaraka ya umiliki.

Nakala ya nyaraka hiyo inayodaiwa kuthibitisha haki ya walalamikaji juu ya eneo hilo inaambatanishwa na ripoti hii kama kiambatanisho namba KTA 38. Kamati ilielezwa kuwa wananchi hao walilalamika hatua ya kupimwa eneo hilo na malalamiko yao waliyafikisha kwa Mkuu wa Wilaya ya Micheweni ambaye aliwaahidi kulitafutia suluhu jambo hilo.

Kamati ilielezwa na walalamikaji kuwa Mkuu wa Wilaya ya Micheweni aliwaahidi kuwa watalipwa Tsh. 15 milioni ambazo hawajalipwa mpaka sasa. Wananchi hao wamesisitiza kuwa hawapo tayari kwa hivi sasa kupokea kiasi hicho cha fedha kwa vile thamani yake imepungua tokea 2005 hadi hivi sasa. Walichokuwa wanakitaka sasa ni kurejeshewa eneo lao ili wauze kwa bei muafaka wanayoitaka.

Wizara ya Ardhi ilithibitisha kukodishwa eneo hilo kwa kampuni ya *Mpapindi Holiday and Diving Company* tangu tarehe 24 Machi, 2004 na kuipatia Kamati nakala ya Hati ya Makubaliano ya Ukodishaji wa eneo hilo ambayo inaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho nam. KTA 39. Hata hivyo Wizara ilithibitisha kuwa Kampuni hiyo iliyokodishwa eneo hilo ambayo ilipaswa kulipa dola za Kimarekani 9,230 kwa mwaka, toka mwaka 2007 haijawahi kulipa fedha hizo hadi sasa.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Micheweni aliieleza Kamati kuwa aliwahi kufanya mazungumzo na walalamikaji wa eneo hilo na kukubaliana kuwa walalamikaji hao wamuachie muwekezaji huyo aendelee na shughuli zake kwa ahadi ya walalamikaji hao kupatiwa *TZS* 15,000,000/- ambazo *ZIPA* walielezwa kuwa wangesimamia upatikanaji wa fedha hizo. Mkuu wa Wilaya

aliwasilisha nakala ya barua walizowasiliana na taasisi za serikali katika kadhia hiyo pamoja na kumbukumbu za kikao cha pamoja na walalamikaji ambazo kwa pamoja zinaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho nam. KTA 40.

Aidha kamati ilipata nakala ya barua kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba iliyosainiwa tarehe 7 Machi, 2007 ambayo ilimtaka Afisa Mdhamini wa *ZIPA* huko Pemba kusimamia upatikanaji wa haki za walalamikaji kutoka kwa muwekezaji. Barua hiyo inaambatanishwa na ripoti hii kama kielelezo namba KTA 41.

MAONI YA KAMATI

Kwa mujibu wa kifungu cha 56 cha sheria ya Ardhi, Waziri anaweza kufuta haki ya matumizi ya ardhi. Isipokuwa katika ufutaji huo, atapaswa kuzingatia masharti yafuatayo. Kwanza ni sharti kuwa ufutaji huo uwe kwa maslahi ya umma na pili fidia kwa bei ya soko ilipwe.

Serikali kupitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Micheweni na Mkoa wa Kaskazini Pemba, ilikubali haki ya fidia kwa wananchi wa Makangale waliodai kuwa na haki katika eneo hilo, kutokana na kumbukumbu za kikao baina ya Mkuu wa Wilaya na wananchi hao na pia kutokana na barua ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba aliyomuandikia Afisa Mdhamini wa *ZIPA*, Pemba kumtaka ofisi yake isimamie upatikanaji wa haki za wananchi kutoka kwa mwekezaji.

Kamati inaamini kuwa serikali ilipaswa kulipa fidia kwa walalamikaji kwa wakati kama ambavyo walikubali suala la kuwalipa fidia kwa kumbukumbu zilizotajwa hapo juu kama yalivyo masharti ya sheria.

Kuchelewa kulipa fidia kwa muda mrefu toka mwezi Disemba, 2005 wakati walalamikaji walipokubaliana na serikali ya wilaya, kunapelekea uchocheaji wa migogoro ya ardhi isiyo ya lazima.

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya baada ya kukubaliana na walalamikaji, ilipaswa kusimamia kwa umakini makubaliano hayo kwa kuwasiliana na mamlaka nyingine za serikali ili malipo hayo yafanyike kwa haraka.

Kamati inapendekeza kuwa serikali ilipe fidia kwa walalamikaji hao katika eneo la Makangale ili kumaliza mzozo huo na kwa kuwa kiwango cha shilingi milioni kumi na tano (Tzs 15,000,000/-) kilikubalika mwaka 2005, takriban miaka minane iliyopita, ni vyema serikali ikafanya mapitio ya kiwango hicho

hasa kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 56 cha sheria ya Ardhi kinachoelekeza fidia kulipwa kwa thamani ya soko (*market value*).

Aidha, kamati inapendekeza marekebisho ya sheria ili kuweka muda maalum wa kulipa fidia kwa mwananchi ambaye umiliki wa eneo umefutwa kwa ajili ya maslahi ya umma ili kuepuka athari ya thamani ya fedha kushuka kutokana na muda na hivyo kukaribisha mgogoro.

HADIDU REJEA NAM. 7

Mgogoro wa Ardhi kati ya wananchi na viongozi wa serikali, Mchangamle, Kizimkazi.

Kamati ilifuatilia hadidu rejea hii kwa kufika huko Kizimkazi na kukutana na wananchi wa Mchangamle, Kizimkazi.

Kamati ilipokea taarifa ya wananchi hao ambayo hatimaye ilieleza kuwepo kwa kesi iliyofunguliwa Mahakamani kuhusiana na kadhia ya mgogoro huo baina ya wananchi na Hoteli ya *The Residence*.

Kamati kupitia kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi, iliandika barua kwa Mahakama Kuu ya Zanzibar kutaka ufafanuzi kuhusu uwepo wa kesi hiyo na hatua iliyofikia. Barua hiyo iliandikwa tarehe 12/02/2013.

Kamati Teule haikuweza kuendelea na hadidu rejea ikisubiri majibu kutoka Mahakama Kuu kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2012 chini ya Kanuni ya 108(17), Kamati haipaswi kushughulikia suala linalosubiri maamuzi ya Mahakama.

Mahakama Kuu ilijibu kwa barua ya tarehe 15/07/2013 na kueleza kuwa kesi hiyo ilifunguliwa tarehe 24/11/2011 ambayo hata hivyo ilifutwa tarehe 24/04/2013 kwa maombi ya Mdai. Barua hiyo ya Mahakama inaambatanishwa na Ripoti ya Kamati hii kama Kiambatanisho Nam. KTA 43.

MAONI YA KAMATI

Kamati ilisita kushughulikia hadidu rejea hii kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi Toleo la Mwaka 2012.

HADIDU REJEA NAM. 8

Mgogoro wa Ardhi kati ya wananchi, Vitongoji Makaani.

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati

Kamati ilifuatilia suala hili kwa kutembelea eneo la Vitongoji, Makaani na kukutana na wananchi wa eneo hilo pamoja na masheha wa eneo hilo, Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake, Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mkurugenzi wa Ardhi na Usajili, Afisa Mdhamini wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na watendaji wengine wa wizara hiyo.

Katika kikao hicho Kamati ilielezwa na wananchi wa maeneo hayo kuwa kiini cha mgogoro huo ni maeneo waliyokuwa wakiyatumia kwa shughuli za kilimo kuchukuliwa na kupimwa viwanja na kugaiwa makundi mbali mbali wakiwemo wafanyabiashara, viongozi na watendaji wa serikali na wanasiasa bila ya kuwazingatia wakaazi wa vitongoji ambao walikuwa wakiyatumia maeneo hayo kabla ya ugawaji wa viwanja hivyo.

Aidha, wananchi hao waliieleza Kamati kuwa baadhi ya wananchi waliomba kupimiwa maeneo hayo kwa mujibu wa taratibu za maombi ya viwanja, lakini hawakujibiwa maombi yao na baadhi yao walilipa fedha kwa ajili ya upimaji kupitia kwa sheha wa eneo, ambazo zilielezwa kutofika katika wizara inayohusika na ardhi. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa sheha huyo tayari alishafariki. Kamati ilitaka wizara inayoshughulikia masuala ya ardhi kuwasilisha nakala za hati za matumizi ya ardhi zilizotolewa katika maeneo hayo. Pamoja na vielelezo vyengine vinavyohusika katika zoezi la utoaji wa haki ya matumizi ya ardhi.

Hata hivyo, wizara hiyo iliwasilisha fomu moja tu ya maombi ya haki ya matumizi ya ardhi ya Bw. Seif Suleiman ambayo haikuwa imekamilika kwa kuwa ilijazwa na Sheha pekee na haikuidhinishwa na taasisi za ardhi kama inavyopaswa kufanywa kwa mujibu wa sheria. Fomu hiyo ya maombi inaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho Nam. KTA. 44.

Aidha, katika fomu hiyo, Bw. Seif Suleiman alieleza madhumuni ya kuomba eneo hilo, ni ujenzi wa hoteli ya kitalii. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi wowote wenye kuonyesha kuwa muombaji alipitia taratibu za kisheria za uwekezaji kama sheria ya Matumizi ya Ardhi chini ya kifungu cha 39(7). Pamoja na kasoro hizo, muombaji alipewa haki ya matumizi ya ardhi.

Aidha, eneo hilo la Vitongoji ambalo Wizara ya Ardhi iliithibitishia Kamati kuwa eneo la Vitongoji ni eneo lililopangwa kwa ajili ya uwekezaji. Lakini

hata hivyo, miongoni mwa maeneo yaliyotolewa, maeneo matano yalitolewa kwa ajili ya kilimo. Nakala za hati hizo zilizotolewa katika eneo hilo zinaambatanishwa kwa pamoja kama Kiambatanisho Nam. KTA. 45.

MAONI YA KAMATI

Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 1992 imeeleza kuwa Mzanzibari anaweza kupewa ardhi sehemu yoyote ndani ya Zanzibar. Hata hivyo, sheria hiyo chini ya kifungu cha 39 imeweka masharti ya Mzanzibari kupatiwa ardhi mbili tu za makaazi, ambapo ardhi moja atapatiwa katika eneo alilozaliwa na nyengine ni ardhi ya makaazi mbali na eneo alilozaliwa.

Aidha, Mzanzibari anastahili kupata ardhi moja kwa ajili ya kilimo. Kamati pia inatambua kuwepo kwa haki kwa Mzanzibari kupatiwa ardhi kwa ajili ya matumizi ya biashara au shughuli za viwanda kwa mujibu wa kifungu cha 39(3), (5) na (7). Hata hivyo, kifungu cha 39(7) kinataka eneo litakalotolewa kwa madhumuni ya biashara au shughuli za viwanda kufuata utaratibu wa sheria inayohusika na uwekezaji.

Kamati imebaini kuwa baadhi ya watu walipatiwa viwanja zaidi ya kimoja katika eneo hilo kwa madhumuni ya huduma. Hata hivyo, Kamati ilipohoji matumizi ya viwanja hivyo vilivyotolewa kwa ajili ya huduma, wizara haikuwa ikifahamu matumizi ya viwanja hivyo kwa kuwa ni muombaji mmoja tu ndiye aliyejaza fomu kuomba eneo hilo kwa mujibu wa vielelezo ambavyo Wizara ya Ardhi iliviwasilisha mbele ya Kamati. Hivyo, kuonyesha kuwa utaratibu wa sheria inayohusika na uwekezaji haukutekelezwa.

Kamati imebaini kuwa hatua hiyo ya wizara siyo sahihi kwa vile imekwenda kinyume na Sheria ya Matumizi Ardhi No.12 ya Mwaka 1992. Aidha, viwanja vilivyotolewa katika eneo hilo la Vitongoji, vimetolewa kwa madhumuni tofauti ambapo baadhi vimetolewa kwa matumizi ya kilimo wakati eneo hilo limepangwa kwa ajili ya uwekezaji jambo ambalo ni kinyume na utaratibu. Hivyo, kutoa ardhi hiyo kwa matumizi ya kilimo na makaazi ni kwenda kinyume na mpango uliowekwa.

Kamati inapendekeza kuwa wizara inayoshughulikia masuala ya ardhi isimamie kwa dhati mipango ya miji na vijiji kama inavyopangwa kwa mujibu wa sheria ili kuyaweka maeneo ya Zanzibar katika mpangilio mzuri.

Kamati inapendekeza kuwa upimaji na ugawaji wa maeneo ya ardhi ambapo tayari kumekuwa na manung’uniko kutoka kwa wananchi, uzingatie masharti ya sheria ya ardhi ili kuepusha migogoro ya ardhi.

Aidha, Kamati inashauri kuwepo mfumo unaoeleweka wa upimaji na ugawaji wa viwanja utakaokuwa wa uwazi na haki utakaowapa fursa wananchi wanaoshi maeneo yanayopimwa, nao kupatiwa viwanja hivyo.

HADIDU REJEA NAM. 9

Mgogoro wa Ardhi baina ya Wanakijiji na Mwekezaji, Pwani Mchangani.

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati

Katika kufuatilia hadidu rejea hii, kamati ilifuatana na Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini "A", watendaji wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na Mhe. Kazija Khamis Kona, aliyewasilisha malalamiko ya wananchi hao Barazani.

Kamati ilikutana na wanakijiji wanaolalamika ambao walieleza kamati kuwa kuna mwekezaji aliyefahamika kwa jina la Bw. Majura ambaye amejenga ukuta wa kuzungushia hoteli yake ambao umezuia njia ya wanaopita kwa miguu na sehemu ya uwanja wa mpira.

Wananchi pia walieleza kuwa Mwekezaji huyo ameuziwa eneo na kupimiwa mipaka yake ambayo inatambulikana kwa alama maalumu (*beacons*) ambazo anadaiwa kuzivuka hadi kuibana njia ya wanaopita kwa miguu. Imeelezwa kuwa watu wa upimaji ndiyo walioweka alama hizo (*beacons*) ambazo mwekezaji huyo amezivuka.

Serikali ya Wilaya iliieleza Kamati kuwa haikuwahi kuelezwa kuhusu mgogoro huo. Ingawa watu wa Wizara ya Ardhi walikuwapo hawakuweza kutoa ufafanuzi wowote wa usahihi wa mipaka iliyopimwa katika eneo hilo. Kamati ilitaka kupata maelezo ya Mwekezaji huyo ambaye bahati mbaya yupo nje ya Zanzibar na jitihada za kumpata Mwakilishi wake hazikuzaa matunda.

Aidha, kamati iliitaka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuipatia kamati nakala ya kielelezo chenye kuonesha uhalali wa matumizi ya eneo hilo kwa Bw. Majura pamoja na "*site plan".* Pamoja na jitihada za kamati kuikumbusha Wizara hiyo kuhusu kielelezo hicho, wizara hiyo ilishindwa kufanya hivyo hadi wakati wa kuwasilisha ripoti hii (tafadhali rejea Kiambatanisho Nam. KTA. 9) ambayo ni barua ya kamati kwa wizara inayohusika na ardhi ya tarehe 22/10/2013.

MAONI YA KAMATI

Katika kadhia hii Kamati ilihitaji vielelezo kadhaa ili kuweza kufanya uchambuzi sahihi. Miongoni mwa vielelezo ambavyo Kamati ilivihitaji kutoka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ni nyaraka za uhalali wa matumizi ya eneo la Bw. Majura, *'site plan"* ya eneo hilo na nyaraka zinazoonyesha hatua mbali mbali za uombaji wa eneo hilo.

Pamoja na hatua mbali mbali zilizochukuliwa na Kamati katika kuhakikisha kuwa inapatiwa vielelezo hivyo, ikiwa ni pamoja na kuiandikia wizara barua mara kadhaa, wizara imeshindwa kuipatia Kamati vielelezo hivyo hadi wakati wa kuwasilisha ripoti hii.

Kamati imesikitishwa na hatua ya wizara kushindwa kuwasilisha vielelezo hivyo wala kutoa maelezo yoyote kuhusu kadhia hiyo licha ya kukumbushwa kwa barua juu ya wajibu wao wa kuwasilisha vielelezo hivyo.

HADIDU REJEA NAM. 10

Mgogoro wa Ardhi baina ya wananchi na viongozi wakuu wa juu wa serikali, Tondooni

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati

Kamati ilipokuwa inaifanyia kazi hadidu rejea hii ilifuatana na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na watendaji wake, Watendaji Wakuu wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Mheshimiwa Ali Salum Haji, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ambaye ndiye aliyetoa hoja hiyo wakati wa Mkutano wa Baraza.

Mjumbe huyo aliieleza Kamati kuwa akiwa na baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, alipokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa Tondooni wakati Kamati ilipokuwa ikipita eneo hilo, kuwa eneo lao limechukuliwa na viongozi wa serikali.

Baada ya kuhojiwa na Kamati ili abainishe viongozi wanaodaiwa kuchukua eneo hilo, Mjumbe aliieleza Kamati kuwa kiongozi aliyeelezwa na wanachi kuhusika na uchukuaji wa eneo hilo ni Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba Bw. Dadi Faki Dadi.

Wananchi walilalamika walipopata fursa ya kuzungumza na kamati teule walieleza kuwa malalamiko yao yanahusu shamba ambalo Mkuu wa Mkoa

wa Kaskazini Pemba, Bw. Dadi Faki Dadi amewanyang'anya. Walidai kuwa Bw. Dadi Faki alikuja akawataka wakulima hao kuliachia eneo hilo kwa vile kuna mwekezaji ambaye anaisaidia serikali aliyetaka kuwekeza katika eneo hilo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa huyo, alieleza kamati kuwa yeye siye anayemiliki eneo hilo kama inavyodaiwa na anayemiliki eneo hilo ni mwekezaji aitwaye Ronit. Anachohusika yeye ni kule kusimamia malipo yaliyotolewa na mwekezaji huyo ambayo aliagizwa na Mhe. Mansoor Yussuf Himid (aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati) kuyasimamia, kwa vile mwekezaji huyo alishapoteza fedha nyingi ambazo hazikuwa zikiwafikia walengwa.

Kwa mujibu wa maelezo ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, kupitia Mkurugenzi wake wa Ardhi na Usajili, aliieleza kamati kuwa eneo hilo lenye ukubwa wa hekta 4.4 limekodishwa kwa mwekezaji aitwaye Ronit Hershkovitz, huyu ni raia wa Israel, kuanzia tarehe 28/2/2008 kwa mkataba wa miaka 66, kwa malipo ya dola za Kimarekani 11,500. Wizara iliipatia Kamati hati ya Mkataba wa Ukodishaji wa eneo hilo kwa Ndg. Ronit Hershkovitz na hati hiyo inaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho Nam. KTA 46.

Aidha, wizara iliieleza Kamati kuwa wananchi wa eneo hilo walilipwa jumla ya Shilingi 50 milioni kama fidia zao na aliyewawakilisha kwa Hati ya Uwakala (*Power of Attorney)* kwenye malipo hayo ni Ndg. Shaame na kueleza kuwepo kwa orodha ya waliolipwa licha ya orodha hiyo kutowasilishwa mbele ya Kamati. Kamati ilielezwa kuwa waliosimamia malipo hayo pamoja na Ndg. Shaame, Ndg. Msellem na Ndg. Nassor Mmanga.

Walalamikaji waliiambia kamati kuwa uthibitisho wao wa umiliki wa mashamba hayo ni urithi kutoka kwa wazee wao ambao walikuwa wakiyatumia maeneo hayo kwa kilimo.

Aidha, wanachi hao walifungua kesi katika Mahakama ya Ardhi dhidi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba, Ndg. Faki Dadi Faki pamoja na Mkuu wa Idara ya Ardhi Pemba, wakidai kutotendewa haki kwa kushurutishwa kuachia maeneo waliyokuwa wakiyatumia kwa malipo kidogo. Kesi hiyo namba 50 ya 2010, iliamuliwa kwa kuwapa haki katika eneo hilo walalamikaji Ndg. Mpongwe Juma na wenzake saba (7). Nakala ya hukumu na mwenendo wa kesi hiyo inaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho Nam. KTA. 47.

MAONI YA KAMATI

Kwa kuzingatia maamuzi na mwenendo wa kesi iliyofunguliwa katika Mahakama ya Ardhi, Pemba baina ya Mpongwe Juma Simba na wenzake dhidi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na Mkuu wa Idara ya Ardhi, Pemba, kesi namba 50 ya 2010, Mahakama iliamua kuwa eneo hilo kurejeshwa mikononi mwa walalamikaji Mpongwe Juma Simba na wenzake 7. Maamuzi ya kesi hii yalitoka tarehe 17/11/2011 na hakuna kumbukumbu yoyote ya kutenguliwa kwa maamuzi ya Mahakama hii.

Aidha, kwa mujibu wa mwenendo wa kesi hii, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba ambaye alifunguliwa kesi hii kwa dhamana yake ya Mkuu wa Mkoa huyo wa Kaskazini Pemba na kupitia kwa Mwanasheria wa Ofisi ya Mkoa wake, aliiomba Mahakama kuondoa shauri hilo kutokana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kutoshiriki kwa namna yoyote katika suala hilo na kuieleza Mahakama kuwa Mkuu wa Mkoa huyo ushiriki wake katika kadhia hiyo ulikuwa wake binafsi na si kupitia ofisi yake.

Kamati inaamini kuwa suala hili halikupaswa kuwa la kibinafsi kwa kuwa mwekezaji wa eneo hilo alipatiwa mkataba wa ukodishwaji wa eneo hilo na Taasisi ya Serikali na Serikali ya Mkoa imekiri kuhusika katika kufanikisha suala hilo.

Kwa maana nyingine kama Mkuu wa Mkoa hakushiriki katika suala hilo la kusaidia kwa ajili ya kupatikana kwa eneo hilo kwa mujibu wa wadhifa wake, inaweza kuaminika kuwa serikali haikulipa fidia kwa wananchi waliokuwa na vipando vyao katika eneo hilo.

Kamati imebaini kuwa utaratibu uliotumika katika kulipa fidia ulikuwa wa kienyeji na haukufuata taratibu za kiserikali kwa mujibu wa kifungu cha 56 cha Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 1992.

Kamati inashauri kuwa hasa kwa kuzingatia maamuzi ya Mahakama ya Ardhi serikali iwalipe fidia wananchi hao kabla ya kuchukuliwa eneo hilo kwa mujibu wa thamani zake.

Kamati pia inashauri serikali kuandaa utaratibu maalum wa fidia na kuiachia taasisi moja ya serikali kusimamia ulipaji wa fidia na utaratibu huo uwekwe wazi na kujulikana kwa wanaotaka kuwekeza ili kuepuka mianya ya rushwa.

Mgogoro wa ardhi baina ya Idara ya Upimaji na Ramani na Wizara ya Kilimo, Tumbe, mgogoro ambao umepelekea wananchi kulivamia eneo hilo.

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati

Kamati iliishughulikia hadidu rejea hii kwa kufanya kikao cha pamoja katika eneo la Tumbe, kilichowashirikisha Maafisa Wadhamni wa wizara husika ambao ni wa Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Katibu Mkuu wa Wizara, inayoshughulikia ardhi, Naibu Katibu Mkuu na ambaye kwa wakati huo alikuwa akikaimu nafasi ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, Mkurugenzi wa Ardhi na Usajili, Mkuu wa Wilaya ya Micheweni, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Sheha wa eneo hilo na watendaji wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Kamati ilielezwa na Afisa Mdhamini wa Wizara ya Kilimo kuwa wizara hiyo ilikuwa ikimiliki shamba katika eneo hilo la Tumbe ambalo lilianza kuvamiwa na kufanya makaazi na wananchi kwa kushirikiana na watendaji wasio waaminifu na waliokuwa wakisimamia shamba hilo.

Maafisa Wadhamini wa wizara ya Kilimo na Maliasili na wa Wizara ya Ardhi waliieleza Kamati kuwa kwa wakati huo ambao Kamati inafanya kikao hicho, hakukuwa na mgogoro baina ya wizara hizo mbili kufuatia makubaliano rasmi yaliyofanywa na wizara hizo mbili tarehe 13/07/2012. Nakala ya barua ya makubaliano hayo inaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho Nam. KTA 48.

Katika makubaliano hayo, Wizara ya Kilimo na Maliasili walikubali kutoa eneo walilokuwa wakilitumia kwa shughuli za kilimo na ambalo lilishavamiwa na wananchi na wizara hiyo kuwapa wizara ya ardhi ili wakate viwanja kwa ajili ya ujenzi na Wizara ya Ardhi nayo kwa upande wake ilitoa shamba walilokuwa wakilimiliki karibu na shamba la wizara ya Kilimo na kuwapatia wizara ya Kilimo shamba hilo.

Hata hivyo, Wizara ya Kilimo ilishindwa kuanza kulitumia eneo walilokubaliana kupatiwa na Wizara ya Ardhi kutokana na kuonyeshwa mipaka isiyo sahihi ambayo ilijumuisha eneo la mwananchi aliyepatiwa eneo hilo kwa mujibu wa sheria. Hadi wakati Kamati inafuatilia suala hili, hakukuwa na muafaka uliofikiwa kuhusu eneo linalomilikiwa na mwananchi huyo ambalo pia ni sehemu ambayo Wizara ya Kilimo walipatiwa na Wizara ya Ardhi.

Kwa upande wake Wizara ya Ardhi ilieleza kuwa wana mipango ya kuwahalalishia wananchi waliovamia maeneo yaliyokuwa yakimilikiwa na Wizara ya Kilimo, kwa madhumuni ya ujenzi wa makaazi.

MAONI YA KAMATI

Katika kufuatilia mgogoro huu, Kamati imebaini kutokuwepo kwa udhibiti wa kutosha wa maeneo ya serikali na kukosekana kwa uaminifu miongoni mwa watendaji wa serikali wanaopewa dhamana ya kusimamia maeneo hayo.

Kitendo cha mtendaji wa serikali aliyefahamika kwa jina la Mselem ambaye alipewa dhamana ya kusimamia maeneo ya kilimo huko Tumbe, Pemba, kuyatoa maeneo hayo kwa wananchi bila ya kufuata taratibu za sheria, ni kitendo cha aibu, kinachorudisha nyuma mipango ya maendeleo ya nchi na kukaribisha migogoro ya ardhi isiyo ya lazima. Hivyo, Kamati inapendekeza serikali kuchukua hatua.

Aidha, kutokana na jambo hili kuchukua muda mrefu katika kufikia makubaliano baina ya Wizara ya Ardhi na ile Wizara ya Kilimo na hivyo, kusababisha wananchi wengi kuvamia maeneo ya serikali, Kamati inapendekeza kuwa taasisi za serikali zinapobaini mapungufu katika utekelezaji wa shughuli zao, zichukue hatua haraka ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

HADIDU REJEA NAM. 12

Mgogoro wa ardhi baina ya wananchi na mwekezaji, Shehia ya Mzwardini, Bwejuu.

Namna ilivyoshughulikiwa na Kamati

Katika kufatilia hadidu rejea hii kamati iliambatana na Serikali ya Wilaya, watendaji wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Mhe. Hamza Hassan Juma, ambaye amewasilisha hoja hiyo Barazani.

Mhe. Hamza Hassan Juma, alifahamisha kamati kuwa mzozo wa eneo hilo ulianza kwa mwekezaji mzalendo Bw. Khatib Jecha Zidi, ambaye amejenga nyumba eneo la ufukwe ambayo imeziba njia ya wanaopita kwa miguu kuelekea pwani.Wananchi waliokutana na kamati walieleza kuwa njia hiyo imekuwa ikitumika na wanakijiji kuelekea pwani kwa shughuli zao za kutafuta riziki.

Kwa mujibu wa maelezo ya Serikali ya Wilaya waliagizwa na Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kushughulikia na kuchukua hatua za kuvunja ukuta huo. Serikali ya Halmashauri ilichukuwa hatua kwa kuwaita wahusika wote na kuwasikiliza.

Kabla ya kutolewa taarifa ya kuvunja ukuta huo, ilitolewa taarifa nyengine kutoka Idara ya Mazingira, kwa barua ya tarehe 14/3/2012, ikimtaka Bw. Khatib Jecha Zidi kuchukuwa hatua ya kuvunja ukuta huo na kuacha njia ya kupita wananchi. Barua hiyo inaambatanishwa na ripoti hii kama Kiambatanisho Nam. KTA. 49.

Kwa taarifa hiyo, Serikali ya Halmashauri ilishindwa kuendelea kuchukua hatua kwa vile tayari ya Idara ya Mazingira ilitangulia.

Kamati imefahamishwa kuwa Bw. Khatib Jecha Zidi alikaidi maagizo hayo kwa madai kuwa jirani yake aliyejenga mwanzo, Bw. Abdulsatar ndiye ameongeza ukuta wake hadi kwenye eneo lake.

Kamati ilielezwa kuwa, Serikali ya Wilaya ilipomwita Bw. Abdulsatar, alikuwa na vielelezo vyote vya umiliki wa eneo lake na wala Serikali hiyo ya Wilaya haikuwahi kupokea malalamiko ya Bw. Khatib Jecha Zidi dhidi ya Bw. Abdulsatar.

Aidha, Bw. Khatib Jecha Zidi alipotakiwa atoe vielelezo vyake vinavyoonyesha uhalali wa haki yake ya matumizi ya ardhi, alishindwa kufanya hivyo. Kamati iliitaka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuwasilisha mbele ya kamati vielelezo vinavyoonesha uhalali wa matumizi ya maeneo yanayotumiwa na Bw. Khatib Jecha Zidi na Bw. Abdulsatar, lakini hadi wakati wa kuwasilisha ripoti hii, wizara hiyo imeshindwa kuwasilisha vielelezo hivyo.

Tafadhali rejea Kiambatanisho Nam. KTA. 9, ambayo ni barua ya Kamati kwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ikikumbushia kupatiwa vielelezo mbali mbali vikiwemo nyaraka za hati za matumizi ya ardhi pamoja na *"site plan"* kwa Bw. Khatib Jecha Zidi na Bw. Abdulsatar.

MAONI YA KAMATI

Kamati imebaini kuwepo kwa usimamizi usioridhisha wa sheria za ujenzi na sheria ya ardhi No.12 mwaka 1992, kwa taasisi zinazohusika na usimamizi wa

sheria hizo. Sheria ya Umiliki wa Ardhi *No*.12 ya mwaka 1992, imeweka sharti kwenye kifungu cha 5(1) kwa mtu yeyote anayekaa karibu na eneo la bahari, kuacha njia ya wanaopita kwa miguu angalau mita kumi. Hata hivyo utaratibu huu wa sheria unaonekana hausimamiwi ipasavyo kutokana na kuwepo kwa tatizo la njia katika eneo hilo. Kumeonekana mapungufu ya Mamlaka husika kushindwa kuchukua hatua za haraka za kuzuwia ujenzi usiozingatia Sheria.

Sheria ya Umilikaji Ardhi *No*.12/1992 kifungu cha 6(d), imetowa uwezo kwa hatua kuchukuliwa kwa yeyote atakayevunja agizo la sheria ya Ardhi. Pamoja na kifungu hicho cha 5(1) cha sheria ambacho kinaelekeza haki ya njia kukiukwa, mamlaka husika zimeshindwa kuchukua hatua za haraka.

Kamati inashauri kuchukuliwa kwa hatua kwa mtu yeyote anayekiuka sheria wakati wa ujenzi. Aidha watendaji wa Halmashauri ya Wilaya husika walipoitwa mbele ya Kamati pamoja na watendaji wa Idara ya Mazingira, walikubali kuwa na mamlaka ya kuchukua hatua na kwamba wangelifanyia kazi suala hilo.

Aidha Kamati inapendekeza ujenzi katika eneo hilo uzingatie sheria kwa kuondosha sehemu isiyoruhusiwa ili kupisha njia. Hata hivyo, kamati iliomba kupatiwa nyaraka mbali mbali zikiwemo hati ya umiliki wa eneo hilo na *'site plan'* lakini hadi wakati wa kuwasilisha ripoti hii, Wizara imeshindwa.

Hitimisho:

Waheshimiwa Wajumbe, ripoti yetu tuligawa sehemu tatu, tulianza na muhtasari wa historia, halafu tukenda katika zile hoja ambazo Waheshimiwa Wawakilishi walizileta na kuzifanyia kazi pamoja na vielelezo ambavyo nimekabidhiwa na hiyo kwa mujibu wa sheria za Baraza. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumaliza zake, Kamati Teule inatoa mapendekezo yafuatayo:

1. Wananchi kuelimishwa kuhusu dhana ya ardhi kuwa mali ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ipo haja kubwa kwa wananchi kuelimishwa juu ya dhana ya ardhi kuwa mali ya serikali kwa kuwa Kamati imebaini dhana hiyo kutofahamika vyema miongoni mwa wananchi. Wananchi wengi ambao kwa namna fulani wamekuwa wakiyatumia baadhi ya maeneo bila ya kuwa na nyaraka yoyote ya kuthibitisha haki walizonazo katika ardhi hizo, wamekuwa wakidhani kuwa wana haki zote katika maeneo hayo na kwamba serikali haina mamlaka yoyote katika maeneo hayo.

Kamati inapendekeza kuchukuliwa kwa jitihada kubwa katika kuwaelimisha wananchi juu ya dhana hiyo ili kuepusha migogoro. Aidha ni vyema pia wananchi wakaelimishwa juu ya umuhimu wa kutafuta nyaraka zenye kuthibitisha haki walizonazo katika ardhi kupitia taasisi husika za Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ili kuepuka migogoro ya ardhi.

2. Watendaji wa Wizara inayohusika na Ardhi na Watendaji wengine wa Serikali kuelimishwa Sheria za Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa kutekeleza majukumu yake, Kamati ilibaini mapungufu mengi miongoni mwa watendaji wa Wizara inayoshughulikia ardhi, lakini pia miongoni mwa Watendaji wengine wa Serikali. Mapungufu hayo yametokana na Sheria za Ardhi kushindwa kusimamiwa ipasavyo na hivyo, kuwa chanzo cha migogoro mingi ya ardhi hapa Zanzibar.

Kamati inapendekeza kutolewa mafunzo ya kina kwa watendaji wa Wizara inayosimamia masuala ya ardhi, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Ofisi za Wakuu wa Wilaya, Idara ya Mazingira na Watendaji wengine wa serikali wanaohusika katika taratibu za utoaji wa maeneo ya ardhi pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Mafunzo hayo yatasaidia Watendaji hao kutekeleza majukumu yao kwa kujiamini zaidi na kwa kuzingatia Sheria.

3. Sheria za ardhi zisimamiwe vyema.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na mapungufu mengi ya Kisheria na Kikanuni yaliyoonekana wakati Kamati ikitekeleza majukumu yake, Kamati inapendekeza kuchukuliwa hatua madhubuti za kusimamia Sheria za Ardhi na Sheria nyengine za nchi zinazohusiana na masuala hayo ya ardhi. Miongoni mwa hatua zinazopaswa kuchukuliwa ni pamoja na kutungwa kwa Kanuni kwa kila Sheria inayohitaji kutungwa kwa Kanuni.

Kamati ilibaini kutotungwa kwa Kanuni nyingi zinazohusiana na masuala ya ardhi na hivyo kusababisha utekelezaji wa baadhi ya mambo kuwa na hitilafu kutokana na kukosa muongozo wa Kanuni. Aidha Kamati inapendekeza watendaji wote wa serikali waliopewa dhamana ya kusimamia utekelezaji wa sheria zinazohusiana na ardhi watekeleze wajibu wao kwa mujibu wa sheria hizo.

4. Serikali iongeze kasi ya utambuzi wa ardhi *(Land Adjudication).*

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na migogoro mingi iliyopo maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba ambayo wananchi wamekuwa wakidai kuyamiliki maeneo hayo, Serikali haina budi kuongeza jitihada katika zoezi la utambuzi wa ardhi *(Land Adjudication*) kama njia mojawapo ya Wazanzibari kupata haki ya matumizi ya ardhi kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha sheria ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 1992.

Pamoja na kutambua juhudi za serikali kwa kuanza zoezi hilo kwa baadhi ya maeneo, Kamati inapendekeza kuwa serikali iwekeze fedha na rasilimali nyengine zaidi ili zoezi hilo liende kwa haraka zaidi kwa maeneo yote ya Unguja na Pemba na kuwatambua wenye haki ya maeneo husika na kuwapatia nyaraka zinazohusika. Kamati inaamini zoezi hilo la utambuzi litakapokamilika litaondoa migogoro mingi ya ardhi hapa Zanzibar.

5. Mpango wa matumizi ya ardhi *(Land Use Plan).*

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inapendekeza kuharakishwa kwa mapitio ya mpango wa matumizi ya ardhi kwa Unguja na Pemba ili kuifanya miji yetu kuwa na haiba na pia kuepusha migogoro inayoweza kujitokeza. Aidha Kamati inapendekeza kusimamiwa ipasavyo kwa mpango huo wa matumizi ya ardhi kwa kuwa kumekuwepo na tatizo kubwa katika usimamizi wa mpango uliopo ambapo baadhi ya maeneo yamekuwa yakitolewa kwa watu mbali mbali kinyume na mpango wa matumizi ya maeneo hayo.

6. Sheria zote na Sera za Ardhi zifanyiwe mapitio.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na matatizo mengi yaliyojitokeza katika suala la ardhi, Kamati inapendekeza kufanyiwa mapitio ya kina ya Sheria zote za ardhi pamoja na Sera zilizopo ili kubaini mapungufu yaliyopo na kurekebisha au kuandika upya Sheria hizo pale itakapolazimu. Kamati inapendekeza kuwa zoezi hilo lifanywe kwa umakini mkubwa kwa madhumuni ya kuondosha kabisa tatizo hilo badala ya utaratibu wa sasa wa kuleta miswada ya marekebisho ya baadhi ya vifungu kwenye sheria hizo za ardhi.

7. Sheria ya "*Off Shore Decree*" sura ya 105 itekelezwe ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inapendekeza kuwa Sheria ya *"Off Shore Decree*" sura ya 105 inayohusu usimamizi wa maeneo ya fukwe isimamiwe ipasavyo. Katika kuisimamia Sheria hii, Kamati inapendekeza kupitiwa upya kwa mikataba yote inayohusu maeneo ya fukwe ili kuzingatia ni kwa kiasi gani mikataba hiyo imefuata masharti ya Sheria.

8. Uimarishaji wa Mahakama ya Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, Mahakama ya Ardhi Zanzibar iliundwa kwa madhumuni ya kupunguza kwa kiasi kikubwa migogoro ya ardhi kwa kuiweka Mahakama maalum itakayosikiliza mashauri yanayohusu ardhi pekee na hivyo, Mahakimu wa Mahakama hiyo kupata muda wa kutosha wa kusikiliza mashauri hayo ya ardhi. Hata hivyo, dhamira hiyo bado haijazaa matunda kwa kiasi kikubwa kutokana na Mahakama hiyo kushindwa kuhimili kesi hizo na kufanya mashauri mengi ya ardhi kuchukua muda mrefu.

Kutokana na uzito wa suala hili la ardhi, Kamati inapendekeza kuwa serikali ifanye mapitio ya kina ya Sheria ya Kuanzisha Mahakama ya Ardhi ili kubaini mapungufu na hatimaye kuifanyia marekebisho au kutungwa kwa sheria mpya kadri mapitio hayo yatakavyokuwa.

Aidha Kamati inashauri kuwa baada ya mapitio ya sheria ya Mahakama hiyo, serikali iwekeze rasilimali za kutosha katika Mahakama hii ili iweze kuwa na Mahakimu wa kutosha kwa kila Mkoa Unguja na Pemba na watendaji wengine wa Mahakama, majengo yenye nafasi ya kutosha na yenye hadhi ya Mahakama pamoja na rasilimali nyengine muhimu zinazohitajika katika kuifanya Mahakama hii itekeleze majukumu yake ipasavyo.

9. Uratibu kwa taasisi za Serikali zinazohusika na ukodishwaji wa ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilibaini pia kutokuwepo kwa uratibu (Co-*ordination)* miongoni mwa taasisi za serikali zinazohusika katika masuala ya ukodishwaji wa ardhi, ambapo taasisi mbali mbali za serikali zimekuwa zikikizana katika hatua wanazochukuwa. Jambo hili linadhoofisha utendaji na kukosesha kupatikana kwa ufanisi miongoni mwa taasisi hizo na pia kupelekea migogoro ya ardhi isiyo ya lazima.

Hivyo, Kamati inapendekeza kuwepo kwa uratibu madhubuti miongoni mwa taasisi za serikali kwa kuweka kituo kimoja *(One Stop Centre)* kitakachoratibu masuala ya ardhi hasa katika kushughulikia mikataba ya ukodishwaji wa ardhi, ambacho kitawahusisha watendaji wa taasisi mbali

mbali za serikali ambao watakuwa na ufahamu wa aina moja *(common understanding)* juu ya masuala ya ardhi wanayoyashughulikia.

10. Kuwepo kwa *Database* ya kuhifadhi kumbukumbu za ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imebaini mapungufu kadhaa ya kukosekana kwa kumbukumbu za maeneo ya ardhi yaliyotolewa kwa watu mbali mbali. Kasoro hii imechangia kwa kiasi kikubwa kuibuka kwa migogoro ya ardhi hapa Zanzibar ikiwemo kutolewa hati zaidi ya moja kwa eneo moja, kutolewa maeneo ya ardhi kinyume na mpango wa matumizi ya ardhi kwa eneo husika na kadhalika. Hivyo, Kamati inapendekeza kuwepo kwa "*database*" hiyo itakayohifadhi kumbukumbu zote za maeneo yaliyotolewa Unguja na Pemba na taarifa nyengine muhimu.

11. Viongozi na Watendaji wa Wizara ya Ardhi kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu masuala ya ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa wananchi wengi wa Zanzibar hawana taarifa za kutosha kuhusu mambo mbali mbali yanayohusiana na ardhi jambo ambalo linachangia katika kuibuka kwa migogoro ya ardhi. Miongoni mwa taarifa hizo ni masharti muhimu ya kuzingatiwa kwa wananchi kupata haki ya matumizi ya ardhi, ikiwa ni pamoja na sharti la kuendeleza eneo ndani ya kipindi cha miaka miwili baada ya kupewa hati ya muda ya matumizi ya ardhi, kuomba hati ya kudumu ya matumizi ya ardhi baada ya kuendeleza eneo na kadhalika, mambo ambayo yamekuwa hayafahamiki miongoni mwa wananchi wengi.

Hivyo, Kamati inaunga mkono kauli ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein, iliyonukuliwa katika gazeti la Zanzibar Leo la Novemba 13, 2013, aliyoitoa mbele ya Viongozi na Watendaji wa Wizara ya Ardhi wakati wa kujadili ripoti ya utekelezaji wa Wizara hiyo hivi karibuni ya kuitaka Wizara hiyo kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu mipango mbali mbali inayotekelezwa na Wizara hiyo.

12. Ufutaji wa Haki ya Matumizi ya Ardhi ufuate misingi ya Katiba na Kifungu cha 56 cha Sheria ya Matumizi ya Ardhi

Kamati Teule inashauri kuwa serikali inapotaka kufuta hati ya haki ya matumizi ya ardhi ni vyema ikafanya hivyo kwa kufuata masharti ya kifungu

cha 17 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, pamoja na masharti ya kifungu cha 56 cha Sheria ya Umiliki Ardhi Na.12/1992.

Kifungu cha 17 cha Katiba ya Zanzibar 1984, kinaeleza kuwa:-

> *"*hakuna mali ya mtu yeyote itakayochukuliwa kwa nguvu na hakuna maslahi au haki yoyote inayotokana na mali hiyo itakayochukuliwa kwa nguvu, isipokuwa pale ambapo masharti yafuatayo yametimizwa" yaani:
>
> a) Kumilikiwa au kuchukuliwa kwa mali hiyo ni muhimu sana kwa ajili ya ulinzi, usalama wa wananchi, mazingira ya afya, kuimarisha maendeleo ya upangaji wa mji pamoja na kuendeleza mambo ambayo yataleta faida kwa wananchi kwa ujumla,
>
> b) Umuhimu wa kuchukuliwa kitu hicho ni mkubwa sana hata kwamba unahalalisha uchukuaji wake hata kama utampa ugumu na matatizo mwenye mali hiyo,
>
> c) Sheria imewekwa kuhusiana na umilikaji au uchukuaji huo kwa kutoa fidia inayolingana.

Aidha kifungu cha 56 cha sheria Na. 12/1992 kinaweka sharti la namna ya uchukuaji wa haki ya matumizi ya ardhi. Kifungu hicho kinaitaka serikali iwapo inataka kufuta haki ya matumizi ya ardhi kwa maslahi ya umma, lazima ithibitishe kwenye Mahakama ya Ardhi uwepo wa sababu za msingi za kuchukua ardhi hiyo. Mbali na kuthibitisha huko, sheria inaelekeza fidia ya thamani ya soko ilipwe kwa ardhi hiyo inayotaka kuchukuliwa kwa maslahi ya umma.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho Kamati inapenda kushukuru Uongozi wa Baraza chini yako Mhe. Mwenyekiti, na Katibu wa Baraza kwa kuipa mashirikiano Kamati hii ambayo yameiwezesha Kamati kutekeleza majukumu iliyopewa kwa ufanisi. Aidha Kamati inapenda kumshukuru Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na watendaji wote wa Wizara yake, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya pamoja na watendaji wa Ofisi zao na watendaji wengine na wananchi wote waliotoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati hii.

Pia, Kamati inawashukuru Wajumbe mbali mbali wa Baraza la Wawakilishi ambao walikubali kushirikiana na Kamati kwa kuipatia ufafanuzi wa hoja walizozitoa ndani ya Baraza.

Kabla ya hatujamaliza, ni vyema tukatambua kuwa Kamati hii ndio Kamati pekee iliyoridhiwa na Wajumbe wa Baraza wote na Serikali kwa kauli moja na hapa Kamati inaomba kunukuu maneno yako Mheshimiwa Spika, wakati unaitangaza Kamati Teule,

Lakini jambo lenyewe tayari limeshakubalika Waheshimiwa Wajumbe walisema na Mheshimiwa Waziri akasema kwa kweli na mimi naona nisaidiwe, yaani nakubali hiyo Kamati Teule iundwe. Kwa maana hiyo, kulikuwa na *agreement* kwa pande zote mbili kwa upande wa serikali pamoja na Waheshimiwa Wajumbe.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, naomba nimnukuu Mhe. Waziri wa Ardhi wakati wa majumuisho ya taarifa ya serikali kuhusu ripoti ya *ZECO* katika mkutano wa Baraza wa kumi na tatu ambapo alisema na namnukuu;

> "Mimi naomba kwamba hii ripoti nipewe, yaani ripoti ya *ZECO* kwenda kuifanyia kazi. Itakapopokelewa hapa nitapata nguvu ya kwenda kuifanyia kazi hii ripoti. Ikikataliwa nitaifanyia kazi, lakini nitakuwa naifanyia kazi tu, lakini nitajua sina *support*, maana yake ni ripoti yetu hii lazima niifanyie kazi mimi, itanisaidia hii na ile ripoti ya ardhi ile naomba iletwe alau nipate kuifanyia kazi''

Mhe, Mwenyekiti, mwaka 1980 wakati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Aboud Jumbe analizindua Baraza la Wawakilishi na kwa bahati njema viongozi siku hiyo waliokuwepo ni Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, alisema Baraza la Wawakilishi ni ngome.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimnukuu Waziri Kiongozi Brigedia Ramadhan Haji, muasisi wa mapinduzi, katika hotuba yake ya mwisho mwezi Disemba, 1983 ambapo alitoa tafsiri ya nini maana ya Baraza la Wawakilishi ni ngome ambapo alisema na naomba nimnukuu;

Hapa Mhe. Mwenyekiti, ninataka niseme hata siku hiyo wakati Mhe. Ramadhan Haji anatoa hotuba hiyo Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, alikuwepo:

> ''Maana ya Baraza la Wawakilishi ni ngome maana yake ngome ya kuwatetea wanyonge wapate haki sawa. Tangu mwaka 1964 hadi mwaka 1979 ngome ilikuwa katika Baraza la Mapinduzi. Kimapambano unaweza kusema kuwa makao makuu tu ndio yaliyohamishwa kutoka eneo fulani la vita kwenda eneo jengine. Sasa makao makuu ni Baraza la Wawakilishi.''

Mhe. Mwenyekiti, mimi Ali Mzee Ali nikiwa Mwenyekiti wa Kamati hii, kwa niaba ya Kamati ninayoiongoza, naiomba ngome hii ya Baraza ambayo ni sauti na kimbilio la wananchi wetu, waichangie na waichambue ili tumkabidhi Mhe. Waziri wa Ardhi akaifanyie kazi kama alivyoomba. Tunaamini Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, ambaye ni miongoni mwa askari wa mwanzo wa ngome hii mwaka 1980, ataifanyia kazi kwa dhati ili turudishe hadhi ya ardhi ya nchi hii na kuondosha migogoro ya ardhi na kuifanya rasilimali hiyo kuwafaidisha wananchi wote.
Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ali Mzee Ali.

Mhe. Ali Mzee Ali: Aah! inatosha. Sasa naomba kwa heshima na taadhima nitoe maoni yangu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, naona muda hauturuhusu.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe maoni yangu, muda upo.

Waheshimiwa Wajumbe eeh! Kifungu cha 9 cha Katiba ya Zanzibar kinasema ifuatavyo:-

> "Zanzibar itakuwa ni nchi ya demokrasi na haki ya kijamii" Kwa hivyo, hapa inaeleza rasmi kwamba mamlaka ya kuendesha nchi ni juu ya wananchi wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa serikali kufuatana na Katiba utatokana na wananchi wenyewe.

Kwa hivyo, wenye maamuzi ya kuendesha nchi ni wananchi wenyewe. Usalama na hali nzuri kwa wananchi itakuwa ndio lengo kubwa la serikali, Katiba itahakikisha kwamba wananchi wanashiriki katika serikali yao.

Mhe. Mwenyekiti, ninataka niseme neno moja, katika Katiba ya Zanzibar imeeleza Kifungu cha 43 (5),

> "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais, ndio itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za serikali kwa ujumla na Mawaziri chini ya uongozi wa Makamu wa Pili wa Rais watawajibika pamoja katika Baraza la Wawakilishi"

Kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi hiki ni kifungu cha Katiba. Sasa sera, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza Mapinduzi Dr.

Ali Mohammed Shein, ndio aliyeshinda na kuchukua bendera ya kuongoza serikali hii.

Na Dr. Shein, kwa mujibu wa makubaliano ya Katiba, Rais anayetoka katika chama ndiye atakayekuwa na sera. Sasa sera aliyeichagua serikali hii kuiendesha ni sera ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*).

Hakuna sera nzuri zaidi yenye manufaa zaidi, zaidi ya sera ya Chama cha Mapinduzi. Ni sera ya wanyonge.

Sasa sera inasemaje katika kipindi cha miaka 10 ijayo; 2010-2020 Chama cha Mapinduzi kitaendeleza jitihada zake za kuimarisha Utawala Bora kwa kufanya yafuatayo:-

1.Kuona kwamba serikali wakati wote inaendeshwa kwa kuheshimu na kuzingatia utawala wa sheria, yaani Katiba ya nchi, sheria, kanuni na taratibu zilizopo na ambazo zinaweza kutungwa na kukidhi haja ya wakati uliopo.

2. Kuhakikisha kwamba serikali inasimamia utekelezaji wa maadili ya uongozi kwa dhati ili kuimarisha Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Mzee Ali.

Mhe. Ali Mzee Ali: Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Mzee Ali, Kiti kinaamuru ukae kitako (*Makofi*).

Mhe. Ali Mzee Ali: Samahani kidogo. Mhe. Mwenyekiti, tafadhali naomba nimalize dakika 5.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Baraza linakwenda kwa mujibu wa taratibu. Tunaomba ukae kitako Mheshimiwa. (*Makofi*).

Tutakupa nafasi jioni.

Mhe. Ali Mzee Ali: Nitapata jioni.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza ninachukua fursa hii kukushukuruni sana kwa kusikiliza maelekezo ya taarifa ya Kamati Teule ambayo imetolewa hapa na Mhe. Ali Mzee Ali, zaidi ya masaa mawili na nusu.

Na sasa kabla sijaakhirisha kikao naomba nitoe tangazo kwamba wenyeviti wote wa kamati za kudumu za Baraza wanatakiwa mara baada ya kuakhirishwa kikao hiki wafike afisi ya Mshauri wa Baraza kuna taarifa muhimu.

Baada maelekezo hayo tunaakhirisha kikao hiki hadi jioni saa kumi na moja barabara. Ahsanteni.

(Saa 7.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii sasa nitowe maoni yangu. Wakati nikitoa maoni yangu nilifika pahala nikanukuu katiba na nikawa nasoma ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, nimepata simu nyingi sana, wananiambia wewe ulikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Watu Sita, mbona tena unasoma mambo ya mailani. Nikasema hawa hawajui. Mhe. Mwenyekiti, tulikubaliana kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa, mfumo ni kuwa chama chochote kinachoshinda, basi huyo Rais atakuwa na uwezo wa kutumia ilani. Kwa hivyo, Rais Dk. Ali Mohammed Shein aliamua kuitumia ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo, ni sawa sawa na katiba na ni sawa sawa na muungozo.

Kwa hivyo, nilisoma baadhi ya mambo ambayo yamo ndani ya ilani ya Chama cha Mapinduzi na nilifikiri pale nimeshamaliza, kwa sababu nilisoma yote na nilishamaliza kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, katika haya mabaraza kuna watu wanaitwa *deem*, hata kwenye ubalozi ni watu ambao ni wa muda mrefu. Kwa hivyo, kwa wanawake wa nchi hii *deem* ni Mhe. Asha Bakari Makame, kwa sababu ana muda mrefu sana. Kwa wanaume ni Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, hao ndio ma-*deems*. Sasa naomba nimnukuu Mhe. Asha Bakari Makame, kwa sababu nukuu yake ina mambo mengi sana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Asha Bakari Makame alizungumza wakati wa *ZECO*, lakini alisema maneno mazito ambayo hayawezi kuachwa hivi hivi ni lazima yaungwe mkono, alitoa indhari na alisema hivi;

"Jengine Mhe. Spika, uvamizi wa ardhi umekuwa mkubwa, namuonea huruma Mhe. Waziri, maana ameridhia madhambi lakini Mwenyezi Mungu atamsaidia, *Amin*"

Kwa sababu ameridhia madhambi makubwa sana ya uvamizi wa ardhi. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kwa kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kuwa ajitahidi inavyowezekana kwamba sasa zile sheria ambazo zina umiliki wa ardhi na kwa sababu kuna mahakama ya ardhi pamoja na mambo mengine. Kutokana na hali hiyo, nimuombe sana awakutanishe kwa ajili ya kupanga mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba ardhi sasa basi kuvamiwa. Wala sio kuvamiwa tu, isipokuwa mtu aangalie hapa je ni pahala pa kujenga, au kilimo au kwa ajili ya kufanya jambo gani hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nimuunge mkono Mhe. Abdalla Juma Abdalla, aliposema kwamba itafika wakati hata kile kisiki cha muhogo ukitaka kukipanda pembeni ya nyumba basi huna sehemu hiyo. Sasa namuomba Mhe. Waziri, kwa kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kuwa haya yote pia ayasimamie ipasavyo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nadhani tusimpige madongo Mhe. Waziri, pekee na sisi wenyewe miongoni mwetu tunayo matatizo. Kwa kweli mtu hataki kufuata taratibu na sheria na kama hataki kufuata hayo anapofikwa na janga, basi asimnung'unikie Waziri wala Muwakilishi. Kwa sababu atamfanya yule mheshimiwa ambaye ni mtunga sheria na yeye akiuke sheria.

Kwa hivyo, nitoe wito Mhe. Mwenyekiti, kwamba baadhi yetu sisi viongozi na wala sisemi Waheshimiwa Wawakilishi tu, isipokuwa na baadhi ya viongozi wengine, sisi ndio tuliosababisha tukavamia ardhi bila ya mpango wala bila ya kudhani kuwa hali hii italeta vurugu.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba kwa upande wa wananchi, niwasihi wananchi kuwa sio vizuri kugombana na utawala. Kwa hivyo, ni wajibu wetu kufuata taratibu za kisheria. Pia, maendeleo ya nchi huletwa na wananchi wenyewe na ukitaka kuweka vizuri kama kuna kitu hakipendezi basi ni lazima ukiondoe. Kwa kweli hivi sasa tusibakie kwenye karne iliyopita, ni lazima tufuate karne ambayo wenzetu wanaifuata. Kwa hivyo, nukuu hii niliona ni muhimu sana, na ni nukuu ya *deem* mmoja, Mhe. Asha Bakari Makame.

Mhe. Mwenyekiti, utaona hapa kuna *reports* mpaka 47 Chwaka, kuna *report* Vitongoji Pemba. Matatizo ya ardhi ni makubwa sana na kila mtu amezungumza na asili ya Mapinduzi au miongoni mwa sababu za Mapinduzi ni ardhi. Kwa sababu nchi ambazo wamefanya *land reform*, ni Zanzibar Cairo - Misri, China, Cuba na Urusi, kwengine kote hapana. Zanzibar ni nchi

ambayo imefanya *land reform* kwa sababu ardhi ilimilikiwa na wafalme, halafu Zanzibar ina ubaya mmoja, ni nchi pekee duniani ambayo mfalme ametawala mgeni. Kwa hivyo, hili suala la ardhi haliishi leo ni lazima tuandaliwe semina watu waelimishwe na wako ma-*professor* hapa wa mambo ya ardhi, tupewe elimu, kwa sababu historia yake kubwa na imetoka mbali.

Mhe. Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Zanzibar Dk. Ali Mohammed Shain, leo amekiongoza kikao cha kamati maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM Zanzibar, kilichofanyika Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui Mjini. CCM ilitoa *press* relea*se*. Sasa nasoma *press release* kuhusu ardhi. Naomba munisikilize kwa makini sana.

Mhe. Mwenyekiti, hapa wapo wanadhimu wa Chama cha Mapinduzi, wajumbe wa kamati hii, wapo wajumbe wa *NEC* na wapo wajumbe tumewachagua sisi. Hawa wote niliowataja walikuwepo siku hiyo na waliidhinisha uongozi huu, sasa bado kutekelezwa. Kikao kimeitaka serikali kuendelea na juhudi za kutatua migogoro ya ardhi katika mikoa mbali mbali ya Zanzibar, pamoja na kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria bila ya kuwaonea muhali wale wate watakaobainika kuwa ni chanzo cha kuibuka migogoro hiyo mikoani humo. Hiyo ni kauli ya kamati maalum ya Chama cha Mapinduzi.

Viongozi walihodhi na wanaoendelea kuhodhi maeneo makubwa ya ardhi kwa mujibu wa sheria, watakiwe kuyapunguza na kuwagaiya wananchi na wayatumie kwa shughuli mbali mbali za kilimo na ufugaji, ili kujipatia vipato halali baada ya kuwapatia maeneo mapya. Aidha, wakati wa ugawaji wa maeneo hayo serikali iwashirikishe na kuwapa kipaumbele wananchi wanaoishi katika maeneo husika, pamoja na kupiga marufuku maeneo ya kilimo kufanywa ya makaazi. Izuie ujenzi kwa maeneo ya vyanzo vya maji kuuzwa na kujengwa nyumba za makaazi ya watu. Hiki ndio kikao cha kamati maalum, kilisema mengi lakini mimi nazungumza juu ya ardhi.

Sasa Mhe. Waziri, wewe ni mjumbe wa *NEC*. Kwa hivyo, ningeshauri kwanza mujuane humu ndani wenye zaidi ya eka tatu, halafu wasiokuwa nayo maana "*Charity begins at home*", na tuwe mfano. Mhe. Waziri ulisema siku moja kwamba waturudishie ardhi yetu. Sasa umeshapata silaha kutoka ndani ya Chama cha Mapinduzi ambacho ndio chama kinachoongoza sera ya serikali hii.

Kwa hivyo, na wajumbe wa *NEC* mumsaidie. Mimi namjua mjumbe mmoja wa *NEC* na Mjumbe wa Kamati Kuu, kila siku analia, anaomba eka mbili tu maskini hana, msaidieni. Nitakunong'oneza Mhe. Waziri. Sasa niliona vile vile hili nilitowe kuonesha tu kama suala la ardhi sio suala la mchezo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nataka kumnukuu Mhe. Salmin Awadhi. Lakini namuomba Mhe. Waziri, *Hansard* ya Mhe. Salmin Awadh Salmin, ya juzi alisema maneno mengi sana, maneno muhimu sana na nataka nikubaliane naye kwamba hii kazi ambayo sisi tumepewa ni ngumu. Pia alisema kamati teule imeundwa na mpaka sasa hivi wanashindwa kuleta ripoti kwa sababu ya kazi ngumu. Ni kweli, hii ni historia alianza tangu Mzee Ali Hassan Mwinyi, ardhi ilikuwa na matatizo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye Mhe. Salmin Awadh Salmin, kwamba kazi hii ilikuwa ngumu na nyinyi wenyewe mmeiona na ni kazi ya muhali, lakini Mwenyezi Mungu atatusaidia kwa sababu sisi hatujamkusudia mtu, tumefanya tulilotumwa, hakuna lolote ambalo hatujatumwa. Tumbe tumetumwa na Spika kaiona. Kwa hivyo, wale wenye maneno ya chini chini hayana msingi. Sasa haya ni maoni yangu. Kwa haya maoni yangu niruhusa mtu kuyatolea maelezo. Lakini yale tumetumwa.

Mhe. Mwenyekiti, ni lazima turudi kwenye historia na tujifikirie. Sisi humu ndani nilisema ndio sauti ya wananchi, wananchi wanatusikiliza sana na lazima sisi tuwe na utaratibu wa kuyaenzi mambo mengi ambayo yamefanywa. Tarehe 10 Julai, Kikao cha Baraza la Mapinduzi, ndio Aprili wakati Mhe. Abdu Jumbe anapendekezwa kuwa Rais kabla ya Mzee Karume hajazikwa. Alipendekezwa na akakubali, wakenda kuzika, baada ya kuzika tu walirudi, Baraza la Mapinduzi la siku hiyo likatoa azimio la BLM la tarehe 10/07/1972.

Azimio linasema hivi;

> "Mhe. Rais wa *Afro Shiraz* na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Tanzania Mzee Abeid Aman Karume ameuwawa na amezikwa, lakini kilichouwawa ni kiwiliwili chake tu, chama na Baraza la Mapinduzi liko pale pale, mawazo, fikra, busara na maazimio yake yapo na yataendelea kudumishwa milele"

Mhe. Mwenyekiti, kama nitasema hapa niwaulize wajumbe ambao umri wao ni zaidi ya miaka 60 wanyanyue mikono, sijui kama wanafika watu sita. Kwa hivyo, wengi kati yenu ni matunda ya Mapinduzi na mna wajibu wa kuyaenzi Mapinduzi na kumuenzi huyu mzee na historia. Sasa kumuenzi kwake na yeye ni mtu aliyegombania ardhi, kwa hivyo hiyo ardhi tuitumie au tugawane kidogo kidogo, kwa sababu ardhi hii imekudusiwa kwa kilimo.

Aliposema chama kipo, kuna mtu mmoja aliniambia siku moja CCM, nikamwambia hapana, CCM ni mchanganyiko wa *TANU* na *Afro Shiraz*. Kwa

hivyo, Chama cha *Afro Shiraz* kipo kwenye CCM, Baraza la Mapindizi lipo na Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban wewe ni Mjumbe. Kwa hivyo, bado Baraza lipo na litaendelea kuwepo milele na milele.

Mhe. Mwenyekiti, sisi ndio tuliobeba bendera ya nchi hii, tuondoshe muhali tufuate sheria. *Reporti* yangu karibu asilimia 90 inazungumzia kufuata sheria. Dk. Salmin Amour mara nyingi alikuwa anasema sheria, sheria, tukifuata sheria ni mambo ya kheri.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nataka kumalizia pahala pazuri sana, lakini sipaoni, ngoja kidogo Mhe. Mwenyekiti. Dk. Bilal... Nistahamilieni kidogo hii ni ya mwisho. Mhe. Mwenyekiti, nitaipata. Tulizungumza hapa kuwa ardhi inapochukuliwa ni lazima utaratibu ufuatwe. Hapa ninao mfano;

The land aqusition decree Cap 105, 1946;

> *"In exercise of the power confined upon the British Residence and the above stated decree, noticed by given that all the piece of parcel of land, more particulary described of the scheduled here to, situated at Makunduchi in the district of Zanzibar is required by the Government for public purpose"*. Kwa madhumuni ya taifa.*"Namely to a recture of school building"*.

Sasa unapochukua ni lazima ueleze, unataka ardhi hii kwa madhumuni gani, ili watu wajuwe. A *detail plan on the said land prepared from survey plan number 2135 as deposited in the office of the district commissioner Zanzibar and opened for inspection,* na watu wakaone *scheduled all piece of parcel of land situated at Makunduchi in the district of Zanzibar and measuring 2.4 hecres forming part of the belonging.*

Nani wenyewe; Haji bin Pandu, Mmanga bin Daud bin Suleiman, Mcha bin Pandu, Ameir bin Vuai, Mkwezi bin Amour na Jussa bin Yakoub. Mhe. Ismail Jussa Ladhu, huyu babu yako nini. Hii kwa Zanzibar na Pemba *samething* ilichukuliwa na wako wenyewe, ilichukuliwa kwa ajili ya kujenga skuli tena Chake Chake na wenyewe ni Jaffar Issa Haji, Heirs *of* Mohammed Faki Mohammed, Saleh Ismail, Mahmoud Jaha bibi wa Kiungani. Kwa nini tumeweka hii kumbukumbu, ni kwa sababu ya kuonesha kwamba hivi vitu sio vipya, lakini utaratibu. Leo ukichukua ardhi ni lazima ufuate utaratibu, kama unataka kufanya mambo ya nchi uyaeleze ni mambo gani, sio tu unafuta na kuweka, hapana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi hii ni miaka 50, kwa hivyo tafadhalini sana nawaombeni na hasa serikali, tupige mstari uwe *at the centre of the desert.*

Baraza hili mwaka 1980 lilianzishwa, mawaziri waliopitia mambo ya ardhi tangu mwaka 1980 ni Abdu Talib, Ali Haji Pandu, Abubakar Khamis Bakar, Suleiman Seif na Ishau. Huo ni mwaka 1980 mpaka 1989 ikahamishwa ikawa Kamisheni ya Ardhi, ikahama kwenye ardhi ikenda zake kwenye Ofisi ya Waziri Kiongozi. Huko nako waziri akawa Ali Mohammed Shoka. Kwenye Kamisheni ya Ardhi ilikaa kwa mwaka mmoja tu, ikarudi tena ardhi katika mwaka 1990. Alianza Mhe. Salum Hashim, waziri wake wa nchi akawa Issa, akaja Mhe. Kamal Basha Pandu, Burhan Saadat Haji, waziri wake wa nchi akawa Mhe. Mansour Yussuf Himid, akaja Mhe. Mansour Yussuf Himid, Mhe. Ali Juma Shamuhuna na sasa yuko Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban.

Kwa hivyo, wajumbe wote hawa niliowataja ni *part and percel* la hili sokomoko. Wacha wale wanyuma, kuanzia Mhe. Idrissa Abdul Wakili, mimi nazungumza kuanzia Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo, kila mmoja kati yetu anahusika kwa upande mmoja au mwengine. Viwanja wameuza, tunachukua pesa, halafu waliouziwa tunawafutia, hiyo ni dhambi. Tukifungua ma-*internet* tunakuta ardhi zinauzwa. Sasa Mhe. Salmin Awadh Salmin, anasema tumuogope Mwenyezi Mungu, ardhi ni ya Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, kesho kutwa tunakwenda kusherehekea miaka 50 ya Mapinduzi, sasa Baraza hili tutowe azimio kuwa kazi kubwa itaanza baada ya tarehe 12 Januari, 2014 kuirejesha ardhi katika mikono ya wananchi wetu ili walime na mazao yapatikane.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimalize, isipokuwa nawaombeni ndugu zangu...

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano za ziada Mhe. Mjumbe.

Mhe. Ali Mzee Ali: Ndugu zangu nawaombeni tumpe kila msaada, kila nyenzo Mhe. Waziri na mlango wako wa nyuma na mbele uwe wazi, wawakilishi wawe wanaingia bila ya wasi wasi, upokee mawazo yao ili tufanye kazi, tumsaidie mwenzetu huyu, mwenzetu kaomba tusimpige madongo tu. Tukitoa michango leo tumsaidie ili tumpe miongozo na yeye naamini kuwa ni mtu mzuri, ni mpole, ana uwezo, mtu safi na ni mtu mwema. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwa kuchaguliwa kuwa Makamo Mwenyekiti wa Jumuiya ya Riadha. *(Makofi)*

Mhe. Ramadhan Abadalla Shaaban, mimi niko nyuma yako na nakuhakikishia na Baraza hili liko nyuma yako.

Mhe.Mwenyekiti, kwa hayo naomba kumaliza na mimi nasema naunga mkono *report* hii na nyinyi muunge mkono, lakini tuchangie, hata kama mpaka kesho au keshokutwa lakini wajumbe wachangie ili tumsaidie mwenzetu. Kwa hayo mafupi Mhe. Mwenyekiti, naomba kuondoka. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba sana sio vibaya ukiweka kanuni kando na mimi ukanipa angalau dakika 40. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, sio masihara hii *report* ni kubwa tena sana sijapata kuona. Mwenyekiti mwenyewe aliyeisoma pale pamoja na utuuzima wake anaonesha yuko mzima kabisa kuweza kuhimili vishindo na kuweza kusoma. Nampa pongezi sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nina ushauri mmoja. Ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti, na mara nyingi sana nikitoa ushauri basi Mhe. Rais huwa anausikiliza na anautekeleza, hilo nashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli hii wizara ni kubwa tena kubwa mno, tungeweza kuigawa katikati wizara hii, kwa sababu ukija nishati, ardhi na mengineyo sio masihara nampa pole sana Mhe. Maalim Ramadhan Abdalla Shaaban kwa hili, sio masihara.

Sasa namuomba sana Mhe. Rais afikirie hili jambo, siombi uwaziri mimi kwa sababu nimeshaomba sana sijapewa. Isipokuwa mara hii Mhe. Mwenyekiti, nitaomba moja tu, naomba uniruhusu, kazi iliyobakia sasa nimuombe Mhe. Rais wangu kipenzi changu, mwaka wowote atakaoamua kustaafu, basi anichaguwe mimi niwe Rais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niko *serious* kabisa, hayatatokezea madudu kama haya hata siku moja nikiwa Rais wa Zanzibar na kila mtu atapata haki yake.

Mhe. Mwenyekiti, Katika katiba hii ya Zanzibar kwenye ukurasa wa 30 kifungu cha 41 cha katiba hii, ili tumnusuru Mhe. Makamu wa Pili kutokupigaiwa kura ya kutokua na imani nae, waziri muhusika lazima aliyetajwa kwenye *report* ajiuzulu mwenyewe sio vibaya. Tena ni moja katika sifa nzuri sana, ilimuinua Mhe. Ali Hassan Mwinyi, kilitokezea kitu kama hicho, wala sio yeye maskini ya Mungu, wafungwa tu walikimbia, basi aliamua kujiuzulu na hatimae akawa Rais wa Zanzibar, kajiwekea sifa nzuri sana na ndio ushujaa. Kwa hivyo, tunaomba sana aliyetajwa kwenye *report* hii, ningewaomba kuwa bora mtu ajiuzulu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengine yalisemwa na wajumbe tukachangia, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando, alichangia na alitoa hoja, lakini kwa bahati mbaya au nzuri hakupewa kuwa mjumbe. Kwa sababu

kama tulivyosema kuwa lilikuwa zigo kubwa sana, sio mchezo, Mwenyekiti na katibu wake kwa kweli walitumia akili kubwa sana, walijitahidi kwa kadiri ya uwezo wao. Sioni tabu kuwa mengine walisahau. Kwa hivyo, hayo tutaweza kuyasema na ushahidi tunayo na tukenda katika *Hansard* utakuta yale yale tuliyosema yamo bado.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hili suala linasikitisha sana na linatia umaskini, naomba ninukuu;

> "Sisi tumejitawala ili uchumi wa nchi hii uwe mikononi mwetu, ikiwa yupo kiongozi anayewapa wageni fursa ya uchumi wa nchi, basi hafai"

Nanukuu tena Mhe. Mwenyekiti, labda Waheshimiwa Wajumbe hawajanisikia, naomba Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wanisikilize kwa makini sana, leo natulia wala sina haraka;

> "Sisi tumejitawala ili uchumi wa nchi hii uwe mikononi mwetu, ikiwa yupo kiongozi anayewapa wageni fursa ya uchumi wa nchi, basi hafai"

Tunataka pato la nchi liwarejee wanyewe wananchi. Mheshimiwa hii nimenukuu lakini kuna kifungu chengine.

> "Kama tulivyoupindua usultani sasa tunaupindua ubeberu mtu mmoja kuwa na heka 3,000 peke yake na watu wengine wakawa hawana kitu hapa kwetu, mpango huo basi"

Mhe. Mwenyekiti, kweli lakini kuna watu wana heka 9 wana heka 27, humu ndani nafikiria wengine hata heka 3 hawana. Mimi naomba sana tuwe *serious* kwa sababu mara nyingi nina *experience* na Kamati hizi tunakuwa hatupo *serious*, kazi yetu sisi humu Wajumbe kutafuta mambo kuweka sawa ili serikali iende vizuri hatimae majibu yake yanaingia kwenye *briefcase*. Ndio maana nikasema kuwa tutafute sheria ya kuzipa meno Kamati.

Leo Kamati Teule imeshasema maneno mazuri sana yanayokwenda hatua kwa hatua, mtu baada ya mtu, karatasi baada ya karatasi, hatimae akishakufanya *presentation* Mheshimiwa, tunakuwa haki ya utekelezaji hatuipati. Ndio maana nikasema tunamuomba mwanasheria kwa kuwa tumesomeshwa jinsi gani Mjumbe anaweza akaweka Mswada ambao utakuwa sheria na ukausaidia serikali. Tunaomba tupewe fursa hiyo sasa na sisi tulete sheria hizo, ili kuifahamisha serikali. Sio serikali sasa itupe sisi tu Miswada. Ili kulinda Kamati zetu ziweze kuonekana utendaji wake kwa umahiri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza kuingia migogoro yenyewe kwa kweli waziri wangu, maalimu wangu, kaka angu, nimpe pole sana. Tena basi, bado unao wadudu ndani ya Wizara yenyewe, bure tu hii, yatakupa tabu sana. Kama hukuondoa haya, hukuondoa huruma, Mheshimiwa watakuweka pahala pabaya sana hawa. Sijui wanakufanyia kwa kukukomoa au sijui kwa kuwa unafuata utaratibu. Maana utaratibu uliokuwa nao sasahivi mimi nimeukubali kabisa. Sasa unawaita wale wenyewe na unawakabidhi wenyewe mkononi. Utaratibu ni mzuri sana ndio inavyotakiwa. Umefanya ushujaa, umefuta maeneo yote na umeyarejesha serikalini, ni mtu wa kupigiwa mfano mkubwa sana.

Mpaka sasa hivi kwenye darubini yangu sijakusikia hata pahali pamoja ukiuza eneo la ardhi. Mhe. Waziri *Inshaalla* Mwenyezi Mungu akulinde pamoja na Katibu na Naibu Katibu wako, uzi huo huo, yarejeshe serikalini maeneo yote yenye mgogoro. Serikali itaamua nani wa kumpa. Wawekezaji wapo wengi tu wanataka. Wananchi wapo wengi tena wenye uwezo, wanahitaji ardhi. Nitatoa mfano kama huyu mwananchi wa Kampuni ya *SAGO* akiwa na mshirika wake. Hii kesi imeshahukumiwa, taarifa nilizozipata kwamba *SAGO* amesharejeshewa mali zake zote.

Ni kweli wamefutiwa kinyume na utaratibu, hakukuwa na *notes*, wala hakukuwa na indhari yoyote na tayari anaanza kwenda kulipa *ZIPA.* Naomba mumpe mashirikiano mazuri sana tuendeleze kuwa nae mfadhili huyu kwa sababu ni mtu mzuri na analipa kodi vizuri sana. Ingawa wao wamefutiwa lakini bado walikuwa wanapeleka pesa zao kwenda kulipa kodi ya ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kuna mambo mengine yalisahaulika, naomba niisaidie Kamati. Nilisema mimi ni katika ambao tulikuwa tukipiga kelele sana, nilizungumzia suala la Shakani na hata Mwanasheria wangu aliniita akanambia, Mheshimiwa wewe ulikuwa hulijui lile suala ulilizungumzia katika upande mmoja. Lakini kwa bahati nzuri nilipokwenda nikakaa kitako na yeye akanambia kuwa kumbe kuna Tume ambazo zilikuwa tayari zimeundwa za kushughulikia mzozo wa Shakani mwaka huu wa 2003. Kuna Tume vile vile imeundwa ambayo ni Tume Maalum ya kushughulikia Shakani vile vile ya mwaka huo 2003. Maraisi mbali mbali hao mpaka kumalizia raisi mwenyewe mstaafu Dr.Amani Abeid Karume mpaka kufikia leo na hakuna suluhisho lolote. Humu sikuona lakini wala siwezi kuwalaumu hata siku moja. Yote yalikubalika kua wananchi warejeshewe, aidha serikali inunue eneo wawalipe wale ambao wamepewa kinyume na utaratibu. Lakini suala hili mpaka leo lina utata na wananchi wanadhalilishwa bado.

Ningeomba hili Mhe. Waziri, kwa pamoja na kuwa halimo lakini naomba ulipokee kwa kuwasaidia wananchi wa Shakani. Twende na suluhisho, ripoti na ramani zipo zitakusaidia, hizi hapa. Nimekuwa Mzee Ali wa pili (*Professor*) hizi humu ramani zipo za miaka mingi, ili wananchi waweze kusaidiwa. Naomba sana Mhe.Waziri, Katibu na Naibu Katibu wako ili suala hili lifanyiwe haraka sana yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, nimpe pongezi sana Mhe. Hamza Hassan Juma, nimwambie ni shujaa sana. Na katika kazi hizi unatakiwa usiwe moga, utachekwa, utalaaniwa, utazomewa, lakini wewe usijali, jali lile la wengi. Sisi tunatetea umma hapa, hatumtetei mtu mmoja. Hata na mimi vile vile sijali kabisa nimejitolea muhanga, mbele ya umma. Siwezi nikakaa hali kama hii kupoteza fedha chungumzima mimi nikawaachia watu.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 16, amezungumziwa huyu jamaa Bruno, mimi ningeomba sana huyu Bruno, kwa kuwa kamati imesema hata lile *file* halipo ni kitu cha kushangaza sana. Ina maana hata hiyo ofisi haina kumbukumbu. Lakini ni kweli, mimi nina ushahidi mmoja tosha niuseme. Hata Mhe. Waziri, wa sasahivi alitaka kitu kama hicho akakikosa, huyo hapo Mhe. Waziri, anikatalie. Watu wanaficha *files* au mtu anakwenda kuandika tarehe pale anapobanwa na anaandika tarehe ya nyuma kumbe anajisahau kama zile tarehe zina utaratibu wake wa kuzipanga kinyume chake anafanya manyago. Mhe. Waziri, jitahadhari sana tena sana, usikubali kuyumbishwa kama hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, tunasema kwa unyonge, Bw. Bruno kala hasara sana, tumuonee huruma, arudishiwe ardhi yake ili atuletee maendeleo. Vijana wa Kizanzibari pale wamekosa ajira. Serikali yetu imekosa mapato, alikuwa akilipa pesa chungumzima za kodi. Naomba sana serikali itakapokuja kutoa jibu kwa sababu watu wanatusikia, imeshaonyeshwa *statement* ambayo kwa mujibu wa sheria hata kama mimi ningekuwa Jaji basi ningehukumu apewe mwenyewe kwa sababu *file* lenyewe halionekani. Tunaomba Mheshimiwa arejeshewe, mara moja, popote alipo.

Mhe. Mwenyekiti, nende katika matatizo ya eneo la Matemwe. Naomba sana Mhe. Waziri, wa Ardhi hebu tufanye ziara mimi na wewe Matemwe kwa makusudi, tena tulikuwa tayari mimi na wewe tufanye safari hiyo. Sio Italia, Italia tutakwenda baadae mimi na yeye. Twende nikakuoneshe kule manyago. Mheshimiwa wangu wewe hata ukivaa miwani huoni, lakini sisi tunaona. Naomba sana siku hiyo twende nikakuoneshe, bado uporo upo kule Matemwe. Watu wananyang'anywa hivi hivi. Sasa leo wale waliouziwa maneno kama alivyosema Mzee wangu, *Professor* wangu Mzee Ali Mzee hatari! sasa watu wakadai pesa zao? Sijui zitapatikana wapi.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja mimi nilikwenda Kizimkazi kule nikaangalia mradi wa *SAGO* ambao umepewa *Coconut*. Wakati ule nilikuwa mimi mwenyekiti wa Kamati. Tulikwenda kule tukaangalia, lakini hali tuliyoikuta yule mtu amelishwa hasara, alikuwa tayari ameshaanza kuchimba visima na kuwekeza na kutia zile *polls* za *concrete*, amefika pahali sasa hivi ameondokwa na imani hiyo. Wakati huo nilikuwa nikilisema ilikuwa bado hajakwenda Mahakamani. Baada ya muda alipoona hapati suluhisho lolote ndio akaingia Mahakamani. Kizimkazi ana maeneo mawili; moja ameshafika *foundation* ameshajaza kila kitu, anataka kuinua watu wamekula pesa.

Mhe. Waziri, nimshukuru sana Mkurugenzi wako wa upimaji kwanza nataka nikwambie hilo na kama hayupo mpe salamu. Hakubali siku hizi ukimwambia kapime na ndio mchezo uliokuwa ukichezwa hapo kabla. Ndio maana mkawa mnapima pahali viwanja vikawa vina hati tatu. Mama angu mwanamke. Ninao ushahidi juu ya hilo. Ndio maana tatizo hilo nampa tahadhari sana Mheshimiwa. Mhe. Waziri umejitahidi kufuta lakini wamekupiga changa la macho wamekudanganya waliokuletea.

Kuna kiwanja 547 hicho hawakukuletea kwa makusudi, wamekuficha, hivyo ulivyovifuta sawa sawa, lakini wamekukosesha 343 mtu huyo huyo mmoja, lakini kina hati tatu, 547 mtu huyo huyo mmoja lakini kina watu watatu. Sasa hivi vyengine hawakukupa. Kuwa mkali, naomba sana Mheshimiwa wangu. Amekwambia hapa mzee wangu Mhe. Ali Mzee Ali, una historia nzuri katika Baraza hili na ni kweli. Mimi nakukumbuka hadi kufika leo hii Mwenyezi Mungu akuzidishie, mpaka utakufa kwenda kaburini, hutokuwa na historia mbaya hata siku moja.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, nimezaliwa tokea 1961 mpaka sasa hivi nina miaka mingapi. Sasa hivi vinaingia vipindi viwili katika Baraza hili, lakini ukijichezesha na ukiwakubalia hawa watu watakutia kasoro. Mheshimiwa lakini siwaoni juu watendaji wako wameingia mitini wapo kidogo, nalo hilo tatizo. Sogeeni mbele hatuwaoni, mnaogopa nini, basi msifanye manyago kama mnaogopa. Tulimuona asubuhi Katibu na Naibu Katibu wake, lakini sasa hivi siwaoni sijui wako wapi.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 15, mgogoro baina ya muwekezaji wa *Sunset Paradise Resort* na *Sea Cliff* ya Mangapwani. Sasa hivi huyu bwana kule anaongeza matatizo juu ya matatizo, ambae mmemkodisha ardhi. Naomba sana Mheshimiwa ukatembelee huko, tuna wananchi wetu walikuwa wanafanya miradi yao sasa hivi wanaondoshwa katika maeneo hayo, kimafamba bila ya utaratibu, bila ya kuwalainisha, haya ndiyo matatizo yanayotukuta.

Suala la Bambi Mheshimiwa tulitumia nguvu kubwa hatukutumia siasa ya kuwafahamisha wale watu wakafahamu! hakuna mtu asiyetaka maendeleo. Laiti ingelikuwa watu wa Bambi wameelimishwa, wangelifikia mahali pazuri. Hebu twendeni tukaongee nao vizuri, watafahamu wale wazee wetu. *Ishallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu watafahamu nini kinachotakiwa kufanywa kwenye serikali yao na kuweza kuwasaidia. Lakini wao walijisikia unyonge waliona tulinyimwa sehemu ya ukulima, sehemu ya ufugaji ambayo hii ni kubwa sana. Nashukuru sana Katibu namuona yule pale, Mwenyezi Mungu amzidishie, kasikia wito wetu na hivyo ndio tunavyotaka awe *attendant* vizuri. Najua pengine binaadamu gari yake ilipata pancha.

Mimi naomba sana Mhe. Waziri, endelea kuuweka wazi mlango wako wa ofisi, ili Wawakilishi wote wapate kuja kukupa ushauri na kuweza kukuelekeza vizuri. Kama nilivyosema Wizara yako hili ni kubwa sana, lazima upate washauri wazuri. Mimi naamini Wawakilishi wote hawa ni watu wazuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo sasa nataka nitoe ushauri wangu. Pamoja na utaratibu aliwokuwa nao Mhe. Waziri ningemuomba sana akajigawa sasa na Wizara yake na watendaji wake. Si vibaya akaanza ngaazi ya Wilaya hadi Mkoa. Haidhuru Mhe. Rais ameweka sawa, amesema kuwa matatizo ya ardhi yamalizwe na watu wa Mkoa na Wilaya sawa lakini hawana sheria wale mwenye sheria ni yeye waziri tu. Wajitahidi vya kujitahidi lakini wakifika pahali waseme *stop*. Ili kwa kurahisisha hili jambo kwa kupiga *block* masuala haya yasitokezee tena, lazima Mhe. Waziri awe na timu yake ndani ya Wilaya na Mkoa ili aweze kupata ripoti ya uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, na wale wapimaji sasa hivi wasende tu bila ya kupata ushauri na kwenda kwa Mkuu wa Wilaya, hivyo ndio tutaweza kuondoa tatizo mara moja, hakuna mchawi kwa hilo. Lakini mkitoka tu bila ya ushauri wa Mkuu wa Wilaya au Mkoa, anakwenda kuonewa mwananchi tu. Naomba ushauri wangu huo uzingatiwe.

Mhe. Mwenyekiti, pili ushauri wangu naomba na Wawakilishi nao muwashirikishe kwa namna moja au kwa namna nyengine, kivipi basi. Ukiwa na Kamati yako kama ya Wilaya au Mkoa lazima na Wawakilishi nawao washirikishwe. *Wallahi* Mheshimiwa wangu utaona raha kabisa, kwa sababu sisi ndio wenye wananchi na ndio wenye maeneo. Nimalizie Mheshimiwa kwa kutoa tahadhari dakika zangu za mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mwananchi wangu anaitwa Haji Juma, nafasi yake imepimwa, tena kapeleka ombi yeye sehemu ameshapanda midimu, na mazao

mengineyo sasa hivi watu wananufaika nayo eyo, chakushangaza kenda kapimiwa mtu mwengine na maafisa wako waliopita kwani hawa wa sasa hivi wako makini wasingekubali upuuzi huo. Naomba Mheshimiwa tumsaidie huyu mtu, lile eneo ni lake anatilisha huruma. Mheshimiwa njoo kule ukaone Kiwengwa.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, wamenituma wanachi wangu wa Kiwengwa Kairo, wemenambia kama mtu kapewa ule uwanja wao kinyume na utaratibu na pesa keshakula, akazirejeshe pesa uwanja hawautoi ng'ooo! Hilo wamesema wazi. Na mimi nawaunga mkono kwa sababu ni Mwakilishi wao itakavyokuwa vyovyote na mimi sikubaliani nalo. Watafika wenyewe wanapotaka kwani hii ndio mali yao tumesema humu. Mhe. Ali Mzee Ali, amenukuu maneno aliyoyasema Hayati Mzee Abeid Amani Karume, urithi wenyewe ndio huo, mali zirejeshwe kwa wenyewe wananchi, tumpe tunayemtaka sisi wenyewe tusilazimishwe. Wananchi wangu wapewe wenyewe watengeneze uwanja wa Mshimba *National Stadium,* uwe wa mpira watu waje wacheze kule.

Tunaomba sana Mheshimiwa hilo na lile eneo la *double location* tumekubaliana na wewe tunalifuta, keshokutwa nikuoneshe skuli ipo pale nzuri ya ghorofa ili tufike wakati tunaotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kwa kunivumilia kwa muda wote. Ahsante sana naunga Mkono ripoti mia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tujitahidi twende katika hadidu rejea zilizowasilishwa hapa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia *report* hii adhimu iliyowasilishwa na Mzee wetu, *Alhajj* Mhe. Ali Mzee Ali. Kwanza ameanza kutoa angalizo ili turudi katika hadidu rejea. Mheshimiwa katika watu ambao walizungumza sana migogoro ya ardhi basi nilikuwa mimi ni mmoja wao. Ushahidi ni *report* hii, haya ni sehemu tu ambayo niliyozungumza kuhusu malalamiko ya ardhi kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu uturidhie kidogo tumkumbushe Mhe. Waziri ili apate nafasi, ukiacha hii *report*, lakini aweze kuyafanyia kazi matatizo mengine ya ziada, vyenginevyo itabidi tukishakumaliza *report* hii sasa tuje tujenge hoja nyengine ya kuunda Kamati nyengine ya kumalizia ile migogoro iliyobakia. Nafikiri itakuwa si jambo la busara sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nianze na kumsaidia Mhe. Waziri, kwa vile viporo ambavyo mwenzangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, alisema kwamba vipo Mhe. Waziri, ambavyo Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hakuwaza kuviona. Nitaomba sana Mhe. Mwenyekiti, ili atusikilize hoja zetu kwa sababu baadae anatakiwa aje atoe ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza katika maeneo ambayo nilizungumza ni suala la ulipaji wa fidia wa watu wa Mchangamle. Suala hili katika *report* halikujitokeza. Nitamuomba sana Mhe. Waziri, kama alivyoshauri Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, nije nimkabidhi wale wananchi wa Mchangamle ili akaenao, awasikilize ile kadhia yao na ni ndogo tu, ili kuweza kukaa nao na kuangalia utaratibu wakuweza kuwamalizia fidia zao. Hata yule muwekezaji anashangaa ile fedha aliyotoa na ile waliyopewa wananchi. Sasa mambo kama haya kwakweli hayatuletei taswira nzuri nchini petu. Hili nilikuwa naomba Mheshimiwa katika kiporo vyake hili aliweke na tuje kulifanyia kazi baadaye.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile nilipendekeza katika *report* yangu nilipochangia katika eneo la Kwale. Eneo hili naona hawakuwahi kwenda Kamati sijui kutokana na muda. Na mimi nilipendekeza vile vile tungeshirikiana kwa pamoja tukenda kuangalia lile eneo. Sasa labda akija atatueleza sababu gani iliyowafanya kushindwa kulishughulikia eneo la Kwale.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kiporo chengine Nungwi. Huko kuna viporo viwili ambavyo nilivizungumza. Nilisema kuna eneo moja alikuja muwekezaji akafutiwa katika njia ambazo hazieleweki, lakini baadae eneo lile lile badala ya kurudi serikalini watu waligawana mapande na liko katika mnada linauzwa mpaka hivi sasa, sijui kama mnunuzi keshapatikana. Hiki kiporo naomba Mhe. Waziri, ukichukue ili tushirikiane na wewe eneo hili ulirejeshe serikalini.

Mheshimiwa, mimi nimeridhishwa sana na utaratibu wako wa sasa hivi ambao Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ameuzungumza. Maeneo mengi ambayo yalikuwa yanalalamikiwa na yale ambayo yalikuwa yamewekwa makuta ambayo hakuna uwekezaji. Maeneo mengi ambayo yamezuiliwa na watu kwa tamaa ya fisi kutafuta washtiri, ambapo wanakuja wawekezaji serikalini wanaambiwa maeneo hakuna wanaondoka, kumbe watu maeneo wameyakalia, umeyarejesha serikalini.

Sasa katika kiporo hiki cha Nugwi naomba Mheshimiwa, tukurejeshee tena mikononi mwako ili sasa aje huyu muwekezaji ambaye ataweza kuja kuwekeza bila ya matatizo yoyote.

Vile vile, niliwahi kuzungumzia eneo hilo hilo la Nungwi ambalo kuna wananchi, wazee wangu ambao walitufuata hapa Barazani. Baada ya kusikia kwamba sasa hivi Wawakilishi wao tumechachamaa katika kushughulikia migogoro ya ardhi. Walikuja, tukazungumza nao na kwa kweli eneo lao hili Mhe. Mkuu wa Mkoa na Mhe. Mkuu wa Wilaya ambapo Kamati yangu iliwahi kukutana nao yuko pamoja na wananchi hawa wa Mkoa wa Kaskazini, na eneo lao Mheshimiwa lina hati. Lakini mpaka leo serikali wanashindwa kwenda kuwapimia ili wakapata ile *Site plan* ili kuweza kuendeleza katika uwekezaji, na kiporo hichi namuomba sana Mhe. Waziri, ni vizuri aje kukishughulikia.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kiporo chengine ni cha jimbo lako mwenyewe ambapo leo najua mate yakutoka hupati kuchangia. Sasa mimi nachangia kwa niaba yako. Kuna kiporo tulichokizungumza ambapo Kamati yangu kupitia Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa upande wa Mazingira tulitembelea eneo la Kikwajuni. Eneo ambalo wananchi walitaka kufanya mradi wa maendeleo wa uhifadhi wa mazingira, lakini wameshindwa kulitumia eneo lile kwa sababu kuna hati ambayo imetoka, sisi tunasema kinyemela kwa sababu mpaka leo hatukuweza kupata utaratibu wa hati ile. Na hili nilikuwa naomba katika hivyo viporo nikumbushie. Sasa narudi katika hoja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme naipongeza sana Kamati, na Waswahili wanasema kimya kingi kinamshindo. Miongoni mwa watu ambao nilikuwa nalaumu Kamati hii inashindwa kufikisha *report* yake kwa wakati nilikuwa ni mimi. Kila kitu kina ladha yake, kitu kikishakuwa kiporo tena ile ladha inapungua. Sasa masuala ya ardhi tumeyazungumza sana na mimi nilikuwa katika miongoni mwa hao Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ambao *report* yake Mhe. Ali Mzee Ali, amei - *quote* kupitia kwenye vyombo vya habari, katika maazimia tuliyoyatoa na mimi nilikuwemo.

Sasa leo haiwezekani maagizo ya Chama cha Mapinduzi, yanatolewa yanaambiwa ya serikali na leo serikali wakati mwengine ilikuwa inashindwa kutuchukua hatua kwa sababu huku Baraza la Wawakilishi limeunda Kamati. Sasa mimi nadhani wakati umefika sasa Mhe. Waziri, umeshapata nafasi umeshapata baraka zote, Chama cha Mapinduzi Zanzibar kupitia kwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar Ndugu Vuai Ali Vuai alikukabidhi kazi ya kushughulikia migogoro ya ardhi kupitia kwenye kamati maalum, Baraza la Wawakilishi limeunda Tume kukusaidia kazi hiyo, sasa imeshakamilishwa Mhe. Waziri, tunakuomba uchukulie hatua haya mambo yote ambayo yalichukuliwa.

Kwanza mimi Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na ripoti hii yote kama ilivyo, na kwa kuwa nakubaliana na ripoti hii Mhe. Mwenyekiti, hapa ndio pale

ninaposema kwamba yale ambayo tunayozungumza hapa Barazani Mhe. Mwenyekiti, sio maneno ya kubuni, sio maneno ya kumuonea mtu au labda tuna chuki na mtu. Mhe. Mwenyekiti, katika majimbo ukishachaguliwa kama Mwakilishi wa Jimbo, mfano mimi Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura, siku ambayo niliyolishwa kiapo hapa nikakamatishwa msahafu, majukumu yangu kuitumikia Zanzibar nzima.

Kama wananchi wa Jimbo la Kwamtipura wangekuwa na mgogoro wa ardhi ningeliuleta, lakini kwa bahati jimbo langu liko mjini hata hiyo sehemu ya kulima hatuna, kwa hivyo wananchi wengine wenye nia njema wameniletea malalamiko yao ndio nikawasilisha Barazani. Na ninashukuru kwa kila kielelezo nilichokileta Mhe. Mwenyekiti, kamati ilipofuatilia kielelezo kile kilikuwa ni halali na cha kweli.Kwa hivyo, kweli niliweza kufanya ile kazi ya wananchi na kuweza kufanya utafiti na leo ripoti hii inathibitishwa.

Kwa hivyo, yale ambayo niliyopendekeza mimi, nashukuru Kamati imeyapendekeza yale yale. Sasa Mhe. Waziri, katika utekelezaji wa mambo haya kama unavyojua, mambo haya Mhe. Mwenyekiti, ndio sisi kwa sisi, na ninajua unapata tabu sana hivi sasa kila unaposoma maazimio ya Kamati unapata tabu kwa sababu aidha utanitonesha mimi au utamtonesha Mwenyekiti au utamtonesha swahibu wako, lakini sasa hii ndio ngome ya wananchi ambayo ngome hii aliianzisha Mhe. Aboud Jumbe, ambao Mhe. Mwenyekiti, aliisoma hapa. Mimi nilikuwa nataka niseme kwamba katika viongozi ambao waliweka historia ya utawala bora, watu wanasifu watu wa nje tu, Mandela kasifiwa sana lakini na sisi lazima tusifu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika viongozi walioweka demokrasia katika nchi zao walipopewa nafasi na wananchi kuongoza ni Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi. Mhe. Mwenyekiti Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, alikuwa Rais wa Zanzibar na yeye baada ya Mapinduzi alianza Mzee Karume baada ya kufariki, alipokabidhiwa madaraka yale alikuwa nguvu za kutunga sheria anazo yeye, kwa sababu yeye ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nguvu ya kusimamia utekelezaji alikuwa nazo yeye, lakini binafsi yake akaona haiwezekani kwamba yeye awe ndio mpikaji halafu yeye ndio akawa mpakuaji.

Aliamua kuunda chombo cha Baraza la Wawakilishi na akasema hii ndio ngome ya wananchi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ingelikuwa Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, kaunda Baraza la Wawakilishi wakati anajiuzulu, pale tungesema kwamba kwa kuwa yeye alikuwa keshamaliza kazi yake anataka kumwachia sokomoko anayekuja. Kwa bahati yeye alikuwa bado yuko kwenye kiti nguvu zote alikuwa nazo yeye lakini akaunda chombo ambacho kitakachomsimamia katika kutekeleza majukumu yake.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti katika viongozi ambao wanatakiwa walindwe, wanatakiwa waheshimiwe katika historia na utawala bora katika nchi hii ni Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, Mungu ampe maisha marefu, Mungu ampe uzima, na ninaamini huko aliko sasa hivi anatusikia vijana wake ambao Baraza hili kalitunga yeye na hii ngome sasa hivi inafanya kazi yake.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika mchango wangu nataka na yeye nimuingize katika vitabu vya historia Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Ali Mzee Ali, yeye ni hodari sana wa kueleza mambo ya historia humu, katika kitabu hiki mimi kwa kweli hiki nakwenda kukihifadhi nitakuja kuwapa na watoto wangu.

Mhe. Mwenyekiti, ameonesha kwamba Kamati yake imefanya *research* ya kutosha, sisi tulimpa migogoro hii ya miaka ya 1990 mpaka mwaka 2010, lakini yeye alikwenda *deep* zaidi katuanzia historia tangu mwaka 1933 ambapo sisi wengine wala hatujui kama tungelizaliwa siku hizo. Kwa hivyo, na akasema kwamba katika 29/8/1955 Sir. John Grey alipewa kazi ya kushughulikia mgogoro wa ardhi, kwa hivyo na yeye tunamuingiza katika kumbukumbu katika 2012, 2013 na yeye vile vile kwa hivyo katika vitabu vya kumbukumbu baada ya Sir John Grey, sasa hivi anakuja Sir. Ali Mzee Ali ambaye alikabidhiwa jukumu hili na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, hii ni kuonesha kwamba hii migogoro ya ardhi ni kitu ambacho kinatakiwa kishughulikiwe, na kwa kweli utaratibu kama nilivyosema aliouanzisha sasa hivi Mhe. Waziri, kwanza kufanya uhakiki wa ardhi. Mheshimiwa, katika kitu ambacho umeamua kukifanya kwa uadilifu mkubwa sana ni uhakiki wa ardhi. Kwa sababu kama tunavyoambiwa kwamba ardhi ni mali ya serikali, lakini siku zote Mheshimiwa yuko wapi mzee wangu sasa hivi Mhe. Mohammed Khalid, anasema ardhi ya Zanzibar ni mali ya serikali lakini wananchi wa Zanzibar wanamiliki ardhi kwa sababu serikali ni mali ya wananchi vile vile. Sasa huu uhakiki wa ardhi Mheshimiwa utaweza kuondoa kabisa hiyo migogoro ya ardhi iliyokuwepo.

Sasa ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti, baada ya huu uhakiki wa ardhi ikishatambulikana zile ardhi basi zipimwe ili wale wananchi waweze kupewa hati zao ili kuja kuondoa hii *duplication* ya kutoa hati eneo moja mara mbili mara tatu. Sasa mwananchi kama eneo lake limehakikiwa ana hati yake hata anapotaka kuingia ubia au kufanya jambo lolote jengine atakuwa yuko huru na zile *document* zitakuwa ziko wazi vile vile zitakuwa hazina matatizo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli huu ulikuwa ushauri wangu kwa Mhe. Waziri, vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niendelee katika suala zima la maoni na mapendekezo ya Kamati. Mhe. Mwenyekiti, humu kamati haikupendekeza moja kwa moja wakamrusha paka tu uwanjani, haikupendekeza moja kwa moja kwamba hili lifutwe, hili lirudishwe, huyu anyang'anywe, huyu afanye nini, wamerudi wanasema taratibu za kisheria zifuate. Lakini sasa bado katika sheria zetu zina mapungufu.

Kwa sababu leo amezungumzia zaidi kufata sheria za ardhi na sheria ya ardhi haizungumzii mtu anayetumikia madaraka yake vibaya. Sasa je, Mhe. Mwenyekiti, ukija utwambie, je, baada ya kufuata hii sheria ya ardhi iwe imetosha kwa watu waliotumia madaraka yao vibaya hatua gani za kisheria zichukuliwe, Mhe. Mwenyekiti lazima tupate maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la migogoro ya ardhi, Mheshimiwa migogoro mingi tuliyoizungumza hapa serikalini ipo na inajulikana. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ina kitengo cha Uratibu wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, kitengo kile kinashughulikia vile vile uratibu wa shughuli zote pamoja na matatizo ya wananchi. Mheshimiwa, ukienda katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kweli migogoro ya ardhi ipo mingi, na alianza jitihada yeye mwenyewe kuanza kuishughulikia, lakini alipoona kila akichungulia tumo sisi kwa sisi inaonesha na yeye yalimshinda. Kwa hivyo, kwa kuwa yalimshinda Mhe. Mwenyekiti, ameamua kunyamaza kimya.Kwa hivyo, na sisi ngome ya wananchi tukaamua kuyachukua tumeyafanyia kazi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nategemea ripoti hii Mhe. Waziri, ambaye yeye ndiye atakayekuwa na jukumu kubwa la kuitekeleza na nguvu ya sheria aliyopewa ya kufuta na kutoa ninaamini sheria hii au ripoti hii ataweza kuitekeleza, na kwa kuwa si muda mrefu tutakuwa na ripoti za kamati hatuwezi tukayarejea tena haya lakini tunaamini wakati wa bajeti tutakapokuwa tumekuja kujadili bajeti ya serikali, kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati tutakuja kuangalia Mhe. Waziri ameitekeleza vipi ripoti hii ya Sir. Ali Mzee.

Mhe. Mwenyekiti, sasa suala la kufutwa ukiangalia Mheshimiwa migogoro mingi ambayo ilihusika ilikuwa ni kufutwa maeneo bila ya kufuata utaratibu na sheria. Ninashukuru Kamati imejaribu kufuatilia *document* zile na ile sheria ambayo inayozungumzia suala la kunyang'anywa mtu ardhi kupewa notisi ya miezi mitatu halikufanyika, na limefanyika katika maeneo mengi ambayo katika ripoti hii imejieleza sitaki kuyarejea.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala moja, hivi karibuni kwa bahati nilipata nafasi ya kusafiri na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tulikwenda Marekani katika mji maarufu sana wa uwekezaji wa biashara mji wa *Seattle*

kule Marekani. Mhe. Mwenyekiti Mhe. Balozi, alipata kuzungumza na *African Chamber of Commerce* ya pale *Seattle*, lakini vile vile, alipata *forum* ya wale matajiri wakubwa ambao wana-*donate* katika hizi *rotary club* na moja katika wale wawekezaji walipokuwa wakizungumza na Balozi kuangalia mazingira kuja kuwekeza Zanzibar, Mhe. Mwenyekiti, ni suala la uadilifu na suala la uaminifu. Na kila wakati walikuwa wanataka *commitment* ya serikali, wanauliza, je, *commitment* ya serikali tukija kuwekeza. Je, sheria ziko wazi kiasi gani.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, wenzetu hawa wakija wakisoma ripoti kama hizi kwa kweli sitegemei kama kuna Mmarekani *investor* atakuja kuwekeza Zanzibar kwa utaratibu huu ambao tunautumia sasa hivi. Na kwa bahati nzuri Mhe. Mwenyekiti, wale wenzetu ni wakweli sana. Marekani wenzetu kuna fedha za kutosha, kuna taasisi za fedha ambazo wanaweza wakatoa fedha zote unazozitaka lakini ikiwa mradi wako umeweza kuuelezea vizuri.

Sasa wenzetu hawa Mhe. Mwenyekiti, mambo kama haya nadhani Mhe. Waziri, ujitahidi ndani ya kipindi hiki kilichobakia ujitahidi kuweka sawa, sheria ziwe sawa, ziwe wazi kabisa, naamini wawekezaji wengi watakuja kuwekeza kwa upande wa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile, katika hii migogoro nilizungumzia suala zima la wale wawekezaji ambao waliofutiwa maeneo ambao walikuwa wakilipa ada kubwa na baadae wale waliopewa wakawa wanalipa ada ndogo. Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa naomba sana kama ripoti hii ilivyoeleza kwamba ni lazima kuwe na mawasiliano ya karibu hasa kwa upande wa hizi *lease* zinazotoka. Kwa sababu wenzetu ZRB wao ndio wanaokusanya mapato.

Na ndio maana hapa kuna baadhi ya maeneo yalikwishafutwa lakini bado ZRB walikuwa wanapeleka *invoice* za kuweza kulipwa ile kodi ya ardhi na hao wawekezaji kodi ya ardhi walikuwa wanalipa. Sasa naomba sana katika yale maeneo ya *lease* yaliyotolewa, basi pale yanapofutwa basi zile taarifa ziende mpaka katika maeneo ya ukusanyaji wa mapato ili kusiwe na *duplication*. Kwa sababu huku kama leo serikali imeshafuta hati *ZRB* bado wanaendelea kupokea mapato. Kwa hivyo, ina maana kuna taasisi mbili za serikali zinagongana, ina maana hatujui kitu ambacho tunachokifanya. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana basi ripoti hii iweze kutusaidia kutuweka sawa baina ya taasisi zetu zote tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikiangalia ripoti hii ilieleza suala zima la ufungaji wa njia katika maeneo ya ufukweni. Lakini vile vile, na huku kamati yangu ilikwenda kule Mzuwardini ambao Mhe. Ali Mzee na Kamati yake walikwenda kuona. Lakini vile vile suala kama hili au kadhia kama hii

ilijitokeza katika mgogoro aliouleta Mhe. Khadija Kona katika eneo la Pwani mchangani. Mhe. Mwenyekiti, eneo hili wananchi wanalalamika kwamba eneo lao ambalo wanalitumia muwekezaji kapiga kuta wananchi wameshindwa pahala pa kupita.

Sasa eneo hili Mhe. Mwenyekiti, naliunganisha na eneo la Paje *Cristal Hotel*. Mheshimiwa mimi nitaendelea kulisema kwa sababu kwa kweli serikali inawanyanyasa wananchi wake. Na hapa kama alivyosema Mhe. Ali Mzee Ali, huku iliambiwa kwamba ni dhambi, lakini ingawa ripoti ile kwa sasa hivi imeshapitwa na wakati msemo ule kwamba ni dhambi kubwa kumpa mgeni akawekeza katika nchi na kumwacha mwenyeji.

Sasa hivi tupo katika sera za uwekezaji, biashara huru. Kwa hivyo, wawekezaji wanaruhusiwa kuwekeza, lakini isiwe sababu kwamba wawekezaji wanakuja kuwekeza Zanzibar matokeo yake baada ya kuwekeza walete neema kwa wananchi, wanakuja kuwanakamisha wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana eneo hili lililozungumziwa Pwani Mchangani Mhe. Waziri, alifuatilie; kama kuna njia ambayo wananchi walikuwa wakiitumia, kwa ajili ya shughuli zao hasa kwendea baharini na sehemu nyengine, hiyo njia iweze kufunguliwa ili waweze kupita pamoja na kule Mzuwardini. Lakini Mhe. Mwenyekiti, eneo hili naliunganisha na kiporo chengine cha eneo la *Cristal*.

Mhe. Mwenyekiti, eneo hili la Hoteli ya *Cristal* sisi hatulalamikii uwekezaji wa *Cristal, Cristal* uwekezaji umepata kibali cha *ZIPA*, tatizo lililojitokeza Mhe. Mwenyekiti, yule muwekezaji wa Hoteli ya *Cristal* kule Paje baada ya lile eneo alilopewa na *ZIPA* ameweza kuongeza eneo jengine na watendaji wako wabaya wa Wizara yako ya Ardhi wamekwenda kuliongeza eneo lile kinyume cha sheria.

Mhe.Mwenyekiti, sheria ya *ZIPA* inasemaje, mueekezaji yeyote anapokwenda kuomba eneo, lile eneo linatoka Ardhi, *ZIPA* ndio wanatoa kibali. Kwa hivyo, kama wanataka kutoa *extention* au kama anataka kuongeza mradi wake eneo lile lazima lirudi tena Ardhi lakini hiyo ardhi yenyewe kwa kupata *approval* ya *ZIPA.* Sasa haya maeneo mengine aliyopewa huyu muwekezaji wa Hoteli ya *Cristal* ambayo amepewa kinyume cha sheria, Mhe. Waziri, kwa mamlaka uliyokuwa nayo kama unavyowafutia wengine na huyu maeneo haya ukayafute ili wananchi waweze kuyatumia. Na Mhe. Mwenyekiti, hata kama baadae itakuja kuonekana kwamba eneo lake la uwekezaji liongezwe na kama *ZIPA* watakuja ku-*approve* basi yale maeneo ambayo wananchi wanayatumia kwa ajili ya njia maeneo yale ni *public uses* lazima yawe huru yaruhusiwe kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, na hili sio jipya, katika maeneo mengi hata sisi tunapopewa hivyo viwanja kunakuwa na *block* lazima kila baada ya *block* moja *block* ya pili kunawekwa njia ili watu waweze kupita. Sasa leo inakuwaje muwekezaji baada ya kupewa eneo halafu anaziba njia. Sasa hii Mhe. Mwenyekiti, eneo hili limetolewa kinyume cha sheria. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri, tukishamaliza ripoti hii naomba ulifuatilie eneo lile ukalifute, baadae kama anataka kuongeza eneo aombe tena Ardhi na *ZIPA* watoe kibali, lakini vile vile, ile ada yake ifanyiwe tathmini ili aweze kupima. Mimi sina tatizo na kupimiwa, mimi tatizo langu unyanyaswaji wa wananchi katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili vile vile kama tulivyosema kuna muwekezaji mzalendo ambaye leo zaidi ya mwaka wa 15 tokea eneo lile na yeye alipopewa hati na Wizara ya Ardhi ameshindwa kulitumia eneo lake kwa sababu amezingiwa na tajiri huyu wa Hoteli ya *Cristal* ambaye kwa maneno yake mwenyewe anasema serikali yote iko mkononi mwake, anasema Wakuu wa Mikoa wako mikononi kwake, Wakuu wa Wilaya wako mikononi kwake, watu wa Ardhi, Wakurugenzi wako mikononi kwake, Kamishna wa *ZIPA* anasema ndio kabisa kamkumbatia, mahkamani ndio anasema ndio kahamia.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi siamini kama Waziri wewe unaweza ukatiwa mkononi na tajiri yule. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hawa wengine walitiwa mkononi, kwa sababu mpaka leo hiyo kadhia imeshindwa kushughulikiwa. Sasa naomba sana na ninaamini Mhe. Waziri, wewe unateleza huingiii mikononi kwa mtu, naamini utaweza kuwatendea haki wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, najua unanitizama ninamalizia, nataka niseme kwamba lazima hapa tuwe na utaratibu mzuri hasa katika masuala ya matumizi bora ya ardhi. Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti imeeleza huku kuna watu walipewa maeneo, maeneo yale yale wamepewa watu kwa ajili ya kujenga, maeneo yale yale wanapewa watu kwa ajili ya kulima. Sasa leo inakuwaje. Serikali mimi nadhani na kama sasa Mhe. Waziri, tunashukuru jitihada yako kupitia Wizara yako inayoifanya kutafuta wawekezaji wa ujenzi wa nyumba ikiwemo *real estate* ambayo kule Marekani tumempata muwekezaji mmoja tayari hivi karibuni ataingia mkataba na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya kutoa fedha nyingi kwa ajili ya wananchi kujengewa nyumba za makaazi. Na hivi karibuni Mhe. Mwenyekiti, nasikia Mhe. Waziri, yuko mbioni lakini mbio za Mhe. Waziri, huyu tofauti na wengine mbio zake huwa zinakuwa zinafikia ukingoni. Maana mbio zake zinakwenda kwa mpango maalum, yuko mbioni kutuletea sheria ya kuanzisha Shirika la Nyumba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, kama Waziri yuko mbioni kuleta mswada wa sheria kuanzisha Shirika la Nyumba hiyo ndio sera nzuri ya utekelezaji wa yale maazimio ya Mapinduzi ya Zanzibar. Na katika waasisi kina Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, ndio wamo hao.Kwa hivyo, ndio tunaamini hii sheria ya Shirika la Nyumba hii sasa ndio pale tunaposema tuwe tuna *land use plan;* ambayo maeneo yatatengwa maeneo haya yatakuwa ni ya makaazi, maeneo haya ya kilimo na maeneo haya yatakuwa ya shughuli nyengine za biashara.

Sasa kwa kumalizia kabisa Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie suala la wananchi wa Bambi. Mhe. Mwenyekiti, naishukuru sana Kamati ya Ardhi ambayo iliyokuwa inaongozwa na *Sir* Ali Mzee. Mhe. Mwenyekiti baada ya kwenda kuwaona wananchi wa Bambi mimi Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa tulikwenda, kwa kweli wananchi walilalamika sana, sasa mimi bado nakubaliana na ushauri wa Wizara ambao kamati ilipozungumza nao wao walisema kutokana na hali eneo lile bora libakie na matumizi kama yalivyo.

Na kwa kuzingatia kwamba Mhe. Mwenyekiti, Bambi ya zamani sio Bambi ya sasa. Bambi ya zamani ilikuwa ukimchinja damu yake imeandikwa *Afro* Shirazi. Mhe. Mwenyekiti, kwa tunavyokwenda sasa hivi wananchi wa Bambi wamezaa sana na maeneo yale kwa kweli wanayatumia kwa ajili ya kilimo, na mwezi wa Ramadhani kama nilivyosema katika kipindi kilichopita kwamba tunakula viazi kutoka Matora, tunakula majimbi kutoka Matora na mazao mengi yanayotoka kule yanatusaidia kwa chakula mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Sasa maeneo yale Mhe. Mwenyekiti, yanawasaidia sana wananchi wale kuweza kupata fedha za kujikimu maisha yao, lakini vile vile kuwasomesha watoto wao. Sasa mimi bado naomba Mhe. Mwenyekiti, muwekezaji huyu anayetaka kuwekeza mradi wa ufugaji wa ng'ombe, na kwanza lile eneo tayari lina rutba ya kutosha. Kwa hivyo, bado mimi naamini maeneo makubwa tunayo Zanzibar, Wizara ya Kilimo ina maeneo makubwa mfano kama Pemba pale lile eneo la Chamanangwe, pale mimi nafikiri muwekezaji kama anataka kufuga ng'ombe wanaingia wengi sana pale.

Mhe. Mwenyekiti, bado naomba sana eneo lile wananchi wapewe nafasi waendelee kufanya shughuli zao za kilimo na ukiangalia asilimia karibu 75 ya wananchi wetu wa Zanzibar wanategemea kilimo, wakiwemo wananchi wa Bambi. Kwa hivyo, naamini kama mapendekezo ya Kamati Mhe. Waziri, atakubaliana nayo ili wananchi wetu yale malengo ya Mapinduzi kuwa wapewe eka tatu tatu kwa ajili ya kilimo mambo yale tuweze kuyaendeleza.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura ambao miongoni mwao asili yao wanatoka Bambi naiunga mkono hotuba hii ya Mhe. *Sir* Ali Mzee Ali, kwa asilimia mia moja, pamoja na ziada ya viporo niliyompa Mhe. Waziri, ninaamini tutashirikiana ataweza kufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi kuchangia ripoti hii. Pili, naipongeza kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa kufuatilia na kufanyia kazi matatizo mbali mbali ya migogoro ya ardhi katika maeneo tofauti. Naipongeza sana Kamati Teule ikiongozwa na Mwenyekiti Mhe. Ali Mzee Ali.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti imeeleza kila kitu na kwa kina kabisa kuhusu matatizo mbali mbali ambayo yamejitokeza na ambayo yamefanyiwa kazi na kamati hiyo. Jumla ya maeneo 21 yamefanyiwa kazi. Vile vile, vielelezo mbali mbali vimetolewa ambavyo vimeambatanishwa na ripoti hii. Huu ni ushahidi tosha kwa kadhia hizo. Pia, maelezo mbali mbali yametolewa na baadhi ya Waheshimiwa wa Baraza la Wawakilishi ambao wameibua hoja katika kamati na wametoa maelezo mbali mbali. Na baadhi ya wananchi pamoja na watendaji ambao wametoa taarifa zao mbele ya kamati hii ili kuipa uzito ripoti hii.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti hii sina cha kuongeza wala cha kupunguza, ripoti imejitosheleza lakini nilikuwa na ushauri tu kwa serikali, naiomba serikali ipitie ripoti hii kwa kina na uangalifu wa hali ya juu na kuifanyia kazi ipasavyo.

Pili, serikali ijiridhishe na ripoti hii kabla ya kutoa maamuzi ili kuona kwamba inatoa maamuzi ya haki na kwa usahihi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, na jengine serikali ihakikishe aliyekuwemo hatoki na asiyekuwemo haingii. Vile vile, naishauri Wizara tu, Kamati zikienda katika Wizara husika kutaka viambatanisho au vithibitisho ili viandike katika ripoti zake nilikuwa naiomba Wizara zitoe ushirikiano wa kutosha, kwa sababu katika ripoti hii kuna baadhi ya vielelezo au kadhia ambazo kamati haijapata vithibitisho vyovyote. Kwa hivyo, naiomba Wizara ihakikishe inatoa ushirikiano wa kutosha kwa kamati ambazo zinakwenda kufanya kazi ili irahisishe utekelezaji.

Na kwa vile viwanja ambavyo wawekezaji wamepewa au wananchi ambao hawajaviendeleza kwa muda wa miaka mingi, nashauri tu kwa serikali

viwanja hivyo wapewe wananchi wanyonge wakafanye shughuli zao za maendeleo. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nishukuru kabisa kupata fursa hii kuweza kuchangia hiyo Ripoti ya Ardhi na nianze kwa kuanza kutoa pongezi kwa Kamati iliyoongozwa somo yangu *comrade* Mzee wetu, Mzee anayeweza kuweka historia, anayeweza kuweka kumbukumbu Mhe. Ali Mzee Ali.

Mhe. Mwenyekiti, pongezi za dhati nizitoe baada ya kuangalia hali halisi ya ripoti yenyewe na mimi nishukuru katika ile kadhia ambayo nilikuwa nikizungumza ya ndugu yangu Ali Murad kwa namna kamati ilivyofanya kazi na ilivyowasilisha ripoti yake na kutoa maoni ya kutaka uamuzi ubatilishwe.

Imani yangu kama kamati ilivyofanya kazi basi kwa tunavyomuamini mzee wetu ambaye historia leo imetajwa kubwa sana na yeye ndiye aliyeanza tangu kufunguliwa kwa Baraza hili wakati wa Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, ni imani yangu kwamba yale mazuri mengi ambayo yamezungumzwa katika ripoti hii kwamba atafanya kwa haraka na kwa uadilifu mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, sababu ya kusema hivyo niamini kwamba Maalim Rama ni Alhajj na mimi nategemea mwakani kwenda Makka tukijaaliwa na nimekuwa ninajifunza mengi sana kutoka kwa wanazuoni na nimeanza kujiuliza mambo mengi sana ambao wamekuwa wanapata viongozi wengi wa nchi hii na hususan Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba sababu gani za msingi zinazopelekea baada ya kustaafu wengi Wawakilishi hali zao zinakuwa za mitihani mitihani.

Nina imani kwamba mengi yanakuwa yanatokezea kutokana na sababu ya msingi kwamba tunapoingia katika chombo hiki tunakula kiapo cha Mwenyezi Mungu kwa wale waislamu, na wale wakristo wanakula kiapo kutokana na dini yao kwa kukamata biblia. Sasa nimeanza kutanabahi kwamba yale mapungufu ambayo tunayafanya baada ya kula viapo ndio yanayotupeleka katika mazingira ambayo si mazuri. Sasa kwa mwalimu wangu ambaye najifunza ulamaa nina imani kwamba atajitahidi katika haya ili kuonesha zile kadhia za wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, wakati Mwenyekiti wa Kamati akifanya majumuisho leo amenipeleka mbali sana kwa kutaja ile hali halisi ya majukumu yetu kwa wananchi, pale alipokuwa akisema kwamba Baraza ni chombo cha kuwasaidia wananchi katika kuwatatulia matatizo yao. Lakini akasema tena kwamba utawala bora ndio chombo ambacho kinaweza kutufikisha katika

mazingira mazuri. Na akasema tena kuwa utawala wa sheria ndio haki ya msingi kwa wananchi wetu. Sasa maneno haya ni mazito sana, na kwa kweli kama tutajitahidi kuyafanyia kazi basi tusingefika pahala leo tukawa tunazungumzia haya matatizo ambayo yamejitokeza ya kadhia hizi ambazo kufikia pahala Baraza hili tukataka tuunde Kamati Teule.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, pia nilikuwa nikimsikiliza mwalimu wangu wa siasa Mhe. Hamza Hassan Juma, pale alipokuwa akisema kwamba kama hatukuwa makini basi Kamati hii Teule haitokuwa ya mwisho itabidi tuunde Kamati Teule mara kwa mara lakini suala ambalo kwa wakati tuliokuwa nao na kwa kiongozi ambaye Waziri tuliyekuwa naye hatutegemei kama hilo suala litaendelea.

Kwa nini niseme hivyo Mhe. Mwenyekiti, sababu ya kusema hivyo Mhe. Mwenyekiti, bado madudu ndani ya wizara hii yanaendelea. Mwenyekiti, alisema tupige mstari mwekundu kwa yale ya nyuma yaliyotokezea, sasa sijui haya mapya tutayafanya nini kama tutapiga mstari wa buluu au wa kijani atatwambia baadae wakati wa kuja kufanya majumuisho.

Mhe. Mwenyekiti, sababu ya kusema madudu yanaendelea mimi nitamuomba mzee wangu anipangie siku kuna watu nimpelekee, kuna wazee wa Nungwi ambao sikubahatika kuyazungumza mazungumzo yao na kutiwa katika hadidu rejea hii, ambao wana kipindi si chini ya miaka miwili, wameanza kuuza nyumba zao, viwanja, kufuatilia matatizo ya maeneo yao, lakini hadi leo danadana ndani ya Wizara imekuwa kubwa. Sasa imani yangu Mhe. Waziri, basi yatapokuja kufanywa majumuisho ataniambia hao watu nimpelekee lini ili awasikilize na aweze kutatua matatizo yao.

Matatizo yao yameshafika katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, yamefika katika Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na wakayafanyia kazi, matatizo yao yameshafika wizarani na wakapewa matumaini yaliyokuwa hayamaliziki. Sasa ndio pale ninaposema kwamba bado matatizo ya ardhi ukiachilia yale yaliyokumbwa na viongozi waliopita kuna mengine yanaendelea hadi sasa na kwa kweli yanawarejesha nyuma wananchi wetu.

Sio hilo tu, kuna tatizo liko Kitumba Wilaya ya Kati, kuna Afisa wa Ardhi Wilaya ya Kati anayeweza kwenda kutia *beacon* ndani ya mashamba ya watu na kuwaambia wananchi kwamba kuna utaratibu mpya wa kukata mashamba, kuangalia wale watu ambao mashamba yao yana eka nyingi. Malalamiko haya yuko mwananchi mmoja kule anaitwa Mzee Khalifa, ni imani yangu kwamba na yeye basi atanipangia siku au atanambia siku gani aende akamsikilize na akaangalie *beacon* ambazo ameziweka, yaliyokimbiwa ni makaburi tu, akiona

kaburi basi *beacon* anaweka upande anasema hili tuache, lakini maeneo mengine yaliyobakia yote kadhia inaendelea.

Sasa niseme kwamba niipongeze Kamati kwa kazi nzuri iliyofanya, jitihada imeonekana. Lakini imani yangu kwamba yale yote ambayo yamezungumzwa basi Mhe. Waziri, atayafanyia kazi kwa uadilifu kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, tumechoka kuwazungumza Mawaziri ndani ya Baraza, tumechoka kuwapigia kelele na kuwanyooshea vidole. Leo nilikuwa nasoma Gazeti la Nipashe la tarehe 10 ukurasa wa 4 kama sikosei, kuna maelezo ya Mhe. Waziri, Kiongozi Mstaafu, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, aliyokuwa akiwaelezea watendaji wake. Katika gazeti hilo amesema kwamba, yeye Shamsi Vuai Nahodha hatokubali kwenda kunyooshewa vidole ndani ya Bunge, atachokifanya ni kuwachukulia hatua wale ambao hawatofuata utaratibu wa kazi zao. Naomba na sisi tubadilike. Nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii kuweza kutoa machache katika Ripoti hii ya Kamati iliyoundwa ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii, lakini pia nikushukuru na wewe. Mhe. Mwenyekiti, nataka nichukue fursa hii kwa dhati kabisa na nimesimama hapa kwa niaba ya wananchi wote wa Wilaya ya Micheweni kwa namna moja au nyengine jinsi inavyowagusa ripoti hii. Sina budi kwanza kuiunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja, yale yote yaliyotolewa na Kamati basi namuomba Mhe. Waziri, ayashughulikie lakini pia ayafuatilie.

Kwani Mhe. Mwenyekiti, ukiiangalia ripoti hii kuna maeneo kadhaa ambayo wanafanyiwa hivi wananchi hawa na kwa asilimia kubwa ni watu walio katika hali ya umasikini. Sasa leo kwenda kumnyang'anya ardhi mtu masikini kwa shughuli ambazo si za kimsingi ni kumuonea na kumdhalilisha. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri, hatua za kisheria kama alivyosema Mwenyekiti aliposoma ripoti yake zichukuliwe mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli migogoro hii inayojitokeza na sababu ya migogoro yote hii kujitokeza ni baadhi ya viongozi kutumia madaraka yetu vibaya. Kwa sababu hatuwashirikishi wananchi, sisi tukishakuwa viongozi tuna maamuzi yetu wenyewe na hivi sivyo, lazima kwa namna moja au nyengine serikali inataka eneo lile kwa shughuli za serikali wajibu na hisani wale waliopo pale hata kama pana mali yao duni basi kwa kiasi fulani iwashirikishe ili na wao wawasikilize malalamiko yao.

Lakini serikali haifanyi hivyo na viongozi hawafanyi hivyo, wenye madaraka yao ni wao kwenda katika maeneo yale na kupima bila ya kujali wananchi wale shughuli zao wanazozifanya pale. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, namuomba haya masuala ayafuatilie.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa sina mchango mkubwa, lakini kwanza kuna swali moja na mimi nataka nilizungumze japo halimo kwenye ripoti hii. Mhe. Mwenyekiti, tunajua kwamba eneo la Mziwanda halimo kwenye ripoti hii lakini naomba nilitolee ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, eneo lile lilitolewa kihalali kama sheria inavyosema, lakini tatizo serikali haichunguzi huyu anayetaka eneo hili anakwenda kufanya shughuli gani. Lakini mtu akishataka eneo kwa ajili ya kuwadhalilisha tu wale waliopo basi apewe hatima yake hufanya mambo ya maajabu katika maeneo yale. Mhe. Mwenyekiti, Waziri tunamuomba hili eneo akalichunguze kwa undani panafanywa nini pale.

Mhe. Mwenyekiti, eneo lile ambalo limetolewa lilikuwa lina wakulima wasiopungua 82, wakulima hao masikini, wanyonge na familia kubwa zinazowaelemea wakaweza kuondoshwa pale kwa kupewa mtu yule. Hebu tukaangalieni tangu siku lililotolewa eneo hili panafanywa nini. Katika kupewa pale eneo lile ilikuwa kuna mambo ambayo walisema yatafanyika, walisema sijui kuna ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, mabata, hivyo atoke mtu huku aende akafuge ng'ombe kule, lakini pia wale waliopo pale hawaonekani kuwa wanafanya nini.

Kwa hivyo, badala ya kufanya shughuli hizi ni kinyume na hayo yaliyosemwa, sasa hivi imekuwa kama ni *guest*, na nyumba ile inakodishwa watu kwa kufanya shughuli ambazo ni kinyume na maadili ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, watu wanatoka huko wanakwenda katika nyumba ile wanafanya mambo ambayo hayana maana, kesho kutwa pale sisi tuna watoto wetu na wao watafuata mila na tamaduni zile zile. Lakini sio hilo tu, ikifika kipindi cha sherehe pale huwa kama pana kitu gani sijui, zogo, ghasia moja kwa moja zinazofanywa pale. Huo ndio ufugaji wa ng'ombe na mbuzi.

Jengine ni kuwa pale wanakata miti ya watu pengine wamepanda wenyewe wanyonge na shughuli zao, sasa hivi iingiliwe ikikatwa bila ya matakwa ya wananchi wale. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri, eneo lile walilopewa japo kuwa limetolewa kisheria kama yale makubaliano yaliyokubaliwa hayafanywi pale lile eneo mara moja lifutwe wapewe wenyewe walime. Ardhi tangu hapo hatuna, na ile tuliyonayo kidogo ikichukuliwa wakapewa watu kwa mambo yaliyokuwa hayana maana si

vizuri. Mhe. Waziri, namuomba atuonee huruma kama anavyotwambia kuwa Wilaya ya Micheweni ni wilaya yenye umasikini unaokithiri, lakini leo kuwa tunafanyiwa vituko kama hivi, huku ndio kuendeleza MKUZA.

Mhe. Waziri, namuomba migogoro hii inayojitokeza ya ardhi aifuatilie Mwenyezi Mungu atamsaidia ili haki za wanyonge zipatikane, ili wananchi waweze kufanya shughuli zao za kilimo na kujitafutia riziki maana ajira hakuna. Lakini hata hiyo ardhi ndogo waliyonayo wanyang'anywe, ina maana serikali haiwaonei huruma wananchi hata kidogo.

Kwa sababu haiwezekani ukiangalia humu mote watu pengine washapanda vilimo vyao lakini kwa ajili ya ukubwa wa mtu fulani tu, kwa sababu ya kupata kitu chochote tu, pengine wakaondolewa watu wale masikini hawafikiriwi, ahangaishwe mtu miaka mingapi anakwenda kwenye kesi pengine anashtaki anadhalilika mtu na watoto. Mhe. Waziri, tunamuomba na kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma, itapofika kipindi cha bajeti masuala haya yote yawe yashapatiwa ufumbuzi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia machache katika ripoti hii. Pia, nimshukuru Mhe. Spika, kwa kuniteua kuwa Mjumbe wa Kamati hii. Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyosema historia kwamba ardhi kabla ya Mapinduzi ilikuwa ikimilikiwa na watu wachache, lakini vile vile, ni ukweli usiofichika kwamba Mapinduzi ya mwaka 1964 yameleta usawa na kutoa fursa ya matumizi ya ardhi kwa wananchi wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, sheria nyingi zimetungwa toka wakati wa kikoloni na sheria mbali mbali zimetungwa baada ya Mapinduzi kwa lengo la kusimamia ardhi hiyo. Kufuata sheria ni jambo muhimu sana, pia ardhi imewekwa kwenye maeneo matatu, maeneo ya kilimo, maeneo ya makaazi na maeneo ya uwekezaji, kinyume na hayo ni ukiukwaji wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Sheria ya Ardhi na Haki ya Matumizi ya ardhi, *right of occupancy* ambayo kwa mujibu wa kifungu cha 24 kuwa Mzanzibari atastahiki kupewa ardhi moja ya kilimo na mbili za makaazi kwa mujibu wa masharti ya sheria hiyo.

Pia, kuna sheria ya ukodishwaji wa ardhi kwa uwekezaji wageni na wenyeji, *land lease*. Sheria zote hizi zinampa mamlaka Waziri kufuta kwa kufuata sheria. Kifungu cha 48 cha sheria hii inasema kwamba, anaweza kufuta kwa mamlaka aliyokuwanayo waziri kwa kutoa *notice* ya siku 90 kabla ya kufuta eneo husika.

Mhe. Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba iwapo tutazifuata sheria migogoro hii itaondoka, la muhimu sana Mhe. Mwenyekiti, ni wananchi kuelimishwa kuhusu dhana ya ardhi kuwa ni mali ya serikali, kwani nimeshuhudia wananchi kulalamika kwamba ardhi wamerithi kwa wazazi wao.

Mhe. Mwenyekiti, sheria ya kukatika mkataba wa kodi kifungu nambari 48(1) kinachosema kwamba, Kodi ya ardhi ya umma haitokatishwa isipokuwa kwa hali zifuatazo:-

- Kwa kushindwa kukamilisha uendelezaji ndani ya kipindi cha miaka 30 kuanzia tarehe ya kukodishwa.

- Kushindwa kuendeleza kwa mujibu wa mpango wa uwekezaji ulioidhinishwa na *ZIPA* au mamlaka husika.

Mhe. Mwenyekiti, kwenda kinyume na haya kwa kweli ni kuvunja sheria na kama Mwenyekiti wangu alivyosema kwamba sasa ni lazima tuzifuate sheria hizi za ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nishukuru sana kwamba na mimi nilikuwa ni mmoja katika Wajumbe wa Kamati hii, kwa kweli tulifanya kazi kubwa kwa uadilifu na leo tumeifikisha hapa ripoti hii na nashukuru sana kwamba sheria hii sasa hivi iko mezani na inachangiwa na watu wengi. Mhe. Hamza Hassan Juma, aliyeanza kuchangia hapa kwa kweli amesema kuwa kaipokea kwa mikono miwili na nishukuru kwa hilo.

Kwa sababu tulikuwa tunasikia mengi kwamba sheria hii iwapo itakuja hapa haikutosheleza basi Wajumbe wasingeipokea na ingechanwachanwa hapa hapa, lakini nashukuru kwamba imepokelewa kwa mikono miwili na hilo kwa upande wangu nitoe shukurani kwa Wajumbe kwa wanaoichangia na vile vile wengine wataoendelea kuichangia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sheria ni muhimu na vile vile sheria ili itekelezeke basi kuwe na kanuni. Kwa hivyo, niseme kwamba kwa kuwa ripoti hii ni ya Kamati Teule iliyoteuliwa na Mhe. Spika, na mna mengi humu ambayo yameelezwa katika ripoti hii, basi nisingekuwa na mengi ya kuzungumza kwani hii ripoti imekamilisha kila kitu ndani yake.

Kwa hivyo, nashukuru sana na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani, ingawa kama alivyosema jirani yangu hakuna migogoro ya ardhi katika Jimbo la Amani, lakini kwa niaba ya wananchi wa nchi hii naomba kuunga mkono ripoti hii, na pia nawaomba wenzangu waiunge mkono ili

tuweze kuendeleza ule wajibu wetu wa kuunga mkono mambo mbali mbali yanayoletwa katika Baraza letu hili tukufu.

Baada ya hayo machache nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii nami niishukuru Kamati hii inayoshughulikia mambo ya ardhi na kuipongeza kwa kazi nzuri ambayo wameifanya chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ali Mzee Ali, ripoti ambayo kwa namna moja au nyengine imekidhi haja ile ambayo imekusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, umekuwa ukitafuta Wajumbe wa kuichangia hii ripoti, maana kama ni mvuvi kule baharini basi unaburuza ule mshipi ili angalau wale samaki wanase. Kwa sababu hakuna samaki wengi kule kwenye vidimbwi. Kwa hivyo, unajaribu kuburuza mshipi angalau samaki anase.

Mhe. Mwenyekiti, unajua ripoti hii ni nzito na ni ripoti inayohusiana na jambo zito suala la ardhi. Suala la ardhi ni kubwa si kwa hapa kwetu tu karibu ulimwengu mzima. Sasa suala kama hili katika nchi kama zetu za kimasikini linakuwa na matatizo zaidi kwa sababu ya umasikini wetu na wale wenye uwezo wanatumia fursa ya uwezo wao kuwabana wale ambao hawana uwezo.

Kwa hivyo, wanatumia kila aina, kila mbinu kuhakikisha kwamba ardhi ile wanaichukua wao na wale wanyonge sasa wanabaki kulalamika na wakati mwengine hata hizo sheria za ardhi ambazo Mwenyekiti amesema hapa tokea mwaka 1964, takwimu sikuziweka vizuri wakati wa utangulizi wake kuna sheria karibu 17 za ardhi amesema, lakini inafika pahala sheria hizo watu wanazifumbia macho na hata ripoti hii imeonesha hivyo baadhi ya hadidu rejea.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni ripoti ya nne ya Kamati Teule ambayo Baraza lako tukufu hili limekuwa likiunda na kutoa miongozo mbali mbali ikiwemo Ripoti ya Kamati Teule ambayo nilikuwa naiongoza mimi ya Baraza la Manispaa, lakini hata na Kamati Teule ambayo tumeijadili katika Baraza lililopita iliyoshughulika na masuala ya umeme na nyengine ambazo zipo.

Lakini Waheshimiwa Wajumbe, wamekuwa sasa ni wazito kuzungumzia juu ya ripoti hizi, na kutokana na *reference* ya ripoti zile zilizopita, kwamba ripoti zimekuwa zikifanya kazi kwa nguvu kubwa na kuleta mapendekezo yake hapa lakini utekelezaji sasa umekuwa ni tatizo.

Sasa hili Mhe. Mwenyekiti, limefika pahala sasa Wajumbe wako wamekuwa wanakata tamaa, na kwa sababu ripoti hizi mara nyingi zinakuwa zinawagusa baadhi ya watu lakini ripoti zimekuwa zikizungumzia uwazi juu ya mambo yale, lakini serikali imekuwa haichukui zile hatua stahiki ambazo Wajumbe wako watakuwa wanaridhika na hatua zinazochukuliwa, kinachoonekana ni kujenga uhasama tu kati ya Wawakilishi na baadhi ya watu wanaotuhumiwa, lakini kwa kweli kunakuwa hakuna zile hatua thabiti ambazo zinachukuliwa.

Sasa athari yake ni hii moja; kwamba wasimamizi wa serikali, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanapofika pahala wakakata tamaa basi ni hatari, kwa sababu inafika pahala hakuna mtu wa kuiambia serikali, mwishowe serikali itakuwa inakwenda hakuna msimamizi, hakuna wa kuiambia kitu, waliopewa dhamana na jukumu la kuiambia serikali, kuikosoa, kuiagiza wameshakata tamaa. Huo sasa unakuwa ndio mwisho wake.

Nakumbuka Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe niliwahi kutoa kauli wakati nikichangia Ripoti ya *ZECO*, kwamba hatutounda tena Kamati Teule mbali ya hizi zilizopita. Kwa sababu imekuwa sasa tunatumia fedha nyingi za umma, kwa vile kuunda kamati teule si kitu cha mchezo, tunatumia gharama kubwa kwa sababu haziendi tu kamati hivi hivi, lakini sasa *impact* yake inakuwa haionekani na mwisho wa habari mambo yanakuwa ndio kama hivi.

Kwa hivyo, mimi niiombe sana serikali katika hili, katika masuala kama haya yanayogusa jamii basi tuache muhali, pale ambapo pendekezo linatolewa na chombo hiki basi ionekane kuna hatua zinazochukuliwa na wananchi waridhike juu ya hatua hizo, lakini vyenginevyo tutafika pahala kutakuwa hakuna hata kitu kimoja kinachoonekana kufanyika.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi niipongeze kamati, nimpongeze Mwenyeki kwa kazi nzuri waliyoifanya na kwa kufuata hadidu rejea ambazo wamepewa, nimeona humu ripoti hii wameigawa katika maeneo makubwa matatu.

Mhe. Mwenyekiti, alianza na historia fupi juu ya suala la ardhi Zanzibar, najua ni mtu wa historia ameeleza mengi ambayo wengine hatuyajui, lakini pia ameeleza ahadi ya Chama cha *Afro* Shirazi kuhusu ardhi, kama tunavyojua kwamba Chama cha *Afro* Shirazi ndicho kilicholeta Mapinduzi hapa.

Kwa hivyo, kwenye *manifesto* zake kumekuwa na ahadi nyingi kuhusiana na masuala ya ardhi na jinsi gani sasa ahadi zile zinasimamiwa, wapo wanaozisimamia kwa udhati. Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alizisimamia kwa udhati na akaigawa ardhi ile eka tatu tatu kwa wanyonge,

lakini matokeo yake sasa hivi wametokea watu wengine wanachukua maeneo makubwa tu, mtu anachukua eka 30 wengine hawana kitu, kwa hivyo imetuelezea hivyo.

Lakini pia, ametuelezea juu ya hadidu rejea namna walivyozishughulikia. Ripoti imepangika wameshughulikia vizuri, mapendekezo ni mazuri, maoni ni mazuri. Kwa hivyo, mimi Mhe. Mwenyekiti, nayaunga mkono na kuiomba serikali hasa Mhe. Waziri aifanyie kazi ripoti hii.

Pengine atakapoifanyia kazi ripoti hii kwa muda uliowekwa na Waheshimiwa Wajumbe wakaridhika na utekelezaji wa ripoti ile labda wanaweza kurejesha imani hasa katika maeneo haya. Nimuombe sana Mhe. Waziri, na Mhe. Waziri, ni mtu anayesikia, mtu muadilifu, kipindi chake kifupi alichokaa amefanya shughuli nzuri. Hivyo, naamini kwamba ripoti hii ataifanyia kazi kupitia kila hadidu rejea ambayo ipo. Mapendekezo ya Kamati na mapendekezo ya Baraza.

Sisi kama Baraza la Wawakilishi tunaikubali ripoti hii na tunaiunga mkono na tunaiomba serikali sasa ianze kuchukua hatua na baadae watupe *feedback* juu ya utekelezaji na maoni na hatua zile ambazo zimechukuliwa itakuwa ni kitu muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia ripoti fulani hapo nyuma Mhe. Mwenyekiti, ana kumbukumbu na ripoti hiyo nilisema kwamba ardhi, suala la ardhi ni suala zito na hata katika kitabu kitukufu cha *Quruan* kimesema. Mwenyezi Mungu amesema kwamba "ardhi na mbingu ni yangu, musigombanie", na aliyejua. Ilitoka kauli hiyo kwamba akijua kwamba wanadamu sasa wakifika kule chini wataanza kugombania. Na hilo ni jambo ambalo tumeaswa tusilifanye, tusigombanie ardhi, ardhi yote ni ya mwenyewe Mwenyezi Mungu.

Lakini leo tunafika pahala tunaanza kugombania, kudhulumiana. Kwa kweli tunakuwa hatwendi vizuri na tunakwenda kinyume na makatazo ambayo tumeaswa na aliyetuumba. Leo utashuhudia ardhi moja au sehemu moja wanapewa zaidi ya mtu mmoja. Kuna mmoja unamkuta tayari ana hati ya kumiliki, lakini ardhi hiyo hiyo anakuja kupewa na mwengine. (*Makofi*).

Sasa kwa kweli huo sio utaratibu mzuri katika kugawana ardhi na tunakaribisha matatizo ya makusudi. Kwa kweli Mhe Mwenyekiti, Mhe. Waziri, tunamuomba sana asimamie suala la ardhi ili ionekane kwamba matatizo haya yanapungua kwa kiasi kikubwa, tunasema hayawezi kumalizika, lakini yatapungua.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo na maoni ni mazuri yaliyotolewa. Kazi imefanyika vizuri. Lililobaki sasa kwetu ni kuona utekelezaji. Kwa hivyo, mimi baada ya maelezo hayo sina zaidi isipokuwa moja ambalo nimeligundua katika ripoti hii na ripoti nyengine, niwasihi sana Wajumbe wenzangu kwenye kamati, humu kwenye ripoti hii imeelezwa juu ya kutakiwa *documents* fulani na kamati na wahusika kuacha kuwasilisha zile *documents* katika kamati inayohusika. Humu wametuandikia tumetaka *documents* fulani, lakini hatukuzipata. Sasa iwe ndio hatukuzipata iwe basi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwamba umetaka *documents* fulani kwa ajili ya kuweka mambo yako sawa, ile *documents* hukuletewa, maana yake ndio basi, ndio utaratibu wa kisheria. Mimi ninadhani katika eneo hili lazima tuwe makini na kwa sababu tunayo ile sheria ya kinga, fursa na haki za Wajumbe. Inaelezea juu ya adhabu ya kupewa kwa mtu ambaye ametakiwa na chombo hiki ama kamati ya Baraza ama Baraza la Wawakilishi kuwasilisha *documents* na kuacha kuwasilisha *documents* ni kosa kwa mujibu wa sheria, na hawa wanatakiwa wachukuliwe hatua.(*Makofi*).

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi ninadhani kwa kuanzia Baraza lako tukufu, maeneo yote ambayo kamati yameomba *documents* kutoka katika taasisi inayohusika na *documents* zile zikawa hazikuwasilishwa katika kamati. Kwa hivyo, kwa kuanzia ripoti hii, katika kila taasisi Mkuu wa taasisi ambaye hakuwasilisha *documents* zinazotakiwa na kamati, maana yake sasa aanze kuchukuliwa hatua za kisheria. (*Makofi*).

Na sheria ile ya haki, fursa na kinga za Wajumbe ianze kufanya kazi. Hili Mhe. Mwenyekiti, ninadhani ni lako. Tuorodheshe taasisi zote zile ambazo zimetakiwa na kamati hii kuwasilisha ripoti na wakashindwa kuwasilisha *documents* zile kwa muda uliotakiwa, waanze kuchukuliwa hatua, aarifiwe Mkurugenzi wa Mashtaka awafungilie mashtaka kwa kosa la kutokuwasilisha *documents* katika chombo hiki, ama katika kamati au katika Baraza. (*Makofi*). Kwa sababu hili ni tatizo. Hili linasababisha sasa hata ripoti zisikamilike, utazikuta ripoti nusu nusu. Mwenyekiti hapa anatueleza tulitaka *document* hii, lakini hatukuletewa, ndio mwisho wa habari. Sasa hatutaki kwamba iwe mwisho wa habari. Sasa hatua zichukuliwe dhidi ya wote waliotakiwa kuwasilisha *documents* katika kamati na wasiwasilishe. (*Makofi*).

Kwa sababu hii kufanya hivi inaonekana ni kukidharau hiki chombo na sisi hatupo tayari kudharauliwa. Sisi sote hapa tumechaguliwa na wananchi kupitia majimbo yetu na waliochaguliwa na Rais, sote tupo hapa kwa ajili ya kuwakilisha wananchi. Kwa hivyo, hatupo tayari kudharauliwa. Chombo hiki kipo kwa mujibu wa sheria na Katiba na kinaendeshwa kwa mujibu wa taratibu zote na ndio maana tukaweka kifungu hicho kwamba *documents*

zinazotakiwa na kamati au Baraza ikiwa haikuwasilishwa basi ni kosa la jinai na adhabu yake ipo.

Kwa hivyo, kutokuwasilisha, maana yake ni dharau kuonekana kwamba aah! hakuna hatua zozote na mitindo hii inaonekana ipo hata katika kamati zetu za kawaida. Kamati inaweza kutaka mkataba, tunataka tuletewe taasisi inayohusika tuleteeni mkataba fulani, basi hauletwi. (*Makofi*).

Mimi wakati mmoja nilipokuwa mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, nilitaka Wizara ya Fedha wakati ule haijabadilishwa Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma, kupitia kamati yangu, tuliomba mkataba wa ujenzi wa ukodishwaji wa Mambomsiige. Basi tukiitaka mara ya kwanza hatujaletewa, mara ya pili hatujaletewa, aah!

Mimi nikamwita yule Mkurugenzi, nikamwambia hivi unajua kwamba kutokuwasilisha *document* hiyo katika kamati ni kosa kwa mujibu wa sheria, unajua hilo. Akaniambia ninajua. Sasa nikampa muda, ikifika muda fulani *document* hiyo hujaiwasilisha kwenye kamati yangu, maana yake sasa unastahiki kufunguliwa mashtaka kwa mujibu wa kifungu cha sheria kilichopo.

Bahati nzuri haikufika ile siku akaniletea *documents* zote. Sasa haya tukiacha yaendelee, maana yake kwanza yatakwaza muendelezo wa shughuli zetu, lakini pili inaonesha kwamba ni dharau katika utekelezaji wa shughuli hizi za umma. Kwa hivyo, hili Mhe. Mwenyekiti, kwa Baraza, Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati Teule ambaye ameshughulikia hili, hili tusilifumbie macho.

Maelezo mengi humu ukiyasoma yanaonesha kwamba kuna *documents* hazikupatikana. Kwa mfano kuna malalamiko ya huyu ndugu anaitwa Ali Mradi, sijui ambaye ardhi yake ilichukuliwa, kukawa kuna maelezo tofauti, imechukuliwa ardhi yake akapewa mtu mwengine. Sasa kila Waziri anakuja anasema maelezo yake. Kuna mwengine anasema hii ardhi tuliitoa kwa makosa, lakini tayari ilikuwa kishapewa mtu mwengine.

Kwa hivyo, tunakuomba hii ardhi..., sasa hebu tupeni hiyo *document* ambayo inaonesha kwamba huyo mtu mwengine alipewa, si unasema alipewa mtu, kama alipewa mtu maana yake si kulikuwa kuna *document* inaonesha kama alipewa. Sasa basi tuleteeni hiyo *document* inaonesha kwamba ardhi hii alipewa mtu fulani, tukakupa wewe kimakosa, hata hili nalo linakuwa ni gumu. (*Makofi*).

Inaonekana pana lugha ambazo Mhe. Mwenyekiti, si za ukweli ndio maana inashindikana. Kwa hivyo, mambo kama haya Mhe. Mwenyekiti, si mambo

ya kuyafumbia macho, si mambo ya kuoneana muhali, lazima tusimamie chombo hiki kiukweli na kwa sababu tupo hapa kwa masuala haya ambayo wananchi wenyewe wanatutegemea sisi na sisi ni viongozi, tumepewa jukumu la kusimamia mambo haya.

Kwa hivyo, lazima tufike pahala tuwe wakweli, tusifike pahala tukawa tena tunababaisha-babaisha umma, kila jambo linahitaji kwenda kwa ukweli na uwazi. Unapotoa maelezo yako, ikitakiwa *document* ilete *document* hiyo, basi wasilisha *document* inayohusika. Vyenginevyo, utakuwa unatoa lugha ambayo si ya ukweli na hatua sasa za kisheria inabidi zichukuliwe dhidi ya wale wote wanaoambiwa walete *documents* wakawa hawaleti. Kwa hivyo, hatua za kinidhamu na kisheria zichukuliwe dhidi ya wote. (*Makofi*).

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, ninasema ninakubaliana na ripoti hii na niombe serikali sasa ianze kuichukulia hatua kwa mapendekezo yote yale ambayo yamewasilishwa. Na hawa wote waliotajwa kuwasilisha *documents* katika kamati inayohusika, basi wasiwasilishe, basi taasisi hii nayo ichukue hatua ya kisheria dhidi ya watu hawa waliokuwa hawakuwasilisha hizo *documents*.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja na niwapongeze wote walioshiriki.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Salmin Awadh Salmin, majadiliano yanaendelea. Sasa tunampisha Mhe. Asaa Othman Hamad.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia na wenzangu kutupa neema ya uhai na uzima tukaweza kufika jioni hii kuendelea na shughuli zile ambazo wananchi wametutuma.

Mhe. Mwenyekiti, niungane na wachangiaji wote waliofika kuipongeza kamati chini ya mwenyekiti wake Mhe. Ali Mzee Ali, kwa kazi nzuri waliyoifanya iliyotupa matumaini na kutaka kuzusha changamoto kwa Wazanzibari. Lakini hata wale ambao wanaumwa na dhulma inayoendelezwa na wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti, ningependa nianze pale alipopaachia mwenyekiti wangu Mhe. Salmin Awadh Salmin. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi, hebu tuachane na kunung'unika. Mambo mengine tunajitakia wenyewe. Sisi ni Wawakilishi wa wananchi.

Wananchi kwa Katiba tuliyonayo ndio wenye mamlaka na madaraka ya nchi hii. Wananchi hao wametuchagua sisi na sisi hapa tupo kwa niaba yao. Sasa wenye mamlaka wametutuma, sisi tunakuja kuilalamikia serikali iliyoekwa na hao waliotutuma sisi ili tunategemea serikali itunge sheria ya kujitia kitanzi wenyewe.

Sisi tunayo mamlaka ya kupeleka mswada wa sheria, ni vipi Baraza hili likataliwe, watungaji ni sisi wenyewe na tuweze kuidhibiti serikali katika hili. Mabaya yote haya tunayoyazungumzia yanatendwa na watendaji wa serikali na watendaji hao ndio wanaokaa wakaleta miswada, hivi wanaleta miswada inayowadhibiti wao wenyewe. Hebu tujiulizeni.

Sasa tuacheni na masuala ya kulalamika, tufanyeni kazi tuliyotumwa, kama hatuwezi hivyo, tutaendelea kusema tunaishauri, tunapendekeza, tunaiomba, tushaomba sana. Hizi kamati wenyewe tunafahamu hii ni ya nne, sijui ya nane, hakuna lolote na halitokuwa lolote kwa sababu hatujataka liwe, Wawakilishi wenyewe hatujataka serikali iwajibike, bado tunasimama kuishauri pasipokuwa na lazima ya kushauri, tunaiomba hakuna sababu ya kuomba, mtu kadhulumu, unamuomba kitu gani, ni hukumu tu. Taratibu za sheria zifuatwe na adhabu inayostahiki ichukuliwe. (*Makofi*).

Leo unasema unamuomba, leo unamshauri na anayeshauriwa hataki. Ninadhani wenyewe tuna kumbukumbu nyingi ya Kamati Teule. Ni ipi iliyochukuliwa hatua, hivi serikali haisiki na hivi serikali haipo. Sasa tusimameni tufanye shughuli moja. Hivyo, wananchi hawa wafahamu kwamba Wawakilishi wao wanatuwakilisha kusimamia na kudai haki zetu.

Hapa tunasimama kwa unyonge unyonge vile kama tumekuja kuazima nafasi serikalini, sisi hatuja kuazima nafasi hapa. Sisi tumeletwa na wananchi na wao ndio wenye mamlaka na madaraka yao. Sasa tunachoshauriana ni kitu gani. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari wataendelea kumkumbuka Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume. Historia, watoto wetu na wajukuu itawashangaza. Lakini pia niseme malengo na madhumuni ya *Afro*-Shirazi, chama kilichowakomboa wanyonge wa visiwa vya Unguja na Pemba. Wazanzibari wataendelea kuikumbuka *Afro*-Shirazi na malengo yake na watajiuliza leo wamejikwaa wapi. (*Makofi*).

Afro-Shirazi Mhe. Mwenyekiti, ndio iliyoleta mapinduzi ya nchi hii. Malengo ya mapinduzi, ninashukuru sana Mwenyekiti na kamati hii wametoa historia

inatosha. Wazanzibari kufahamu walikotoka na wajiulize leo wapo wapi na hatma ni ipi kama *trend* ni hii.

Mhe. Mwenyekiti, Sheikh Abeid Amani Karume aliona umuhimu wa Muafrika wa Zanzibar kujitawala, kutawaliwa ni unyonge. Mhe. Mwenyekiti, na ndio akasema itakapokamata madaraka Afro-Shirazi, ardhi ya Zanzibar ni bure na itakuwa ni mali ya serikali. Maana aliyokusudiwa sio bure hii inayofanywa leo na wenzetu. Ni bure kwa maslahi ya Mzanzibari. Ni bure kwa faida ya wananchi wote. (*Makofi*).

Leo Mhe. Mwenyekiti, baada ya mapinduzi, ahadi ile ya *Afro*-Shirazi ilitekelezwa chini ya uongozi wa Mzee Abeid Amani Karume. Wasiomiliki ardhi wakati ule waligaiwa eka tatu tatu, kila mwananchi awe na sehemu ya kuishi na sehemu ya kulima ili aweze kuishi ndani ya nchi yake bila bughdha. (*Makofi*).

Bahati mbaya sana kuna wenzetu mapinduzi yale kwao yalikuwa kumbe itafsirike vibaya. Tafsiri si kuwakomboa kumbe Wazanzibari wanyonge na maskini. Wamefanya kwamba ni *transparency of powers*. Waliowaonea choyo wakoloni wale. Sasa kuna wakoloni wengine weusi ndani ya Zanzibar hii, weupe hawapo, tumekuwa sisi kwa sisi.

Mhe. Mwenyekiti, bora adui asiyekujua kama yule anayekujua. Maumivu yake yanatofautiana. Ndugu yako akikufanyia ubaya unaumia mara tatu au tano zaidi kuliko kufanyiwa na mgeni. Hivi Mhe. Mwenyekiti, tukijiuliza iweje leo, *inshaallah* kesho tuna sherehe za miaka 50 ya mapinduzi hayo tunayosema, ndio yaliyoleta utu na heshima ya wananchi wa nchi hii.

Unamdhulumu mwananchi huyu huyu ambaye alitarajia kesho na yeye aikumbuke siku ile ya tarehe 12/01/1964. Afanye tathmini na yeye namna alivyonyang'anywa ardhi yake na iliokuwepo ya wazazi wake, lakini leo ananyang'anywa na Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Salmin Awadh Salmin na Mhe. Asaa Othman Hamad, huyu huyu.

Mhe. Mwenyekiti, kama hatukuwa wakweli na hatujataka kumuogopa Mungu. Ninawaomba Waheshimiwa, turudi bado nafasi tunayo, dhuluma haidumu na ikidumu ni nakama. Nawaomba wale wenzetu waliojifanya walafi, wanakula kwa mikono miwili, wasije wakainakamisha nchi hii. Kuna watu hawana makosa yoyote ni watoto wachanga, wazee ambao wanahitaji msaada mkubwa wa serikali hii na watoto wao. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kuna mabaya mengi yameshafanyika na mimi nasaha yangu kubwa sasa kwa Baraza lako Tukufu, sitaki niiseme tena serikali,

serikali haitaki kusikia. Ninadhani tusiendelee tu kupiga makelele. Ni lini Wajumbe wa Baraza hili watahakikisha kwamba serikali inatekeleza majukumu yake. Ni vipi serikali inakwenda kwenye ule mstari wake. Serikali imechukua dhamana hii.

Wananchi hawa haki zao zisimamiwe na serikali hii. Ripoti imetoka ya Kamati yako ya Baraza lako tukufu. Hebu tusemeni sasa kwamba tunataka serikali ichukue hatua na serikali kama haitaki tusiseme tu, tunapokuja kuichangia bajeti Mwenyezi Mungu akitufikisha salama, *inshaallah* atatufikisha kama nia ni njema, tuna nia ya kuwatetea watu wa nchi hii, tuna nia ya kusimamia haki zao, Mwenyezi Mungu atatufikisha tuone Wawakilishi wako watafanya nini juu ya serikali, kama serikali haikuchukua hatua yoyote, kwa sababu imani yangu ni vigumu sana serikali kuchukua hatua hapa. (*Makofi*).

Ninavyoamini mimi na kama sivyo *inshaallah* tutafika tuone ni serikali itachukua kweli hatua. Sisi kwa sheria ziliopo hatuwezi kumpeleka mtu Mahakamani, lakini sasa mwanzo wa kuwapa hao wanaostahiki kazi ya kufanya tumeshakuwa nayo ni hii hapa. Ni taratibu tu sasa zifuatwe ili wale wote waliostahiki wamevunja sheria za nchi tumezitunga sisi hapa, wamewadhulumu wananchi kwa kutumia madaraka yao mabaya.

Nimeona majina hapa ya wenzetu wengine tunao humu ndani, lakini kamati bado pamoja na sifa tunazozisifu inazungukazunguka. Mhe. Mwenyekiti, bado watu wanadhulumiwa ardhi zao, waliopewa kwa haki za kisheria zinafutwa, watu wanapeana wanavyotaka wenyewe. Hilo zoezi bado lipo Mhe. Waziri, unanisikia.

Ni imani yetu kwako ni kubwa, umetoka mbali, ni muasisi wa Baraza umetajwa. Lakini tunakwambia, safari tunayokwenda ni ngumu sana inahitaji uaminifu na uadilifu mkubwa. Lakini mwenyewe kwanza ukisimama kwenye mstari, Mwenyezi Mungu atakusaidia. Sina wasi wasi na wewe, nina wasi wasi na waliokuzunguka.

Mhe. Mwenyekiti, bado tuna kazi kubwa na tuna dhima nzito kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii ya kumsaidia Mhe. Waziri. Mhe. Waziri, tutakusaidia utakapohitaji msaada wetu, lakini tutataka na serikali ituoneshe kwamba inataka msaada wetu na pale tutakapohisi kwamba serikali ni yale yale, Waheshimiwa Wajumbe wajibu wenu na nyinyi ni kuidhibiti serikali iliopo madarakani, uwezo munao, uwezo mumepewa wa Katiba na sheria, hapana kutizama mtu machoni katika hili. Kila mmoja kati yetu atakwenda kujibu kwa wakati wake, ninajaribu kukumbusha hilo.

Masheikh, Maimamu na Maamuma mutajibu, mukipenda musipende mutajibu. Ukicheka sana leo umefurahi kwa dhuluma, utakuja kulia sana siku hiyo. Mpe mwanao, mpe dada yako hiyo ardhi, mpe mjomba wako, mpe mkweo almuradi sio yako, itatoka ndani ya mifupa yako. Furahia tu, kilio ni kikubwa mno. (*Makofi*).

Sasa Waheshimiwa Wawakilishi kujiepusha na hilo, tutende wajibu wetu. Serikali haitaki kuchukua hatua, tuchukue hatua sisi wenyewe, ikija serikali hapo itakuwa umetenda wajibu na umejiosha. Waionea, ni serikali yangu, ni serikali ya nani, hakuna serikali yako, sote ni yetu. Hii ni Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, sote ni Wazanzibari; kama ni mweupe, mwekundu, kijani, wewe ni Mzanzibari. Mwenyezi Mungu ametofautisha kwa rangi tujuane, makabila yetu na tumepeana majina, hiyo ndio tofauti si nyengine, hakuna ubora katika hilo. (*Makofi*).

Kesho akiwa Mhe. Hamza Hassan Juma, ana ridhaa ya Wazanzibari, nitaendelea kumuheshimu, lakini akifanya makosa lazima aambiwe. Na Mhe. Hamza Hassan Juma, ikifika zamu yangu lazima akubali, tumekubaliana hivyo, sio Katiba yetu inavyosema. Sasa sio kwamba kuna dhambi inatendeka, ni serikali yangu na ni chama changu. Chama anakitia madoa huyu lazima tumwambie hufai ondoka, chama gani kitakachodhulumu tukanyamaza kwa kuwa ni chama chako, hakuna hilo. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, tunataka uaminifu na uadilifu, tumeaminiwa, tusilindane kwa kupeana majina ya vyama, halipo hilo. Vyama vitakuja na kumalizika na Zanzibar itaendelea kuwepo. Tunataka tuwaridhishe wananchi wa nchi hii, kizazi cha Wazanzibari, salama, amani na utulivu endelevu. Zanzibar na sifa yake tunataka irudi, acheni kuiharibu kiasi kwa kutumia mamlaka na madaraka musiyopewa, hamjapewa kuvuruga watu kiasi hichi. Watu wanachukiana kwa dhuluma tu. Serikali ipo inanyamaza. Viongozi munasaidia dhuluma, mupo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nasaha yangu kwa Waheshimiwa Wawakilishi, mulioshiriki munajijua wenyewe mikoani na mawilaya, munashirikiana na Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa na leo na Masheha munawadhulumu watu bure. Mumekula kiapo pale kwa dini zenu wenyewe. Halafu mnasimama mnadanganya, mnapiga kelele sana msikilikane kwenye vyombo.

Lakini mujiulize hivi Mwenyezi Mungu hatuoni tunayosema. Ninawaombeni sana Waheshimiwa turudini. Ni sifa ya binadamu kukosoa, lakini Mwenyezi Mungu kaweka mlango wa kurudi tumuombe samahani na yupo tayari kutupokea. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ninataka niseme la mwisho. Zanzibar ya miaka 45 iliyopita tumeivuruga, tuna kazi ya miaka 50 kuifunika. Tumeharibu mila na desturi. Mzanzibari akiogopa hata ile senti aliyoiokota kwenye ghafla yoyote ile, akiipeleka Polisi, ama pale redio au televisheni, anaogopa dhambi ya dhuluma anaogopa.

Leo kila mbinu ana uwezo wa kuifanya na hata rushwa yupo tayari almuradi ikamilike. Mhe. Mwenyekiti, nasaha yangu kwa Waheshimiwa Wawakilishi, ndugu zangu ninakuombeni tufanye wajibu wetu na kazi tuliyotumwa na wananchi. Na kwa Serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyopatikana kwa jasho kubwa la Chama cha *Afro-Shirazi Party* na kuja kurithiwa leo na Chama cha Mapinduzi, malengo na madhumuni ya *Afro*-Shirazi ilipoomba ridhaa, sio haya ya leo, tusikipake tope. *Afro*-mama tumeiaga wala haikutufanyia lolote baya.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Asaa Othman Hamad, kwa mchango wako mzuri na mahiri sana.

Waheshimisa Wajumbe dakika tulizonazo ni chache mno na hapa nina wachangiaji watatu waziada. Sasa ninahisi kwamba bora tutoe fursa hii tujuane ili kesho asubuhi baada ya kipindi cha maswali na majibu tuweze kuchangia, lakini wakati huo huo upande wa mawaziri pamoja na mwenyekiti kule watakuwa na wao wameshajiweka tayari kwa ajili ya kumalizia, mara baada ya michango hiyo.

Waliobakia kwa sasa ni Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, pamoja na Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa. (*Makofi*).

Baada ya maelekezo hayo sasa, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru sana kwa namna tulivyoshirikiana kwa pamoja hadi kufikia hapa na *inshaalla* kesho tutamuomba Mhe. Naibu Spika, ili aendelee na sisi wengine tuweze kuchangia.

Mhe.Mwenyekiti: Ninachukua fursa hii kuakhirisha Baraza hili hadi kesho siku ya Jumatano saa tarehe 18/12/2013 saa 3.00 asubuhi.
Naomba kuahirisha.

(Saa 1.35 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 18/12/2013 saa 3.00 asubuhi)